ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI
ZANZIBAR
MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Hamad Masoud Hamad	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ole.
9.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge
10.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa
11.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa
12.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Gando
13.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Kuteuliwa.
14.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Jang'ombe
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la Makunduchi
18.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Kiembesamaki
19. Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu
22.Mhe. Issa Haji Ussi	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka

23.Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
29.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
30.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
31.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini
32. Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa
33. Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
34.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
35. Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
36.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
37.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
38.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
40.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
42.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
43.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
44.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
45.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
46.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
47.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
48.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Jimbo la Kikwajuni
49.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
50.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa	Jimbo la Mkwajuni
51.Mhe. Mgeni Hassan Juma	Nafasi za Wanawake

52.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma Jimbo la Bumbwini

53.Mhe. Mohammed Haji Khalid Jimbo la Mtambile

54.Mhe. Mohammed Mbwana Hamad Jimbo la Chambani

55.Mhe. Mohammed Said Mohammed Jimbo la Mpendae

56. Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak Nafasi za Wanawake

57.Mhe. Mussa Ali Hassan Jimbo la Koani

58. Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali Jimbo la Uzini

59.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa Nafasi za Wanawake

60.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi Nafasi za Wanawake

61.Mhe. Nassor Salim Ali Jimbo la Rahaleo

62.Mhe. Omar Ali Shehe Jimbo la Chake-Chake

63.Mhe. Panya Ali Abdalla Nafasi za Wanawake

64.Mhe. Rashid Seif Suleiman Jimbo la Ziwani

65.Mhe. Raya Suleiman Hamad Nafasi za Wanawake

66.Mhe. Rufai Said Rufai Jimbo la Tumbe

67.Mhe. Saleh Nassor Juma Jimbo la Wawi

68.Mhe. Salim Abdalla Hamad Jimbo la Mtambwe

69.Mhe. Salma Mohammed Ali Nafasi za Wanawake

70.Mhe. Salma Mussa Bilali Nafasi za Wanawake

71.Mhe. Salmin Awadh Salmin Jimbo la Magomeni

72.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman Nafasi za Wanawake

73.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha Jimbo la Mwanakwerekwe

74. Mhe. Shawana Bukheti Hassan Jimbo la Dole

75.Mhe. Subeit Khamis Faki Jimbo la Micheweni

76.Mhe. Suleiman Hemed Khamis Jimbo la Konde

77.Mhe. Ussi Jecha Simai Jimbo la Chaani

78.Mhe. Viwe Khamis Abdalla Nafasi za Wanawake

79.Mhe. Wanu Hafidh Ameir Nafasi za Wanawake

Ndg. Yahya Khamis Hamad Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha Kumi na Mbili – Tarehe 16 Aprili, 2012

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (Pandu Ameir Kificho) alisoma Dua

HATI YA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii: Mhe. Spika, naomba kuwasilisha mezani hati ya ripoti ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii, naomba kuwasilisha.

Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha mezani ripoti ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, naomba kuwasilisha.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, kabla hatujaendelea na maswali, kuna wageni waliofika katika ukumbi wetu kama kawaida. Waheshimiwa Wajumbe, wananchi wetu wamekua wanapendelea sana kuja ili kuona shughuli zetu tunavyoendesha na namna tunavyowatengenezea masuala na mambo yao yanayowahusu wananchi wetu.

Kwa hivyo, kwa leo naomba Waheshimiwa Wajumbe niwatambulishe kwenu wageni wetu, vijana wetu wanafunzi kutoka skuli ya maandalizi ya Alkhamis Camp kule Pemba. Nawaomba wanafunzi hao na walimu wao wanyanyuke ili wajumbe wawasalimie, wale pale. *(Makofi).*

Ahsanteni sana wageni wetu tunawashukuru karibuni sana na ninawapongezeni kwamba mmechukua nafasi, hatua na fursa ya kutoka Pemba hadi hapa Unguja, kuja kuangalia na kusikiliza wazee wenu wanafanya nini, karibuni sana.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 130

Kuzimika Ovyo kwa Umeme

(Mhe. Mjumbe aliyetaka kuuliza swali hili ameliondoa).

Nam. 82

Ukosefu wa Mashine za *X-Ray, Ultra Sound Na CT Scan*
Katika Hospitali za Pemba

Mhe. Hassan Hamad Omar – Aliuliza:-

Pamoja na Serikali kufanya jitihada za kua na vifaa kwa ajili ya uchunguzi wa maradhi ya binadamu kama vile mashine za *X-Ray, Ultra Sound na CT- Scan*, bado katika hospitali ziliopo Wete, Chake-Chake na Mkoani inaonekana kuna upungufu wa vifaa hivyo;

(a) Kati ya vifaa hivyo, ni vifaa gani ambavyo kwa sasa vipo na vinafanya kazi katika hospitali za Wete, Chake-Chake na Mkoani.

(b) Serikali ina mpango gani wa kuweka vifaa vinavyokosekana katika hospitali hizo ili kuepusha usumbufu kwa wagonjwa kutoka Pemba kuja kufanya uchunguzi wa maradhi kwa kutumia vifaa hivyo katika hospitali ya Mnazimmoja.

Mhe. Waziri wa Afya – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 82 lenye vifungu (a) na (b) kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Spika, huduma ya kuchunguza magonjwa mbali mbali zinapangwa kwa madaraja ya hadhi ya hospitali husika. Pia vifaa vya kuchunguzia navyo vinawekwa katika mahospitali kwa mujibu wa ngazi na hadhi za hospitali hizo. Lakini si vifaa tu bali hata wafanyakazi wenye fani husika pia nao wanakuwepo katika hospitali kulingana na ngazi za hospitali hizo.

Vifaa kwa ajili ya uchunguzi wa maradhi ya binaadamu kama vile mashine ya *X ray, Ultra sound,* na *CT – Scan* ni katika jumla ya vifaa ambavyo vinawekwa katika hospitali kwa kufuata utaratibu huo, na hivyo ndivyo ilivyo kwenye hospitali zetu.

(a) Vifaa ambavyo vinavyopaswa kua katika hospitali za Wete, Chake Chake na Mkoani ni mashine ya *X-ray* na *ultrasound* ambazo zipo na zinafanyakazi.

(b) Mashine ya *CT – Scan* inapaswa kua katika hospitali ya rufaa nayo ni Mnazi Mmoja ambapo ipo.

Hassan Hamad Omar: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa fursa ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Mhe. Waziri utakubaliana na mimi kwamba hospitali ya Chake Chake wanapiga *X-ray* na *X-ray* hiyo inakwenda kusomwa Mkoani. Je, kama ni hivyo huoni kua ni usumbufu kwa wananchi wetu wengi waliokua masikini.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, ninavyofahamu mimi na nilivyouliza leo asubuhi kwa Afisa Mdhamini wetu, kua Hospitali ya Wete, ya Chake Chake na Mkoani zote zina *X-ray* na zinafanyakazi. Kwa hivyo, sio kweli kwamba imehamishwa kupelekwa Mkoani.

Mhe. Spika: Sijui kama umelipata sawa sawa swali. Anasema kwa mfano, *X-ray* imepigwa Wete au Chake Chake, lakini ile picha inakwenda kusomwa Mkoani, ndicho anachouliza Mhe. Mjumbe hapa, kua huo si usumbufu.

Mhe. Waziri wa Afya: Ni sawa Mhe. Spika, nakubali kua huo ni usumbufu, lakini inategemea na uwezo wa utaalamu tulionao. Yule mwenye kusoma na kutafsiri yuko katika hospitali ya Mkoani na hiyo tunakua nayo kutokana na upungufu wa wafanyakazi. Kwa hivyo, ni usumbufu kweli na tuko katika jitihada ya kutafuta ufumbuzi huu.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Kwa kua hali ya maisha ni ngumu sana kwa wananchi wenye kipato cha chini na kwa kua kila baada ya muda wanaumwa na kulazimika kufanyiwa *X-ray*. Je, isingekua vyema kwa huyo mtaalamu aliyeko Mkoani akawa anazunguka katika hospitali hizi, angalau mara moja kwa siku kwa kila hospitali ili kuondoa usumbufu na makali ya maisha kwa wananchi wetu.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, tumesikia ushauri wa Mhe. Mwakilishi na tutalizingatia hilo. Kwa sababu utaratibu wa madaktari kuzunguka upo kwa pale penye upungufu. Mtaalamu wa maradhi anaweza kua yuko Wete, lakini Mkoani hayupo basi akawa anazunguka. Hivyo hivyo hata kwenye hospitali za vijijini. Kwa hivyo, tutazingatia ushauri wake.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi hii kumuuliza Mhe. Waziri swali moja tu la nyongeza. Mhe. Spika, kabla sijamuuliza napenda nitoe shukrani zangu kwake kwa kuona kwamba kila hali inavyotengenea na yeye anatoa shukrani.

Mhe. Spika, kwa kua vifaa vilivyotajwa hapa hutegemea sana vile vile na kuwepo kwa *ICU* kwa wale waliozidiwa na hususan ni kwamba Pemba ni kisiwa ambacho huna pa kwenda. Je, katika mkakati wa wizara pamoja na kulishughulikia la hospitali ya Mnazi Mmoja, lakini ni lini hospitali moja wapo ya Pemba itapangiwa kupata kifaa hichi cha *ICU*, ili wale wagonjwa wanaozidiwa kwa kungojea matibabu basi waweze kupata huduma hiyo bila ya matatizo.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, ni suala la msingi ambalo tunalielewa umuhimu wa kua na *ICU* Pemba. Moja katika marekebisho makubwa yatakayofanywa katika hospitali ya Mkoani, chini ya msaada wa Serikali ya China ni ICU, kwa sababu tumeona kuna ugumu hata wa kumsafirisha mgonjwa kutoka Pemba kuja Unguja wakati akiwa mahatuti. Ni suala muhimu sana na linahitaji kupewa umbele. Kwa hivyo, tunashukuru kwa kutukumbusha na tutaendelea kulizingatia katika mradi huu.

Nam. 83

Utafiti wa Maradhi ya Moyo, Sukari na Shindikizo la Damu

Mhe. Hassan Hamad Omar – Aliuliza:-

Katika miaka ya hivi karibuni, kumekua na ongezeko kubwa la matatizo mbali mbali ya kiafya hapa Zanzibar yakiwemo maradhi ya Moyo, Kisukari na Shindikizo la damu ambayo yamekua yakiwashambulia hata watoto wa visiwa vya Unguja na Pemba;

(a) Kuna utafiti gani wa kina uliowahi kufanywa na Serikali ili kubaini chanzo cha kuongezeka kwa maradhi hayo.

(b) Kuna mpango gani wa kusambaza matokeo ya utafiti huo wa kina yatakayoweza kuwafikia wananchi wengi wa Unguja na Pemba ili waweze kuchukua hatua za kujikinga na maradhi hayo.

Mhe. Waziri wa Afya – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 83 yenye vifungu (a) na (b) kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Spika, nakubaliana na Mhe. Mjumbe kwamba maradhi yasiyo ya kuambukiza (*NCD*) yaani *Non Communicable Diseases* yamekua yakiongezeka siku hadi siku na kusababisha maisha ya watu wengi kupotea. Ili Wizara iweze kukabiliana na matatizo hayo uchunguzi ilibidi ufanyike na Wizara sasa imeyapa kipaumbele juu ya jinsi ya kukabiliana nayo.

a) Mhe. Spika, Wizara ya Afya Zanzibar kwa kushirikiana na wafadhili ambao ni *Danida, Copenhagen* na Shirika la Afya Duniani (*WHO*) imeweza kufanya utafiti mkubwa wa kina uliowahi kufanyika na Serikali ili kubaini chanzo cha ongezeko la maradhi hayo yasiyo ya kuambukiza. Utafiti ulijumuisha maradhi ya sukari, shindikizo la damu, magonjwa ya akili pamoja na vitu hatarishi vya magonjwa hayo na umehusisha shehia zote za Zanzibar.

b) Hatua tulizochukua kwanza ni kutoa marejesho ya matokeo ya utafiti huo kwa masheha wote wa Unguja na Pemba, zoezi hilo tayari limeshaanza kwa masheha wa Pemba na sasa linaendelea Unguja.

Wakati wakufanya zoezi hilo pia kunafanyika zoezi la kuwachunguza afya zao masheha. Kama vile tulivyofanya juzi kwa Waheshimiwa Wawakilishi hapa, kwa kuwapima sukari, moyo, uzito, wingi wa mafuta katika damu na kutoa majibu wakati huo huo pamoja na kutoa elimu ya afya kwa masheha hao. Pia kwa kushirikiana na masheha hao tumeweza kujipangia mikakati ya kuwafikishia wananchi taarifa hizo.

Mhe. Spika, kwa upande wa vyombo vya habari kuna vipindi katika redio mbali mbali, pamoja na televisheni kwa kuwafahamisha wananchi juu ya matokeo ya utafiti huo na namna gani ya kuweza kujikinga na magonjwa hayo.

Vile vile tumeandaa mpango wa kuweza kuwafikia na kuongea na watoto skulini, kuwapatia majibu ya utafiti. Vile vile kutoa elimu ya afya juu ya magonjwa hayo hatari, hasa ugonjwa wa sukari.

Mhe. Hassan Hamad Omar: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri wa Afya, naomba kumuuliza swali moja dogo la nyongeza. Mhe. Waziri wa Afya je, ni wagonjwa wangapi waliopelekwa nje kwa ajili ya matibabu ya maradhi ya moyo.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, idadi ya wagonjwa wangapi mwaka jana na mwaka huu waliopelekwa, hivi sasa sina nambari. Lakini ukiniuliza ni fedha kiasi gani zilizotumika nazijua. Kama nilivyowahi kutoa taarifa hapa, kwamba hivi sasa kuna msaada maalum tuliopata kwa ajili ya maradhi ya moyo ya watoto wadogo waliochini ya mwaka mmoja mpaka miaka 9, ambapo kundi la mwisho linaondoka wiki hii. Jumla yao itakuwa ni 62 wamekwenda hospitali ya India kwa msaada wa Serikali ya Oman, wengine hivi sasa wameshafanyiwa matibabu na wameanza kurudi na wengine bado wako huko. Naishukuru sana Serikali ya Oman kwa msaada

huo. Lakini ukiniuliza watu wazima wangapi, nambari hivi sasa sina. Lakini si chini ya bilioni moja tumetumia mwaka uliopita kuwapeleka wagonjwa nje na mwaka huu mpaka mwezi huu ninaosema ni kama milioni 600 tumeshatumia kuwapeleka wagonjwa hao nje.

Mhe. Ali Abdalla Ali: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa fursa ya kuuliza swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba nimuulize kama ifuatavyo. Katika ripoti ya utafiti amesema kwamba kuna mambo mbali mbali yamebainika pamoja na vitu hatarishi. Naomba nimuulize vitu hatarishi kwa maradhi ya sukari ni vipi na vitu hatarishi kwa maradhi ya presha ni vipi.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, nasikitika sikufahamu nini hatarishi.

Mhe. Ali Abdalla Ali: Mhe. Waziri katika ripoti yake alizungumza kwenye hiyo ripoti iliyotolewa ya kuchunguza maradhi mbali mbali, muna vitu hatarishi vimeelezwa Je, katika sukari vitu hatarishi ni vipi na kwenye maradhi ya presha vitu hatarishi ni vipi.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, narudia tena kama nilivyokwisharejea kwamba mimi sio daktari, lakini kwa maelezo ya madaktari, moja katika vitu hatarishi vinavyosababisha sukari ni kutokufanya mazoezi. Ni kwamba tunakula tukishakula tunalala, uzito unaongezeka na hivyo tunasababisha mwili unashindwa kusaga vyakula na unapelekea hivyo.

Mhe. Spika, nakumbuka kuna taarifa moja walinipa watu wangu kwamba kwa vipimo vya wastani, umetizamwa watoto wa Dar es Salaam wanaokula sukari na watoto wa Zanzibar wanaokula sukari. Basi watoto wa Zanzibar wanakula sukari sana tangu wakiwa wadogo kuliko wale wa Dar es Salaam. Kula sukari nyingi ni kujikaribisha kwenye matatizo hayo.

Vitu hatarishi kwa ugonjwa wa moyo vinalingana kidogo na vile vya sukari, lakini hasa ni uzito. Mhe. Spika, uzito ni tatizo sana kwa matatizo ya moyo. Vile vile tumeambiwa kwamba matatizo ya moyo mara nyengine inategemea na mwenendo wa maisha. Zamani tulikua tukiamini kua ukiugua sukari na moyo ni kwamba wewe ni tajiri.

Hao watoto waliokwenda India. Waheshimiwa Wajumbe, leo nilikua nazungumza na ofisa wangu, takriban wote ni watoto wenye maisha duni sana, familia zao ni watoto wa kimasikini sana kiasi cha kwamba wazee wao wengine hata kumuambia nenda kakate *passport* hajui, ikabidi tuwasaidie, nini *Visa* hajui, wengine kusoma na kuandika hawajui.

Kwa hivyo, kwa wastani hali ya maisha nayo ni moja katika chanzo cha maradhi haya hasa kwa watoto wadogo. Kuna wakati fulani, lakini sitaki kulitolea mfano, kuna mtu alisema vile vile jinsi ya vyakula tunavyokula. Ikiwa kila siku rundo ya sembe na dagaa watatu, nalo vile vile ni tatizo, tunakosa ile *balance diet*. Kikubwa tunachokimbilia ni kushiba. Kumbe mara nyengine kushiba kujaza tumbo nayo ni hatari na sio lazima ule nyama au samaki ya kukata vipande. Ukipata mchicha na dagaa, hata chai ya mchai chai, basi mambo yanakua. Mhe. Spika, kwa ufupi hayo ndiyo ningeweza kueleza, maana sio mtaalamu zaidi.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii, naomba nimuulize Mhe. Waziri kama ifuatavyo. Mhe. Waziri amekiri hapa kwamba tumetumia karibu bilioni moja kuwapeleka wagonjwa wetu India kwa ajili ya maradhi ya moyo na hivi karibuni tumetumia karibu milioni 600.

Mhe. Spika, tunawapeleka wagonjwa wetu huko kwa sababu hatuna wataalamu, hatuna vifaa na hatuna pengine fedha za kutosha. Hebu Mhe. Waziri atuelimishe, hivi kuendelea kutumia bilioni hizi moja na milioni hizi 600 hazitoshi kujipanga kwa serikali kuamua kuwasomesha wataalamu wetu na kutafuta vifaa, au serikali imeona njia muafaka ni kila mwaka kupeleka watu nje kwa kisingizio kua hatuna wataalamu.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, Mhe. Mjumbe ameuliza swali zuri sana na ni suala ambalo sote linatuumiza kichwa kwenye serikali. Unamuona Mhe. Omar Yussuf ananitizama pale, hakuna hata mmoja anayependelea tutumie fedha zote hizi kupeleka wagonjwa wetu nje. Moja kati ya juhudi ambazo tunazifanya ni jinsi ya namna gani tutapunguza matumizi haya na badala yake yafanyike hapa hapa nchini.

Mhe. Spika, hatua moja tuliyofanya ni kwamba tumekua tunashirikiana na wataalamu wa nje kuja hapa wakakaa kwa muda kama miezi mitatu, wakafanya matibabu yale ambayo hatuna uwezo nayo na halafu kurudi. Moja katika jambo tulilofanikiwa ni wale madaktari wa uti wa mgongo na kichwa, kila baada miezi mitatu kuna madaktari huwa wanakuja hapa wanafanya matibabu hayo.

Mhe. Spika, matibabu mengine ambayo tunafanya juhudi ni yale siku hizi kuna wale watoto ambao wana matatizo ya midomo, wana jina lao kitaalamu mimi sijui, wanakatika ile midogo inakua kama upande hivi, wanakuja nao watatusaidia. Lakini juhudi tunazofanya ni kuhakikisha kupata idara hizi za maradhi ya moyo, sukari na kibofu cha mkojo na mengine ni kua na *clinic* hapa hapa.

Mradi wetu wa *orio* nilishaeleza kwamba unategemewa kuanza mapema mwaka huu au katikati ya mwaka hapo litakapotengenezwa lile jengo ambalo lilikua zamani kiwanda cha madawa. Tutakuwa na idara pekee ya mambo ya moyo, sukari na maradhi mengine yanayohitaji utaalamu huo. Baadhi ya wataalamu wetu tumekubalia na hivi karibuni kama mnakumbuka tulifungua nyumba hapa katika Chuo cha Mbweni, nyumba zile ni za madaktari ambao watakua wanakuja kutoka Holand, watakua wanakaa pale miezi mitatu, wanafanya kazi za matibabu na halafu wanarudi, wakimaliza wanarudi tena badala ya kukaa hoteli.

Kwa hivyo, juhudi za kutatua matatizo haya zinaendelea kwa kasi kubwa. Mimi nitafurahi sana kwamba badala ya fedha hizi kuwahudumia wagonjwa kwenda nje, basi ikawa watu wanatibiwa hapa hapa. Mara nyingi wengi wanaopata maradhi hayo huwa hawana uwezo na ndio maana serikali inabidi ibebe mzigo huu. Kwa hivyo, juhudi zinafanyika Mhe. Hija Hassan na katika kipindi cha mwaka mmoja au miwili basi tutaona tofauti ya mambo haya.

Nam. 127

Ujenzi wa Madaraja ya Mkokotoni na Mto wa Pwani

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando) - Aliuliza:-

Kwa muda mrefu sasa Madaraja ya Mkokotoni na Mtoni Pwani bado hayajakamilika huku wananchi na watumiaji wa barabara kwa ujumla wanapata tabu na usumbufu mkubwa.

(a) Kwa mujibu wa Mkataba wa ujenzi wa bara bara hiyo, ni lini Madaraja hayo yatakamilika.

(b) Je, kuna sababu zipi zilizochelewesha ujenzi wa Madaraja hayo.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 127 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, madaraja haya kwa jumla ni manne, ambayo ni daraja la Mwera, Mwanakombo, Mto wa Pwani na Mkokotoni, yote kwa jumla yamo katika mkataba wa ujenzi wa barabara mbili za Amani – Dunga na Mfenesini – Bumbwini ambazo kwa ujumla zina urefu wa kilomita 25.9. Aidha, kwa mujibu wa mkataba madaraja hayo yalitakiwa kukamilika mwezi Machi, 2012. Hivi sasa madaraja hayo yameshakamilika na hatua zinazoendelea ni za ukamilishaji wa kazi ndogo ndogo, ikiwemo suala la upakaji rango na maeneo ya wapitaji kwa miguu.

(b) Mhe. Spika, sababu zilizopelekea madaraja hayo kuchelewa ni pamoja na mvua, ucheleweshaji wa kupewa eneo la kufanyia kazi kwa mkandarasi na pia ucheleweshwaji wa malipo kutoka kwa mfadhili wetu Benki ya Maendeleo ya Afrika (ADB).

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Nakushukuru Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kumuuliza Mhe Naibu Waziri swali moja la nyongeza. Katika majibu yake Mhe. Naibu Waziri anasema kwamba mwezi wa Machi madaraja haya yalikua yanatarajiwa yawe yameshakamilika na anasema yameshakamilika. Mimi nataka nimuulize, hivi lile daraja la tinga tinga ndio limeshakamilika lile. Maana anachosema limebakia sehemu ndogo, lakini tuangalie lile daraja la tingatinga ndio limekamilika.

Lakini Mhe. Spika, nilikua nataka kujua kwamba je, kwa ukamilifu huo kuna adhabu yoyote ambayo anaipata mkandarasi huyo au faini ambayo wanamtoza kwa kukawia ujenzi huo.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, tumeeleza kwamba madaraja yote manne kwa jumla yameshakamilika na kazi zinazoendelea ni kazi ndogo ndogo. Taarifa hizi zinatokana na

taarifa za kitaalamu na wao ndio wenye kujua vigezo vinavyostahiki kwa kusema kwamba daraja hili limekamilika ama kinyume chake.

Mhe. Spika, ni kweli kwamba kuna kazi zinaendelea, lakini kwa mujibu wa utaratibu wa madaraja yameshakamilika.

Mhe. Spika, sababu zilizopelekea kuchelewa kwa madaraja haya kwa muda uliokusudiwa ni pamoja na sababu za upande wa mkandarasi, lakini pia kulikua kuna sababu za sisi kama waajiri na pia kulikua kuna matatizo ambayo ni masuala ya mvua hayakuwa katika upande wowote kati ya upande wa mkataba huu. Kwa msingi huo hatukuona vyema kuingia kwenye mgogoro hadi kufika pahala pa kwenda kushtakiana na kulipana fidia, kwani tungezidi kupoteza muda pasi na ukamilishaji wa kazi hizo. Kwa maelezo hayo kwamba hakuna fidia yoyote ambayo tumemtoza mkandarasi huyo.

Mhe. Mussa Ali Hassan: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipatia nafasi ya kumuuliza Mhe. Naibu Waziri kama ifuatavyo. Mhe. Spika, barabara ya Uzi Ng'ambwa haijafanyiwa matengenezo ya kiwango cha lami kwa muda mrefu. Je, ni lini itafanyiwa matengenezo ya kiwango cha lami pamoja na kuwekewa madaraja, ili kuwaondoshea wananchi matatizo ya muda mrefu.

Mhe. Spika: Mhe Mjumbe, sina hakika sikufahamu vizuri kama daraja hili limo kwenye yale madaraja manne yaliyomo kwenye mkataba, kama ndivyo Mhe. Waziri ni vyema ukajibu, kama sivyo. Nadhani nimuombe Mhe. Mjumbe aulize swali la msingi. Kwa kweli inaonesha sivyo.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Spika, ahsante sana na mimi kuweza kunipa nafasi ya kumuuliza Mhe. Naibu Waziri. Wakati alipokuwa akijibu Mhe. Naibu Waziri alisema kuwa madaraja hayo tayari yameshakwisha kabisa.

Je, Mhe. Naibu Waziri haoni kwamba analidanganya Baraza kwa sababu hivi sasa wananchi hawayatumii madaraja hayo?

Mhe. Naibu Waziri Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, samahani maelezo yake ya mwisho sikuyapata vizuri.

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, rudia swali na ielekee vizuri hiyo *microphone*, ili Mhe. Naibu Waziri asikie vizuri.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Spika, wakati Mhe. Naibu Waziri alipojibu swali alisema kwamba madaraja tayari yameshakwisha.

Je, Mhe. Naibu Waziri atakubaliana na mimi kwamba analidanganya Baraza, kwani wananchi bado mpaka hivi sasa hawajaweza kuyatumia madaraja hayo hususan la Tinga Tinga?

Mhe. Naibu Waziri Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, tumeeleza kwamba madaraja haya ujenzi tayari umeshakamilika, na anachokizungumza Mhe. Mjumbe ni madaraja haya kuweza kutumika, hivi ni vitu viwili tofauti.

Kwa hivyo, tunachokizungumza hapa ni madaraja yamekamilika. Kwa mfano, kuna madaraja kama vile Daraja la Mwera limekamilika na linatumika, Daraja la Mkokotoni limekamilika na linatumika, Daraja la Mto wa Pwani limekamilika na linatumika.

Kwa upande wa Daraja la Tinga Tinga ni daraja ambalo tayari limekamilika, lakini utaratibu wake wa kutumika sio muda wote, kwa sababu kuna kazi ndogo ndogo ambazo zinaendelea kufanyika na hicho ndicho tulichokieleza. Sasa kwa msingi huu ni sehemu gani ambayo tunawadanganya wananchi. *(Makofi)*

Nam. 128

Ujenzi wa Barabara za Ndani (*Feeder Roads*)

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa – Aliuliza:-

Napenda kuipongeza Serikali ya Awamu ya Saba kwa kuendeleza ujenzi wa barabara za ndani (*feeder roads*) katika mitaa na majimbo mbali mbali, hali ambayo inarahisisha huduma za jamii na kupendezesha miji yetu.

Hata hivyo, Ujenzi huo wa barabara umekwama katika Jimbo la Mkwajuni.

(a) Ni lini barabara za ndani za Jimbo la Mkwajuni zitakamilika ?

(b) Kuna kipaumbele kipi kinachopelekea ujenzi wa barabara hizi kukamilika katika baadhi ya majimbo na kuchelewa ama kutojengwa kabisa kwa majimbo mengine ikiwa ni pamoja na Jimbo la Mkwajuni ?

(c) Je, serikali inatoa tamko gani kwa wananchi wa Jimbo la Mkwajuni juu ya tabu wanazozipata kutokana na kutokamilika kwa ujenzi wa njia hizo wanazozitumia kila siku ?

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 128 lenye kifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, barabara za ndani (*feeder roads*) katika Mitaa na Majimbo mbali mbali kiutaratibu zinatakiwa zihudumiwe na Halmasharui zao. Wizara yangu kwa kutambua uwezo mdogo wa Halmashauri, inashirikiana nazo kwa kuzifanyia matengenezo barabara hizo, ili kurahisisha huduma za usafiri na usafirishaji wa abiria pamoja na mizigo.

Hivi karibuni Wizara yangu kupitia Idara ya Ujenzi na Utunzaji Barabara kwa kushirikiana na baadhi ya Halmashauri. Kwa mfano, Wilaya ya Kaskazini 'A' pamoja na Viongozi wa Majimbo imeweza kuzifanyia matengenezo barabara mbali mbali za Vijijini.
Miongoni mwa barabara hizo ni:-

1. Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini "A"
- a) Barabara ya Bwekunduni Shehia ya Pita na zako ina urefu 1.5km (Mkwajuni).
- b) Barabara ya Chaani Mtakuja ina urefu 1.2km
- c) Barabara ya Chaani Miomoni ina urefu 500m
- d) Barabara ya Kinyasini Ziwani ina urefu 800m
- e) Barabara ya Nungwi ina urefu 1.2km

2. Jimbo la Koani
- a) Barabara ya Kidimni – Ubago
- b) Barabara ya Koani – Kibondemaji

3. Jimbo la Magogoni
Barabara ya Kinuni

Aidha wizara yangu inajiandaa kufanya matengenezo ya barabara ya Mkunazini kwa kushirikiana na Viongozi wa Jimbo hilo. Pia kwa kushirikiana na Viongozi wa Jimbo la Uzini tunategemea kuzishughulikia barabara ndani ya jimbo hilo.

Kwa hivyo, namthibitishia Mhe. Mjumbe kwamba Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano pamoja na Idara yetu ya *UUB*, tuko tayari muda wote kushirikiana naye, jambo la msingi ni kutoa ushirikiano unaostahiki.

(b) Mhe. Spika, hakuna kipaumbele chochote kilichowekwa kwenye baadhi ya majimbo zaidi ya mashirikiano kati ya Idara ya *UUB*, viongozi husika wa majimbo pamoja na Halmashauri zao.

(c) Mhe. Spika, tunatoa wito kwa wananchi wa Jimbo la Mkwajuni kuwahimiza viongozi wao, kwa kusaidiana pamoja na kushirikiana nao, ili wapate imani na nguvu ya kushirikiana na viongozi na watendaji wa Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano, kwa ajili ya kuweza kuzifanyia matengenezo barabara zao za ndani kwa madhumuni ya kuondoa na kupunguza usumbufu wanaoupata.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mhe. Spika, nakushukuru pamoja na majibu marefu ya Mhe. Naibu Waziri ambayo sikuridhika nayo. Kwa kweli mwaka jana katika Mkutano wa mwezi wa *March* kama huu, niliuliza swali kama hili kutaka kujua ujenzi wa barabara zile za ndani na Mhe. Naibu Waziri alikubaliana na mimi kwamba tufuatane twende tukakague zile barabara, tulizifanyia ukaguzi na tukawa tunasubiri taarifa ya upembuzi yakinifu, lakini mpaka hii leo sijaipata.

(a) Kwa hivyo, sijui taarifa ile ya upembuzi yakinifu lini itakuwa tayari?

(b) Mashirikiano yepi anayoyataka kutoka kwa viongozi wa majimbo na Idara yake ya UUB, ili barabara hizo ziweze kujengwa?

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, ni kweli kwamba maelezo aliyotoa Mhe. Mjumbe mimi mwenyewe binafsi nilishirikiana naye kwenda kuzikagua hizo barabara za ndani. Vile vile ni kweli kwamba wenzetu wa *UUB* wamefanya tathmini.

Lakini tulichokizungumza hapa Mhe. Spika ni kuona kwamba viongozi husika kutoa ushirikiano. Kwa hivyo, tunaposema ushirikiano ni suala la uwezeshaji kwa taasisi yetu, yaani taasisi yetu ipo tayari kutoa *man power* ya wataalamu wao, vifaa tulivyonavyo pamoja na muda, kwa sababu kuna huduma muhimu kama vile mafuta ambayo yatakayowezesha kwenda kupata vitendea kazi ikiwemo kifusi na huduma nyengine muhimu, basi ni lazima viongozi husika watoe ushirikiano huo.

Kwa maana hiyo, katika Jimbo hilo la Mkwajuni kuna barabara ambayo Halmashauri imekuja kushirikiana na Idara yetu ya *UUB* na tumeweza kufanya huduma hiyo ya kutia kifusi kwa urefu wa 1.5km.

Halikadhalika katika Jimbo la Tumbatu imetokea kama hivyo, pia Jimbo la Makunduchi na baadhi ya majimbo mengine.

Mhe. Spika, napenda kumfahamisha Mhe. Mjumbe pamoja na Baraza lako tukufu kwamba, ushirikiano tunaoutaka ni pamoja na kusaidia fedha kwa ajili ya huduma za kuimarisha miundombinu hiyo. Mhe. Spika, nadhani maswali ya Mhe. Mjumbe yote (a) na (b) yamejibika kwa pamoja.

Mhe. Nassor Salim Ali: Mhe. Spika, ahsante sana na mimi kunipa nafasi moja ya kuuliza swali la nyongeza. Kwanza nachukua fursa hii kumpongeza Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri na kuzitaja barabara ambazo serikali imeweza kuzifanyia matangenezo.

Katika Jimbo la Rahaleo kuna barabara ya *feeder road* ambayo ipo pale Miti Ulaya kuelekea kwenye Hospitali ya Mwembeladu. Je, Mhe. Waziri kutokana na umuhimu wa barabara ile, haoni kwamba ipo haja katika Bajeti ya mwaka 2012/2013 kuweka kifungu cha fedha, kwa ajili ya kujengwa barabara ile.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, kiutaratibu napenda kurejea tena kusema kwamba barabara hizi za ndani zinapaswa kutengenezwa na Halmashauri zetu. Lakini tunashirikiana na Halmashauri zetu kwa kuwa uwezo wao ni mdogo. Pamoja na hayo, napenda kumkumbusha Mhe. Mjumbe pamoja na Baraza hili tukufu, yeye mwenyewe binafsi kwa kushirikiana na Idara yetu ya UUB tumeweza kumtengenezea barabara moja, na tumemuwekea lami ubavuni kwa sheli na alikuwa na kilio cha muda mrefu.

Kutokana na hali hiyo, imani yangu ni kwamba wenzetu wa Mfuko wa Barabara watakuwa wamekisikia kilio hicho, na watakiingiza katika hisia na umuhimu unaostahiki kwa mujibu wa uwezo na fedha watakazoweza kuzitenga. *(Makofi)*

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza kama ifuatavyo.

Kwa kweli matengenezo ya barabara ni kitu ghali sana, na imekuwa ni mtindo kwa Wizara ya Miundombinu tunapokumbusha kuhusu barabara zetu Mhe. Spika huwa tunaambiwa tuchangie, wakati wizara hii inatambua wazi kwamba katika mshahara wa Mwakilishi hakuna fungu la ujenzi wa barabara.

Je, Mhe. Waziri haoni kama hivi sasa kuna haja ya kutafuta jawabu nyengine isiyokuwa hii?

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, nakubaliana na maelezo ya Mhe. Mjumbe kwamba katika mshahara wa Mhe. Mwakilishi hakuna fedha za utengenezaji wa barabara.

Vile vile napenda kumkumbusha Mhe. Mwakilishi pamoja Baraza lako hili tukufu kwamba, katika Mfuko wa Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano hakuna fedha za kutengeneza *feeder roads*.

Kwa maana hiyo, jambo la msingi ni kuendelea kushirikiana nao wenzetu wa *Road Funds*, kuwashawishi, ili kuona kwamba kuna umuhimu wa kuongeza fedha kwa kusaidiana, na kutambua kuwa maeneo haya

yanayostahiki kufanyiwa matengenezo na uimarishaji wa barabara hasa hizi za ndani, yamekuwa ni makubwa na yanahitaji ufumbuzi utakaoweza kuondoa changamoto hii, kwa ajili ya kuweza kurahisisha mawasiliano na miundombinu kwa wananchi wetu.

HOJA ZA KAMATI

Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi

Mhe. Spika: Mhe. Mwenyekiti, bado sijakwita nakuomba ukae kitako. *(Makofi)*

TAARIFA YA SPIKA

Waheshimiwa Wajumbe, nadhani mtakumbuka juhudi za ofisi tunazojaribu kuchukua, ili shughuli zetu za Baraza tuzijadili kwa mapana na Waheshimiwa Wajumbe tumekuwa tunalalamika sana kwamba muda unaowekwa kwa ajili ya Ripoti za Kamati ni mdogo.

Kutokana na hali hiyo, mara hii tukasema basi angalau ripoti mbili kwa siku moja badala ya tatu au nne kama ilivyokuwa huko nyuma. Kwa kweli tumejaribu hivyo, kikao chetu mara hii kimekuwa kirefu kidogo kwa sababu ya shughuli nyingi.

Vile vile kwa kuzingatia suala la umuhimu wa Ripoti za Kamati za Baraza, kwa sababu pale ndipo hasa kamati kwa maana ya Waheshimiwa Wajumbe tunasimamia serikali, katika kuona utekelezaji wa yale ambayo yalikuwa yameahidiwa katika chombo hiki, hasa katika kipindi cha bajeti na wakati mwengine pale tunapouliza maswali na kutaka kwamba serikali ishughulikie jambo fulani.

Wiki iliyopita siku ya Ijumaa, Hati ya Mwenyekiti iliwasilishwa kwamba itatolewa hapo baadaye, wakati ulipofika Mwenyekiti hayupo. Kwa kweli hii si nidhamu, ni utaratibu mbaya ambao utatuvurugia utaratibu wa shughuli zetu. *(Makofi)*

Jambo hili mimi kama Spika silisamehe, kwa sababu tunawaambia mawaziri hapa wakati anapokuwa hayupo, kwamba waziri huyu ajieleze kwa nini hayupo, hivyo Mjumbe au Mwenyekiti inabidi ajieleze kwa nini alikuwa hayupo bila ya taarifa. Waheshimiwa Wajumbe, tunapaswa kuwa *serious*, yaani tuwe *committed* na shughuli zetu, kwa sababu tunatumia fedha za serikali kwa ajili ya shughuli za wananchi. *(Makofi)*

Sasa inapofika pahala kwa Mjumbe, Mwenyekiti anaitwa hayupo, na wala hakumuachia kazi hiyo mtu huyo mwengine yeyote ndani ya Kamati ile, hiyo si nidhamu. Kwa hivyo, barua inafuata ili muhusika wa Kamati hii atoe maelezo, aje aombe radhi Baraza hili, kwa sababu amevunja utaratibu wa shughuli za Baraza. *(Makofi)*

Kwa maana hiyo, kwa sasa barua hiyo itamfuata na mimi simjui Mwenyekiti huyo ni nani? Ilikuwaje? Hatukupata sababu na huo si utaratibu mzuri na wala sio nidhamu. *(Makofi)*

Kwa hivyo, nakemea jambo hili, ili tuone kwamba tujipange vizuri wakati tunapopanga shughuli zetu, kwa sababu tunazipangia muda, ili kuona shughuli zote zimalize. Sasa kama Mwenyekiti hayupo na wala hakuna taarifa, hiyo nidhamu na utaratibu mzuri wa chombo hiki tunauweka wapi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wajumbe, nimetoa taarifa hiyo makusudi ili tuone umuhimu wa shughuli zetu za Baraza, na kimsingi nataka Wajumbe wawepo, ili tuone tunaendesha shughuli zetu kwa niaba ya wananchi wale wanaokaa pale, na wengine wanaosikiliza moja kwa moja kupitia vyombo vya habari. *(Makofi)*

Kwa bahati nzuri hivi sasa Mhe. Waziri wa Habari mambo haya anarusha moja kwa moja. Kwa maana hiyo, imeeleweka na wananchi kikao kimekishwa mapema, kwa sababu Mwenyekiti hakuwepo. Kwa hiyo, si utaratibu mzuri, si nidhamu na hivyo anayehusika inabidi aombe radhi Baraza na barua inakuja. *(Makofi)*

Sasa tuendelee, naomba nimkaribishe Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi. Waheshimiwa Wajumbe, kumbe ndiye huyu. *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk (Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi): Mhe. Spika, pamoja na yote hayo nimesikia na umesema kuwa Mwenyekiti mwenyewe humjui, ndiye mimi. Kwa kweli Mhe. Spika binadamu ni binadamu.

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, nadhani hivi sasa ungeendelea na kazi na huo utaratibu utafanya baadae, kuna barua utaijibu na tutaisoma hapa, ili tuone kwamba unaomba radhi Baraza. Kwa hivyo, tutachukua muda mwengine ambapo kwa kweli ratiba imeanza kuvurugika, kwani kuna barua uijibu kwanza na hivi sasa endelea na kazi.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk (Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi): Mhe. Spika, ahsante sana nitaufuata utaratibu wako na Inshaallah Mwenyezi Mungu atanijaalia.

Mhe. Spika, naomba kuchukua fursa hii kwa kutoa muhtasari wa Ripoti ya Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi mwaka 2011/2012.

Utangulizi

Mhe. Spika, kwa niaba ya Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi, napenda kukushukuru wewe binafsi pamoja na Ofisi ya Baraza la Wawakilishi, kwa kuipa Kamati yetu ushirikiano mkubwa uliotuwezesha kutekeleza majukumu yetu kwa ufanisi mkubwa. Lakini pia tunashukuru kwa kutupatia nafasi ya kueleza japo kwa muhtasari, Ripoti ya Kamati inayotokana na kazi ambazo zimekuwa zikitekelezwa na Kamati kwa takriban mwaka mzima.

Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi ya Baraza la Wawakilishi imeundwa kwa mujibu wa kifungu cha Kanuni cha 104 (c) cha Kanuni za Baraza la Wawakilishi (2011), na majukumu yake yametajwa katika kifungu cha (109) kama ifuatavyo:-

a) Kufuatilia utekelezaji wa maagizo ya Kamati yaliyotolewa kwenye ripoti ya Kamati ya mwaka uliotangulia.

b) Kufuatilia utekelezaji wa Sera na Mipango ya wizara husika kwa kadri Spika atakavyoelekeza kwa mujibu wa malengo yaliyowasilishwa Barazani wakati wa usomaji Bajeti na Hotuba nyengine za Waziri alizotoa Barazani.

c) Kufuatilia utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ya Kitaifa na Miradi ya Wananchi ya Wizara husika.

d) Kuchunguza na kufuatilia mapato na matumizi ya kila mwaka ya serikali, na kama matumizi yaliyofanywa yalizingatia thamani halisi ya fedha.

e) Kuchambua mapendekezo ya serikali kuhusu makadirio ya wizara husika ya mapato na matumizi ya kila mwaka.

f) Kushughulikia Miswada ya Sheria itakayokabidhiwa kwako na Spika.

g) Kuchambua ahadi zote za wizara zilizo chini ya Kamati kama zitakavyokuwa zikitolewa katika Baraza na kufuatilia utekelezaji wa ahadi hizo.

h) Kufikiria jambo jengine lolote litakalopelekwa kwake na Spika.

Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi kwa mwaka wa fedha 2011/2012 ilianza shughuli zake za kufuatilia utekelezaji wa kazi za maendeleo ya wizara zifuatazo:-

- Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati
- Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano

Kamati ilifanya kazi zake kwa muda wa wiki sita

i) Unguja wiki mbili kuanzia tarehe 26 Septemba hadi tarehe 7 Oktoba 2011

ii) Pemba wiki mbili kuanzia tarehe 12 hadi tarehe 23 Disemba 2011 na

iii) Unguja kuanzia tarehe 20 Februari hadi tarehe 2 Machi 2012.

Mhe. Spika, ingawa tayari Wajumbe wa Baraza lako tukufu tulishataarifiwa kuhusu kifo cha mwenzetu Mhe. Salum Amour Mtondoo, sitoweza kuisoma ripoti hii bila ya kumkumbuka marehemu Mtondoo ambaye kama Wajumbe wa Baraza wanavyokumbuka, alikuwa mjumbe wa Kamati hii hadi mauti yalipomfika.

Kwa kadri tunavyomkumbuka wakati wa utekelezaji wa kazi za Kamati, marehemu alikuwa mpole, mcheshi, hodari na aliyekuwa tayari kufanya kazi wakati wowote. Hata pale afya yake ilipokuwa si nzuri siku chache kabla ya kufariki kwake, marehemu alisisitiza kushirikiana nasi katika kazi za Kamati. Wajumbe wa Kamati ya Mawasiliano, na naamini Wajumbe wote wa Baraza, tutamkumbuka daima mwenzetu, rafiki yetu marehemu Mtondoo.

Napenda kuchukua nafasi hii adhimu kuwashukuru Wajumbe wa Kamati hii kwa mashirikiano yao, ambayo yamewezesha kufanya kazi zetu kwa ufanisi mkubwa. Wajumbe wenyewe ni hawa wafuatao:-

1. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk - Mwenyekiti
2. Mhe. Rashid Seif Suleiman - M/Mwenyekiti
3. Mhe. Shawana Bukheti Hassan - Mjumbe
4. Mhe. Salma Mussa Bilal - Mjumbe
5. Marehemu Mhe. Salum Amour Mtondoo – Ambaye kutokana na mchango wake mkubwa katika utekelezaji wa kazi za Kamati, ripoti hii imeweza kuandikwa.
6. Mhe. Subeit Khamis Faki - Mjumbe
7. Mhe. Hassan Hamad Omar - Mjumbe
8. Ndg. Mussa Kombo Bakar - Katibu
9. Ndg. Aziza Wazir Kheir - Katibu

Mhe. Spika, Kamati ilifanya kazi zake kwa utaratibu wa kupokea taarifa za utekelezaji wa malengo ya wizara pamoja na taasisi zake, na baadae kutembelea na kukagua utekelezaji wa shughuli zinazofanywa na taasisi hizo.

WIZARA YA ARDHI, MAKAAZI, MAJI NA NISHATI

Mhe. Spika, kamati yetu ilitembelea taasisi mbali mbali za wizara hii, na kukagua miradi kadhaa inayotekelezwa na taasisi hizo. Baada ya kutembelea na kuona utekelezaji wa shughuli hizo, kamati ilitoa maelekezo na ushauri kwa wizara na taasisi zake kwa lengo la kuongeza ufanisi katika utekelezaji.

Mhe. Spika, muhtasari huu unabainisha baadhi ya mambo ambayo kamati inaona kuwa ni muhimu sana, kwa ajili ya kuisaidia serikali katika utendaji wake na wananchi kwa ujumla. Mambo yenyewe ni kama yanavyofafanuliwa hapa chini.

Mhe. Spika, ardhi ni miongoni mwa rasilimali muhimu sana, na isipotumika inavyotakikana, matatizo mbali mbali hujitokeza. Kutokana na udogo wa nchi yetu na matumizi ya ardhi kuwa ni makubwa, kutokana na matatizo mbali mbali yaliyopo hivi sasa katika suala zima la ardhi.

Kamati inazielekeza idara zinazohusika na masuala ya ardhi, ambazo ni Idara ya Ardhi na Usajili, Idara ya Upimaji na Ramani na Idara ya Mipango Miji na Vijiji na nyenginezo, kuyasimamia maeneo yote ambayo tayari yameshapimwa na kuhakikisha kuwa matumizi ya maeneo hayo yanalingana na mipango iliyopangwa na taasisi hizo. Pia kamati inasisitiza kuwa suala la "*Master Plan*" lizingatiwe kwa kutoa kipaumbele kwa maeneo yote ya mijini na Vijijini.

Mhe. Spika, kamati yetu ilikagua katika eneo la *Stendi* ya Chake Chake na kusisitiza kuwa pamoja na mipango iliyowekwa na wizara kupitia Idara ya Mipango Miji na Vijiji, ya kutaka kurekebisha mipango miji ya Mji wa Chake Chake, kamati inasisitiza kuwa njia ya kutokea katika *stendi* hiyo ni muhimu kuwepo, ili kuepuka msongamano mkubwa uliopo sasa unaosababishwa kwa kiasi kikubwa na gari za abiria kuingia na kutoka s*tendi* kwa kutumia njia hiyo hiyo moja.

Aidha kamati inaiagiza Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati na Wizara ya Miundombinu na Mawasilino, washirikiane katika kulimaliza tatizo hilo.

Mhe. Spika, kamati yetu katika kazi zake imegundua kuwa, kuna baadhi ya viongozi ambao hawahusiki na masuala ya ardhi, lakini wamekuwa wakiyatumia. Hivyo, kamati inawataka viongozi wa ngazi zote kuacha tabia ya kutoa maamuzi yasiyowahusu hasa katika masuala ya ardhi, jambo ambalo huwagombanisha maafisa wa taasisi husika na wananchi.

Vile vile kamati inaziagiza Idara zote za ardhi kuhakikisha kuwa ardhi inatumika kwa mujibu wa inavyoombwa na wananchi, kwani hivi sasa kumekuwa na tabia ya baadhi ya wananchi kuzitumia eka zilizotolewa na serikali kwa ajili ya kilimo na kuzigeuza kuwa ni maeneo ya makaazi. Hivyo kamati inaelekeza idara husika, izisimamie na kuzidhibiti eka hizo hasa zile ambazo hazijavamiwa na kujengwa makaazi. *(Makofi)*

Mhe. Spika, masuala ya ardhi yamekuwa na malalamiko hapa nchini, na kusababisha mrundikano mkubwa wa kesi za ardhi katika Mahakama ya Ardhi. Hivyo kamati inaishauri wizara kuendeleza ahadi zake za kujenga Mahakama za Ardhi, ambazo zitasaidia kuondoa msongamano wa kesi zilizopo hivi sasa ambazo zimekuwa ni mzigo mzito kwa taasisi hiyo.

Pia kamati inasisitiza kuwa suala la kuongezewa posho wazee wa Mahakama "*Accessors*" ni muhimu sana, kutokana na kazi kubwa wanazozifanya wazee hao, ambapo nyongeza hiyo itakuwa ni hamasa kwao kufanya kazi kwa bidii zaidi.

Mhe. Spika, jambo jengine ambalo ni muhimu kwa maslahi ya wananchi wa Zanzibar, ni suala zima la upatikanaji wa huduma ya maji Mijini na Vijijini. Kamati ilitembelea miradi mbali mbali inayoendelezwa na Mamlaka ya Maji katika kutatua tatizo hilo hapa nchini. Pamoja na kukamilika kwa baadhi ya miradi na kuanza kufanya kazi kwa kutoa huduma hiyo kwa baadhi ya maeneo.

Kamati yetu inaendelea kusisitiza kuwa, Mamlaka ina jukumu kubwa la kuwa na mpango maalum wa kulimaliza tatizo hilo hapa nchini, hasa katika Mkoa wa Mjini Magharibi, ambapo fedha nyingi zimeshatumika kutatua tatizo hilo lakini bado hali haijawa ya kuridhisha.

Mhe. Spika, kamati yetu inaisisitiza serikali kulitilia mkazo suala la uongezaji wa kodi kwa nyumba zote zinazomilikiwa na serikali, ili kuisaidia Idara ya Nyumba na Maendeleo ya Makaazi kujiendesha na kuongeza pato la taifa, ambalo litasaidia katika mendeleo ya wananchi. Aidha kamati inaunga mkono wazo la Idara la kuongeza kodi kwa nyumba zote zinazomilikiwa na serikali, jambo ambalo litaiwezesha idara kutekeleza majukumu yake ipasavyo, likiwemo jukumu la kuzifanyia matengenezo nyumba za maendeleo na nyumba nyengine za serikali kwa ufanisi mkubwa.

Mhe. Spika, kamati yetu imeguswa sana na taarifa ilizozipata kuwa, fedha zilizotengwa kwa ajili ya ujenzi wa Nyumba za Mpapa zinataka kuchukuliwa na kupelekwa Pemba kwa ajili ya ujenzi wa Nyumba za Kengeja.

Hivyo, kamati inaisisitiza wizara kuliangalia upya suala hilo, na kuziacha fedha hizo zitumike kwa ajili ya kumalizia Nyumba za Mpapa, na badala yake zitafutwe fedha nyengine kwa ajili ya matengenezo ya Nyumba zilizopo Kengeja, kwani kuna umuhimu wa nyumba zote hizo kutengenezwa.

Mhe. Spika, kamati yetu imesikitishwa sana na kitendo kinachofanyika hivi sasa kati ya Baraza la Manispaa na Mamlaka ya Uhifadhi na Uendelezaji Mji Mkongwe, ambapo suala zima la *Parking* na suala la fedha za Bustani ya Forodhani, limekuwa na utata miongoni mwa taasisi hizi. Kutokana na taarifa tulizopatiwa kuwa Rais mstaafu wa awamu ya sita, alitoa agizo kuwa fedha zitakazokuwa zinaingia katika bustani ya Forodhani zitengwe katika akaunti yake maalum na zitumike kwa ajili ya kuiendeleza bustani hiyo. Hata hivyo Kamati yetu ilipatiwa taarifa kuwa fedha hizo hivi sasa hazitumiki kama ilivyoelekezwa na badala yake Mkurugenzi wa Baraza la Manispaa amezihamisha fedha hizo katika akaunti husika bila ya kutoa taarifa kwa Mkurugenzi wa Mamlaka ya Mji Mkongwe. Hivyo Kamati inaisisitiza Wizara kulifuatilia suala hilo na hatimae fedha hizo zitumike kwa madhumuni yaliyokusudiwa, ili kuirudisha haiba inayopotea katika bustani ya Forodhani.

Mhe. Spika, Kwa upande wa Shirika la umeme Zanzibar (*ZECO*) Kamati inaelekeza kuwa, ni vyema Shirika hilo likawasogezea wananchi huduma ya umeme hasa wale wa vijijini ambao hali zao kiuchumi ni duni jambo ambalo litaliongezea Shirika wateja. Pia Kamati inazidi kulisistiza Shirika la umeme kuwajali wateja wake wote wadogo na wakubwa kwa kuwapatia huduma zilizo bora na kuondoa malalamiko yanayojitokeza hivi sasa

kutoka kwa baadhi ya wananchi. Aidha Kamati inasisitiza umuhimu wa Shirika kushirikiana na taasisi nyengine zinazotoa huduma kwa wananchi ikiwemo kampuni ya simu za mikononi ya ZANTEL.

WIZARA YA MIUNDOMBINU NA MAWASILIANO

Mhe. Spika, Katika Wizara hii Kamati ilipata fursa ya kuzitembelea baadhi ya taasisi na kukagua miradi inayosimamiwa na taasisi hizo. Baadhi ya mambo muhimu ambayo Kamati iliyaona na kuyatilia msisitizo ni kama yanavyofafanuliwa hapa chini.

Mhe. Spika, Kamati yetu ilitembelea katika Shirika la meli na kubaini kuwa, kuna mwekezaji amejitokeza kutoka kampuni ya *FAMAL INTERNATIONAL CO. LTD* ya nchini Sudan ambapo muwekezaji huyo yuko tayari kuisaidia nchi yetu kuliondoa tatizo la usafiri liliopo hivi sasa kati ya visiwa vyetu vya Unguja na Pemba. Hivyo Kamati inazidi kuisisitiza Serikali kuharakisha na kukamilisha taratibu zote za uwekezaji ili mwekezaji huyo aweze kupata nafasi ya kutoa huduma za usafiri kwa wananchi, ambao umekuwa ni usumbufu na changamoto kubwa kwa Serikali.

Mhe. Spika, Kamati yetu ilipotembelea Shirika la Bandari ilipatiwa taarifa na kushuhudia kuwa bado Shirika linakabiliwa na changamoto ya mrundikano wa makontena katika eneo la Bandari hapo Malindi, kutokana na eneo la bandari hiyo kuwa dogo na mahitaji kuwa ni makubwa. Kamati yetu inasisitiza umuhimu wa kupewa eneo liliopo mbele ya Hoteli ya Bwawani kwa ajili ya kuyaweka makontena hayo, ili kupunguza mrundikano huo ambao unazorotesha shughuli za kiutendaji katika bandari yetu na kutukosesha mapato mengi. Aidha Kamati yetu inalielekeza Shirika kuzidi kuziimarisha bandari zake ziliopo Pemba kwa kuharakisha upelekaji wa vifaa vya kupakulia mizigo katika bandari hizo, kwa kufanya utanuzi wa bandari ya Wete na matengenezo ya Bandari ya Mkoani.

Mhe. Spika, katika ufuatiliaji wake katika Mamlaka ya Usafiri Baharini, Kamati ilielezwa changamoto nyingi zinazoikabili Mamlaka hiyo zikiwemo za ukosefu wa wataalamu, ambapo hapo awali Mamlaka ilikuwa na wataalamu watatu ambao wote kwa sasa wamesimamishwa kazi kutokana na matatizo yaliyotokea katika ajali ya Mv Spice Islander na ufinyu wa bajeti, ambapo Mamlaka inashindwa kufanya kazi zake. Aidha Kamati inashauri Serikali kuchukua hatua za dharura ili kupata wataalamu watakaoweza kutekeleza majukumu ya taasisi hiyo. Pia Kamati inaielekeza Mamlaka kuongeza juhudi katika kufanya ukaguzi wa vyombo mbali mbali vya baharini, ili kujiridhisha kuwa vyombo hivyo ni vizima na vinaweza kufanya safari zake bila ya matatizo.

Mhe. Spika**,** Kamati pia ilitembelea ujenzi wa uwanja wa ndege mpya na kuangalia hatua iliyofikiwa hivi sasa mbayo ni ya kuridhisha. Hata hivyo uwanja wa ndege wa Pemba unahitaji matengenezo makubwa ili uweze kutumika kwa wakati wote kwa kuzingatia kuwa kwa sasa uwanja huo hautumiki wakati wa usiku kutokana na kukosa taa. Mhe. Spika**,** pamoja na ukarabati mkubwa na uboreshaji mkubwa uliofanyika katika uwanja wa ndege hapa Unguja, Kamati inaishauri Mamlaka inapotaka kufanya marekebisho yoyote yale iwe na utaratibu wa kuwashirikisha wadau wote wa Mamlaka, ili waweze kutoa mawazo yao ambayo yanaweza kusaidia kwa asilimia kubwa.

Mhe. Spika, Kamati katika Idara ya Ujenzi na Utunzaji wa Barabara imeielekeza Wizara kuwa katika miradi ya Ujenzi wa barabara ambayo serikali inapata mikopo, Kamati inashauri kuwa gharama za fidia ziingizwe moja kwa moja au kwa njia nyengine yoyote, katika thamani ya jumla ya mkopo ili iwe sehemu ya mkopo huo, kwa ajili ya kuufanya utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa barabara usichelewe kutokana na kukosekana malipo ya fidia kwa wananchi watakaovunjiwa kupisha ujenzi wa barabara hizo, na kuwafanya wajenzi wa njia hizo kuifanya hali hiyo kuwa ni kisingizio kikubwa cha kuchelewa kumaliza kazi zao kwa mujibu wa mkataba walioufunga.

Mhe. Spika, Kamati yetu inaamini kuwa Karakana ya Serikali endapo itatumika vyema, inaweza kusaidia katika kukusanya mapato lakini pia kuokoa fedha nyingi za Serikali, Kamati inaendelea kuelekeza haja ya kufanya tathmini ya vifaa vyote vilivyoharibika katika Karakana ya Serikali pamoja na wataalamu wa kutumia vifaa hivyo wanaohitajika na kuiwasilisha Wizarani kwa ajili ya kuviombea fedha, ili kuirejesha Karakana katika hadhi yake na kuongeza uwezo wa kutoa huduma na kuchangia katika pato la Taifa. Aidha Kamati inaendelea kusisitiza Wizara nayo kwa upande wake, kutoa kipaumbele katika suala la kuiimarisha Karakana hiyo kwa kuipatia fedha kwa ajili ya mahitaji ya vifaa, wataalamu na mambo mengine ya msingi yanayohitajika. Mhe. Spika, Kamati pia inazishauri taasisi zinazohusika kutoa ushirikiano wa kutosha kwa mujibu wa sheria na taratibu ziliopo, wakati Kampuni ya *ZANTEL* inapoomba vibali vya ujenzi wa minara ya simu katika maeneo mbali mbali.

Mhe. Spika, suala jengine ambalo Kamati hii ingependa kulitilia mkazo, ni suala la wafanyabiashara wetu wanaosafirisha mizigo kutoka Tanzania Bara kuja Zanzibar wanapotozwa gharama kwa huduma ambazo hawakuzitumia. Kumekuwa na malalamiko makubwa kwa wafanyabiashara wetu kutozwa gharama za kutumia vifaa maalum vya kunyanyulia mizigo na kuingiza ndani ya meli wakati wafanyabiashara hao huwalipa wachukuzi kubeba bidhaa zao na kuziingiza ndani ya meli. Kamati inaelekeza kuwa suala hilo lifanyiwe kazi na kupatiwa ufumbuzi haraka.

HITIMISHO

Katika kutekeleza wajibu wake kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar, Kanuni za Baraza la Wawakilishi na Sheria nyenginezo, Kamati imetoa maelekezo na ushauri wake ambao tunaamini kuwa utasaidia katika kuleta ufanisi kwenye utekelezaji wa majukumu ya Serikali kupitia Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati na Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano. Maelekezo na maoni hayo yalitolewa na Kamati kwa dhamira ya kuwawakilisha vyema wananchi wa Zanzibar na kuona kuwa maslahi ya wananchi hao, kwa mujibu wa sheria, yanapewa kipaumbele. Kamati yetu inatumai kuwa maelekezo na maoni yaliyotolewa na Kamati kwa Wizara hizo yatazingatiwa kwa lengo la kutoa huduma zilizotukuka kwa wananchi wa Zanzibar.

Mwisho, Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi ya Baraza la Wawakilishi inaushukuru uongozi wa Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati chini ya Waziri wa wizara hiyo, Katibu Mkuu wake pamoja na watendaji wote wa wizara hiyo, kwa ushirikiano mkubwa walioupatia Kamati yetu katika kipindi chote cha kazi za Kamati kwa Unguja na Pemba.

Aidha Kamati pia inaushukuru uongozi wa Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano chini ya uongozi wa Waziri wa wizara hiyo, Naibu Waziri na Katibu Mkuu wa wizara hiyo na watendaji wote wa wizara kwa ushirikiano mkubwa kwa Kamati yetu, ulioiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi mkubwa.Kamati inatoa shukurani za pekee kwa Spika wa Baraza la Wawakilishi, Mhe. Pandu Ameir Kificho, Katibu wa Baraza la Wawakilishi na watendaji wa Ofisi ya Baraza la Wawakilishi kwa kuiwezesha Kamati hii kutekeleza majukumu yake vizuri, lakini zaidi kwa ushauri walioupatia Kamati yetu katika kipindi cha utekelezaji wa majukumu yake.

Mwisho kabisa, Kamati inawashukuru Makatibu wa Kamati hii kwa kutekeleza majukumu yao ya kuisaidia Kamati na Wajumbe wa Kamati ili waweze kufanya kazi zao kwa ufanisi mkubwa. Kamati isingependa kusahau kutoa shukurani zake kwa waratibu wa ziara za Kamati kutoka Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati na wale wa Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kwa kuweza kuratibu ziara za Kamati yetu katika wizara zao kwa mafanikio makubwa.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

Lakini Mhe. Spika, pamoja na hayo yote, na mimi naomba kama dakika tano, ili wananchi wangu wa jimbo la Kitope kwa mujibu wa kanuni ili niweze na mimi kuchangia kidogo naomba.

Mhe. Spika, mchango wangu mimi ni mdogo sana sio mkubwa, na hasa pale Mheshimiwa kuhusu vyombo vya wenzetu wanapokwenda Dar es Salaam mara nyingi sana vinakuwa vyombo vile vinatakiwa vitumiwe zile krini, lakini kwa kuwa hakuna vile vyombo wanakuwa wanatumia wale wachukuzi, sasa wanalipishwa mara mbili, wanalipishwa wakati wale wachukuzi wanawalipa, wanalipwa wakati zile krini hazifanyi kazi wanalipishwa. Sasa ningeomba kwa makusudi wizara husika au serikali yetu hili suala walitilie mkazo, ili kuwasaidia wenye vyombo hivyo kwa kweli wanapata hasara kubwa sana.

Lakini isitoshe Mhe. Spika, utakuta hata zile siku za Mapumziko ambazo zinakuwa hazina kazi ya aina yoyote, wale wanatozwa fedha ni kitu ambacho kinasikitisha sana, kwa hivyo kamati yangu imeona hili suala nilitilie mkazo ili kuweza kulisaidia sana.

Lakini Mhe. Spika, tulizungumza katika kifungu wakati alipokuwa anatoa hoja hapa kuwa, viongozi ambao wanaingia katika idara ambayo si yao na kuitolea amri, hili suala halileti sura nzuri, suala hili ambalo linakwenda kwa upande wa wanyonge wanakuwa hawapati haki baada ya kuwa kiongozi Mkuu ameshafika pale kutoa amri. Hili suala sio zuri hata kidogo na ushahidi upo ndani ya *document* kuna kiongozi ambaye tayari, kuna wananchi ambao eneo la Donge maskini ya Mungu hao ni yatima hao walikuwa wameomba kwa utaratibu wa kutaka kurithishwa ile heka kwa mujibu wa sheria. Walikwenda kwa Sheha akaidhinisha akasema hakuna tatizo na sina pingamizi yoyote wapewe, wamekwenda kwa Mkuu wa Wilaya naye kathibitisha vile vile kuwa na mimi sina pingamizi wamepewa.

Wamekwenda kwa Mkuu wa Mkoa hali kadhalika na kule hakuna pingamizi wamepewa, lakini cha kushangaza Mkuu wa Mkoa amekubali kuwa hakuna tatizo baada ya muda barua ile ile ya Mkuu wa Mkoa imekwenda kusimamisha, na apewe mtu mwengine ni suala ambalo linasikitisha sana.

Kwa hivyo, suala hili mheshimiwa muhusika tunakuomba uliangalie, masuala kama haya yana matatizo yake na sisi kamati tumeliona hilo kuwa viongozi tuwaaachie idara husika. Hata kama wewe una swahiba wake, basi wewe tafuta njia nyengine, lakini lisikilize wewe kiongozi kwanza hilo suala je linamuuwa nani.

Leo suala kama hili linauwa wanyonge tena yatima. Ni suala ambalo kwa kweli linasikitisha kabisa. Huyo jamaa alivyopewa tu ile barua ama alivyosikia tu, kwa sababu kapewa barua ya mkono tu na kuambiwa kwamba usijali na hajapewa *official* mpaka sasa hivi. Siku ile ile wakati wa jua kali unaambiwa kenda kupanda mijiti ya kudumu, kwa sababu gani, kwa sababu kajua kuwa haki sio yake. Wewe wakati wa kaskazi uwende ukapande mchungwa, kweli inakubalika hiyo. Sasa hebu tuliangalie hili jamani na ndio maana tukawa tunasema hapa kwa sababu hatusemi kwa sababu tuna matatizo na viongozi wetu, hapana. Mimi nawapendeni sana viongozi wetu. Hakuna mimi kiongozi hata mmoja nisiyempenda hata siku moja hapa, lakini ni haki yangu. Mimi ninapofanya kosa nitakiri kosa, lakini linapokuwa hili jambo lipo basi tukubaliane na tuliweke sawa.

Mhe. Spika, tena kuna tatizo sasa hivi kubwa sana la Matemwe Muyuni. Kuna wananchi wameorodheshwa kule, wakaitwa na serikali kuambiwa nini serikali inataka kuelekeza lile suala, wananchi wako karimu sana na hawana tatizo lolote. Lakini hii *delay* yetu au huku kusita kwetu kuwafikia tena, ndipo pale tunawaweka hatuwatendei haki. Naomba mheshimiwa na hili wanakuita huko Matemwe Muyuni ukawasawazishie suala lao, wao hawana tatizo lolote na serikali yao ya kitaifa ya Zanzibar, hawana tatizo hilo kabisa.

Vile vile Mhe. Spika, huko huko watu wa Mtemwe Bangaloo wameonewa haki yao, Katibu Mkuu wangu wanamshukuru sana wa wizara hii ya ardhi, alifanya tathimini kama wizara yake husika. Lakini mpaka leo tunawapiga danadana tunawategemea nini wananchi wetu. Kwa hivyo, mimi naomba na hili tuwasaidie tuwaite hawa wadau, kwa sababu tathmini imeshafanywa ndani ya wizara husika na wizara husika ile ndio iliyopima na kutoa kibali. Namshukuru sana katibu aliifanya hiyo kazi vizuri sana, lakini nani mlipaji ndio tunamtafuta na ndio danadana ilivyokuwa hapa.

Kwa hivyo, mimi ningeomba hilo suala tulisaidie kwa nguvu zetu zote. Lakini jamani tukumbuke, Zanzibar kumetokea maajali zaidi ya mara mbili kuhusu habari ya vyombo vyetu vya baharini. Ametokea mfadhili huyu. Tulikwenda kama kamati sisi, tukaambiwa ngojeni kuna Kamati ya Uongozi wa Makatibu Wakuu, sijui ngojeni kuna nini. Hivi kweli jamani hawa jamaa zetu, ndugu zetu Wazanzibari wataona tunawatendea haki, kuna mfadhili yupo wa kuleta chombo hapa. Ningeomba wizara husika, hebu tuacheni yote jamani, tumruhusuni yule, tunakaa tunamchunguza mpaka lini na tumchunguze vipi jamani, kama tumeshamuona hafai, basi toweni ripoti waambieni wananchi kwamba huyu hafai, tunao mpango mwengine. Suala hili ningeomba sana kwamba tuwapatie Wazanzibari haraka sana meli ambayo ni ya uhakika, tusingojee tukapata ajali nyengine ndio tukakurupuka, maana yake ndio kawaida yetu kuwa ikitokea ajali ndio tunakurupuka.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, mimi naomba sana wizara husika haraka sana iweze kuwapatia chombo ndugu zetu, ili na wao wajisikie kuwa wanakwenda katika usafiri wa uhakika. Tusiwahini, tuwaruhusu. Mhe. Spika, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii kama nilivyosema kuwa kiriri hiki kinatakiwa kikae wakubwa tu, kuanzia mawaziri na wengine. Lakini mimi siwezi kukaa hapa na kama nilivyosema kuwa uwaziri mimi siutaki hata kidogo, kwa hivyo hapa sio nafasi yangu ya kucheza na kuweza kuogelea.

Kwa hayo machache Mhe. Spika, nasema kwamba mimi na wananchi wangu wa Jimbo la Kitope, tunaomba kutoa hoja. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Tunakushukuru Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwasilisha ripoti hiyo kwa niaba ya kamati na hapo hapo ukatoa na maoni binafsi kama Mwakilishi wa Jimbo. Basi tujadili ripoti hii. Tuanze na Mhe. Hija Hassan Hija, baadae Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, naomba na mimi nichukuwe fursa hii kukushukuru kwa kunipa nafasi asubuhi hii ili niweze kutoa mchango wangu mfupi sana kwenye ripoti hii ya Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi, iliyowasilishwa na mwanasheria mdogo Mhe. Makame Mshimba Mbarouk.

Mhe. Spika, nimpongeze Mhe. Mwenyekiti wa Kamati na wajumbe wake kwa jinsi walivyotuletea ripoti nzuri ambayo imefafanua juu ya mambo ambayo wameyaona. Mhe. Spika, kwenye ukurasa wa 215 wa ripoti hii

kuna changamoto inayoikabili idara ya nishati. Mhe. Mwenyekiti na wajumbe wake wamesema kwamba tatizo la idara ya nishati ni ukosefu wa wataalamu.

Mhe. Spika, mimi nitowe masikitiko yangu makubwa kwamba nchi yetu inaendelea kulalamika kwamba hatuna wataalamu bila ya kujipanga na kuwatayarisha wataalamu hao. Tumekuwa na ukosefu wa wataalamu katika idara mbali mbali na ripoti hii imesema kwamba idara ya nishati ina upungufu mkubwa wa wataalamu. Lakini Mhe. Spika, katika Baraza hili hili tuliahidiwa mara kadhaa kwamba serikali kwa kupitia wizara hii, itajitolea kuwasomesha wataalamu wa nishati na kwa kuanzia walituambia watawapeleka wanafunzi kumi, kwa ajili ya kusoma fani ya nishati ikiwemo mafuta na gesi. Sasa tuendelee kulalamika kwamba hatuna wataalamu, lakini serikali imeshindwa kuwasomesha vijana wetu kwa kuanzia ambao walituahidi wao wenyewe kwamba wamejipanga kuwasomesha vijana kumi kwa ajili ya fani hii ya nishati ikiwemo mafuta na gesi.

Sasa hii tabia ya kuendelea kulalamika tu wakati hatuchukuwi hatua yoyote, kwa kweli sio tabia nzuri na wala sio ustaarabu wa kuendesha mambo yetu. Mhe. Spika, nadhani kwamba tatizo la ukosefu wa wataalamu mbali mbali uwe wa nishati wa kada nyengine ni matatizo yenyewe ya kujitakia, yaani hatuna vipaumbele vya kujipangia kwa ajili ya kuwatayarisha wananchi wetu kwenye fani mbali mbali ikiwemo hii ya nishati.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, mimi nashauri vipaumbele vya kujipangia kwa ajili ya kuwatayarisha wananchi wetu kwenye fani mbali mbali ikiwemo hii ya nishati. Mhe. Spika, mimi nashauri kwamba angalau kwa kuanzia, Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati aanzie pale ambapo tulikubaliana kwamba angalau vijana wetu kumi, watapatiwa fani hii ya nishati. Lakini uchunguzi unaonesha kwamba hata idara yenyewe ya nishati serikali imekuwa ikiitenga, imekuwa kama idara yatima, imekuwa kama idara ambayo haina mashiko. Kwa hivyo, nadhani Mhe. Waziri aliyeko hivi sasa mimi namuomba sana kwa busara zake aweze kukaa na hawa watu wa nishati na kuweza kubadilishana mawazo na aangalie changamoto ambazo zinawakabili.

Mhe. Spika, idara hii ya nishaati kwa kweli ina changamoto nyingi, hivyo bila ya msaada wa Mhe. Waziri tutakuwa hatuna la kufanya. Kwa hivyo, namuomba sana Mhe. Waziri kwamba idara hii ya nishati ni idara muhimu na kwa kweli ina upungufu wa wataalamu na ni jambo la kujipanga sisi kama serikali kutafuta wataalamu hao na kuwasomesha.

Mhe. Spika, jengine ambalo ningegusia katika ripoti hii ni ukurasa wa 216. Kuna changamoto hapo kwenye Shirika la Umeme, tumeambiwa kwamba kuna uchache wa wafanyakazi, kwamba tuna wafanyakazi kidogo na hivyo kazi hazifanyiki kwa sababu wafanyakazi ni kidogo. Lakini ukiangalia matumizi ya shirika ya bilioni 9, kwa mishahara na kazi nyengine ndogo ndogo ni dhahiri inadhihirisha kwamba kuna wafanyakazi wengi. Kwa hivyo, mimi nadhani kwamba sio uchache wa wafanyakazi, lakini tumeajiri *manpower* kubwa ambayo sio wataalamu na hayo tumeyaona kwamba kuna watu wengi pale kwenye shirika na utaalamu wao ni mdogo. Kwa hivyo, huu sio uchache wa wataalamu, huu ni uwezo wa wataalamu wetu kwenye shirika na taasisi nyengine.

Kwa hivyo, ukiangalia matumizi tunayotumia ya mishahara na mambo mengine, bilioni 9 ni fedha nyingi kwa sehemu ya mishahara na kazi nyengine ndogo ndogo. Kwa hivyo, hapo ukiangalia sio tu kwamba wataalamu ni kidogo, lakini uwezo wao ni mdogo kuweza kufanyakazi ya shirika.

Mhe. Spika, jengine katika ukurasa wa 222 kwenye idara ya usafiri wa baharini. Hapa kuna changamoto, tumeambiwa kwamba kuna uchache wa wataalamu, kwa maana kwamba wataalamu watatu wamesimamishwa kazi baada ya kutokea ajali na hivi sasa amepatikana mtaalamu mmoja. Lakini la kushangazi kuwa tumekosa watatu lakini tumempata mmoja lakini Mhe. Mwenyekiti, anatuambia huyo mmoja hana sehemu ya kukaa, sasa watatu wa nini, ikiwa mmoja tumeshindwa kumpa ofisi, tunatafuta watatu wa nini na tuwaweke wapi. Kwa hivyo, nadhani Mhe. Spika, tuwe sambamba na vitendea kazi. Tunapowatafuta wataalamu wetu tuwape na vyenzo, ikiwa ni pamoja na ofisi na vitendea kazi vyengine. Sasa ikiwa mtu mmoja hadi hii leo hana sehemu ya kukaa, halafu tunawatafuta watu watatu tuwaweke wapi.

Mhe. Spika, mimi nadhani Mhe. Waziri ajipange vizuri, mbali na ukosefu huu wa wataalamu, lakini na sehemu ya kufanyakazi watalamu wetu tuwatengenezee. Mhe. Spika, kuna baadhi ya ofisi wataalamu wetu wanafanyakazi katika mazingira magumu. Wataalamu wa kada mbali mbali wanakaa katika ofisi moja, huo sio utaratibu wakufanya kazi.

Mhe. Spika, jengine kwenye ripoti hii ni kuhusu idara ya *UUB*. Idara hii imekuwa ikishirikiana na wananchi kutengeneza barabara zetu za ndani, lakini mimi huwa najiuliza kwa nini idara hii haifanyikazi wakati ule ambao kunakuwa na kiangazi, wanasubiri kipindi cha masika ndio waanze kufanya kazi. Mhe. Spika, barabara

ya Mjini ni tofauti na barabara zetu za ndani, barabara za ndani vijijini zinakuwa na udongo mbya, kwa hivyo mvua zikiisha hata ukifanya kazi hiyo ya kusafisha ni kazi bure.

Mhe. Spika, mimi ningependa kushauri kwamba idara hii wajipange na wajuwe kwamba barabara zipi zinahitaji matengenezo wakati wa kiangazi na zipi zinahitaji matengenezo wakati wa mvua. Vyenginevyo tu kiendelea kufanya kazi wakati wa mvua na hatimaye inakuwa hakuna faida tunayoipata.

Mhe. Spika, sambamba na hilo idara hii nadhani inaupungufu wa vitendea kazi. Mhe. Waziri kuna haja ya kukaa na wataalamu wake wa idara hii ili kutafuta vitendea kazi kwa ajili ya kuifanya hii kazi kwa ufanisi. Inasikitisha sana kuona kuwa idara inahitajika majimboni na mikoani lakini vitendea kazi hawana. Kwa hivyo, namshauri Mhe. Waziri kwamba kuna haja ya kujipanga idara hii ili kutafuta vitendea kazi kwa ajili ya kuwawezesha wataalamu hawa kuweza kufanya kazi mbali mbali.

Mhe. Spika, suala jengine ni kuhusu makampuni ya simu. Tumetoa kilio muda mrefu kwamba baadhi ya makampuni ya simu hayatowi minara yake ikaweza kupatikana vijijini. Tumesema zaidi ya mara sita kwamba kuna mnara wa Tigo kule Mtambile, lakini wananchi wenyewe wa Mtambile, Kiwani, Kangani na Chambani hawafaidiki. Ziko tetesi kwamba wanafaidika wanafaidika wananchi wa Nungwi na mnara ule wa Mtambile. Kwa hivyo, hatuoni faida ya kujengewa mnara ule kule Mtambile.

Mhe. Spika, suala hili tumeambiwa mara nyingi kwamba linafanyiwa kazi, lakini ni mwaka wa pili huu sasa hatuna matunda ya mnara ule. Kwa hivyo, mimi namuomba Mhe. Waziri basi atuambie ule mnara lengo lake hasa ni nini. Kwa sababu mwananchi jirani na Mtambile, Chambani, Kiwani na Mwambe hawafaidiki na mnara ule na badala yake tunaambiwa kwamba ukiwa katika maeneo ya Nungwi basi mnara wa Mtambile unajisoma kwenye simu yako. Kwa hivyo, Mhe. Spika, tunamuomba Mhe. Waziri atusaidie, kama hakuna haja kule Mtambile basi ule mnara uondoshwe, kwa sababu hatuoni faida wananchi kwa mnara ule kuwekewa kitu ambacho hakitusaidii.

Mhe. Spika, jengine sisi ni *shareholders* wa kampuni ya Zantel, lakini tumekuwa tukikatwa fedha kwenye simu zetu bila ya matakwa. Unaweza ukaamka asubuhi tu ukaambiwa umejiunga na huduma fulani, bila kushauriwa na bila ya wewe mwenyewe kutaka na hatimaye wananchi wanakatwa fedha bila ya matakwa yao. Kwa mfano, kila mwananchi akikatwa shilingi 600/= kwa mwezi, itakuwa ni milioni ngapi kwa wateja wetu wa Tanzania, tukijua kuwa Shirika hili la Zantel lina wateja zaidi ya bilioni moja. Sasa ikiwa kuna wateja zaidi ya bilioni moja na kila mteja anakatwa shilingi 600/= tufikirie ni shilingi ngapi. Kwa hivyo, Mhe. Spika, nadhani kuna haja wateja wetu kuarifiwa na kushauriwa kuhusu huduma ambazo wanahitaji kuingia, kuliko mitambo tu ya Zantel kukata bila ya ushauri wa mteja mwenyewe.

Jengine Mhe. Spika, ambalo ningependa kuzungumza, ni kuhusu suala zima la Shirika la Meli. Nadhani serikali sasa hivi imefika wakati watukubalie. Shirika la Meli limekuwa na tatizo kwa muda mrefu, watendaji wetu pale wanafanyakazi ngumu bila ya mafanikio. Naiomba sana serikali Mhe. Spika, iondoshe hili tatizo la usikivu, sasa watusikilize. Shirika la Meli sasa limekuwa ni mzigo. Haiwezekani kabisa kwamba meli moja ipelekwe matengenezoni kwa mwaka mmoja mara tatu, hilo ni tatizo. Mzigo huu unawakumba wananchi wanyonge. Kwa hivyo, njia pekee ya kulisaidia shirika hili ni kuwawezesha kupata mtaji na kuweza kununua meli nyengine pamoja na kuiuza meli iliopo.

Mhe. Spika, Mhe. Naibu Waziri yupo karibu yangu hapa nimuombe sana kwamba hoja ya Shirika la Meli kwa kweli watusaidie na watusaidie kwa maana ya kuwawezesha, pamoja na kuuza meli ambazo hazina faida na sisi. Meli ambayo sasa hivi tunayo inapelekwa matengenezoni kwa mwaka mara tatu, ni tatizo na ni mzigo mkubwa kwa wananchi wanyonge wa Zanzibar.

Mhe. Spika, mwisho kabisa nizungumzie suala zima la migogoro ya ardhi ambalo Mwenyekiti alilizungumza.

Mhe. Spika: Zungumza kwa dakika tatu tu.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, mimi nitowe nasaha tu kwamba migogoro ya ardhi imekuwa ni mikubwa, wananchi wanapata tabu sana. Ni wakati sasa kwa serikali kusimamia hali hii ili matatizo ya ardhi yaondokane kwa Unguja na Pemba na wananchi wapate fursa zao na haki zao za ardhi.

Mhe. Spika, baada ya hayo naunga mkono ripoti hii ya kamati.

Mhe. Spika: Ahsante sana, Waheshimiwa Wajumbe tujitahidini na ratiba yetu.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Ahsante sana Mhe. Spika, kunipa nafasi hii na mimi kuchangia ripoti hii ya Kamati ya Mawasiliano na Uchukuzi. Kwanza nimpongeze Mhe. Mwenyekiti, wa Kamati hii kwa ripoti yake nzuri na kuwaiwasilisha katika Baraza letu hili la Wawakilishi.

Mhe. Spika, baada ya hapo niende katika Idara ya Urdhi, Upimaji na Ramani. Pamoja na chagamoto hizi zinazoikabili Idara hii ya Upimaji bado zipo changamoto ambazo zinaikabili Idara hii pamoja na wananchi kwa ujumla. Kwa kuwa serikali yetu imejipanga vizuri kuanzia ngazi ya Shina mpaka Taifa ili kukabiliana matatizo yanayotokea katika nchi. Inaonekana kitu chochote katika nchi kinapoingia ni lazima kiwasilishwe katika Idara husika au katika vyombo husika.

Mhe. Spika, je, leo inakuwaje watendaji wale wale ambao wanaona ardhi ya serikali inavamiwa na wananchi ikawa habari zile havifiki katika vyombo husika. Hili ni tatizo ambalo linaiathiri sana nchi yetu. Ingekuwa viongozi hao hao wanasimamia vizuri migogoro hii ya ardhi nadhani ingekuwa hakuna matatizo katika serikali yetu.

Mhe. Spika, chengine ni pale ambapo wananchi wamepatiwa ardhi wahusika wale wale wanashindwa kuwaelekeza wananchi wale namna ya ujenzi wajenge plani gani au namna ya ujenzi wajenge vipi. Utakutia mtu anajenga nyumba kaelekeza Kaskazi, huyu mwengine kaelekeza kusini, plani ya mji wetu hasa inakuwa hairidhishi. Kibaya zaidi hata zile barabara ambazo nyumba zimejengwa kwa master plan zinashindwa kuwekewa kifusi na nyumba zile zinabaki kuwa kama magofi. Kwa sababu inakuwa hazina plani na barabara hamna nyumba zile inakuwa kama zimelizozeeka.

Mhe. Spika, kwa hiyo naiyomba serikali pamoja na wizara sasa wakati umefika wa kuwaelekeza wananchi wetu namna ya ujenzi gani tujenge ili kuiletea haiba ya nchi yetu pamoja na miji yetu.

Mhe. Spika, niende katika Mamlaka ya Maji (ZAWA). Pamoja na usambazaji wa maji vijijini bado vipo vijiji havijananufaika bado na maji, kuanzia Unguja mpaka Pemba bado kuna matato ya maji vijijini na bado kuna matatizo ya visima katika vijiji. Kwa hivyo ningeishauri Mamlaka hii kuyafanyia utafiti maeneo yale ambayo hayana majo na wakayafanyia utafiti maeneo yale ambayo yanapatikana maji ili kuwasambazia wananchi wetu hawa na kuondokana na usumbufu.

Mhe. Spika, kwa mfano Bandari ya Mkoani, pale kipo kisima ambacho walichimba wajenzi wa gati ile ya Mkoani. Ningeshauri Mamlaka ya Maji ikakifanyia utafiti kisima kile aidha ikiwa ni kisima kilichokuwa na maji ili kichimbwe kisima kile wasambaziwe wananchi wetu. Mhe. Spika, pia ningeishauri mamlaka ya maji iangalie sana tatizo hili la umwagaji wa maji ovyo, kwa sababu vipo vijiji au wapo wananchi huwa wanamwaga maji ovyo na hali ya kuwa wapo wenzetu ambao maji yale wanayatafuta hawayapati. Kwa hivyo naomba Mamlaka hii itetee sana suala hili la umwagaji ovyo wa maji vijijini.

Mhe. Spika, mwisho nende katika Shirika la Umeme. Pamoja na nia njema ya kuanzishwa laini kubwa za umeme ili kukidhi mahitaji ya umeme lakini bado zipo changamoto kubwa kwenye ukusanyaji wa mapato makubwa ambayo wananchi wetu imai zao zimewatoka kabisa. Wananchi sasa hivi wanatetea sana mapato yanayokatwa ni makubwa katika Shirika la Umeme. Utamkutia mtu ndani hana friji, hana feni, hana jiko lakini mtu yule unamkutia makato yake anayokatwa ni makubwa. Ni vyema Mhe. Spika, Shirika ikawafungia mita za kisasa wananchi wale ili kuondokana na usumbufu huo. Ahsante Mhe. Spika, nakushukuru.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii kuchangia machache. Kwanza namshukuru Allah kwa kutupa uhai na uzima na kuweza kutupa taufiqi ya kuzungumza.

Mhe. Spika, nikiwa ni mmoja kati ya Wajumbe wa Kamati hii nikiwa ni Makamo Mwenyekiti, napenda nisisitize tu kwanza bila ya wasi wasi wowote ripoti yetu naiyunga mkono. Lakini kuna dondoo muhimu naomba nizitilie mkazo kwa Wizara zote mbili.

Mhe. Spika, kwanza kuhusu suala la Sera na Ufatiliaji wa Nishati hapa Zanzibar. Hili nataka nilipe uzito kwa sababu sisi bado hatujakwenda katika viwanda. Wenzetu wengi katika ulimwengu ambao walikuwa wakitegemea asilimia kubwa ya pato lao la taifa iwe ni kilimo lakini walikaa wakaanza kudumaa muda mrefu.

Wiki moja iliyopita Mhe. Spika, Balozi ya Indonesia alikuwa akitoa maelezo yake katika kipindi kimoja cha ITV alisema kuwa wao walikuwa wakitegemea sana kilimo na walipoona uchumi unadumaa wakaelekea

kwenye viwanda. Lakini hawakukiacha kilimo, sasa asilimia 46 ya pato lao la taifa linatokana na viwanda. Juzi wiki iliyopita vile vile nimesikia taarifa kutoka Pakistan wanasema kutokana na tatizo la nishati ambalo wamekumbana nalo Pakistan, hivi sasa baadhi ya viwanda vingi vinaanza kufungwa.

Sasa ukichukua balance hiyo kwamba huku kuna nchi zinaelekea katika viwanda na zinafanyikiwa lakini huku nchi ambazo tayari zilikuwa zina viwanda zimepata tatizo la nishati, hawana nishati ya kutosha viwanda vinaanza kufungwa. Sasa sisi ambao ni wadogo hatujaingia kokote kule, hatujatoka kwenye kilimo kuingia katika viwanda wala hatujakuwa na utaratibu wa kupata nishati yetu. Inabidi tujifunze hapa umuhimu wa kupata nishati yetu wenyewe ambayo itatuhakikishia uwezo wetu wa kuendeleza katika viwanda utakuwa ni mzuri. Kwa hivyo naiyomba sana serikali hapa kupitia Wizara hii ya Maji, Nishati na Ujenzi, kwamba wafanye utafiti kama upo uendelee lakini kuhakikisha kwamba Zanzibar inatoa. *alternative energy* ya kuweza kuendeleza mambo ya umeme na mambo mengineyo ya uzalishaji.

Mhe. Spika, la pili ni suala la uungwaji umeme na ZECO wakati tunaingia katika uungwaji umeme wa kutoka Tanga kuja Pemba nilizungumza miye katika Baraza hili kwamba hapa sasa tutegemee maombi yatakuwa makubwa zaidi kwa hivyo Shirika liweze kujitayarisha. Karibuni hivi nilizungumza na Meneja ya Shirika Pemba, jibu lake lilikuwa kabla ya umeme kuungwa kutoka Tanga kuja Pemba walikuwa wakipata maombi 20 mpaka 30 tu kwa mwezi ya uungwaji umeme. Sasa wanapata kiasi ya 200 mpaka 250 maombi ya kuunga umeme wananchi. Ni *jump* kubwa sana, lakini bahati mbaya unapokwenda hakuna zana za kuungiwa huo umeme. Sasa tunaiyomba basi Wizara kupitia hili Shirika ikaliona tatizo hilo wananchi wanakaa muda mrefu sana bila ya kuungiwa umeme na wanakwenda wanarudi.

Mimi Mheshimiwa ni shahidi, mimi nilipeleka ombo la kuungwa umeme pahali ambao ni Msikiti sasa hivi huu ni mwezi wan ne (4) hakuja kuwa na dalili kwamba lini utaungwa umeme ule. Hili ni tatizo, lile ni Shirika linatakiwe liwe la kibiashara lakini ikiwa wananchi wengi namna hiyo hawajaungiwa umeme ni tatizo.

Kuna sehemu B kuna baadhi ya vijiji havijafikiwa na umeme ule. Bado serikali iliwaku inaiachia Shirika si kazi yao ya moja kwa moja. Kwa hivyo hapa tunaiyomba Wizara iangalie utaratibu wa kuvifikia vijiji hivyo ili na wao waweze kupata hiyo nafasi ya kuungiwa umeme.

Nikitoka katika Wizara hiyo nakuja katika Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano, nina mambo machache ya kutilia mkazo. Kwanza Mhe. Spika, kama nilivyouliza juzi swali langu la Kiwanja cha Ndege cha Pemba. Mimi nahisi kwamba tunapojibu Maswali tukasema kwa nyakati za usiku haiwezi kutua ndege Pemba hili kidogo linapunguza uzito wa lile suala. Tatizo lipo usiku na mchana, ikiwa hali ya hewa itabadilika na mchana haiwezii kutua ndege Pemba. Tatizo hizi ndege kubwa Mheshimiwa huwa zinachukua mafuta mengi lakini vile videge vidogo ambavyo ndio zinazokwenda zaidi Pemba mafuta yake huwa kidogo. Ikiwa haiwezi kutua pale ikaanza kuzunguuka kusema kwamba labda itapata nafasi wakija wakishtuka mafuta yameshapungua hakuna mafuta ya kuwarejesha Unguja kwa kikamilifu wala hakuna uwezekano wa kutua pale, sasa sijui watafanya nini.

Mimi nafikiria muda wa kulifikiria suala la kutiwa taa uwanja wa Pemba kwa kweli hakuna tena muda, tumeshapitwa na muda. Hivi sasa Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano imeshachelewa hasa kutia taa pemba, sasa lazima watie hakuna njia nyengine.

Mhe. Spika, la pili ni suala la mamlaka ya usafiri Baharini. Mimi nafikiria kwamba mbali ya kama ilivyoeleza ripoti yetu sisi tulipata nafasi ya kwenda kutembelea Bandari ya Dar-es-Salaam na Banda ya Tanga. Wakati wa ziara yetu ya Bandari ya Dar-es-Salaam tulikwenda katika kituo cha Mamlaka ya Usafiri kilichopo Kigamboni kina vyombo ambavyo wanaviona vyombo vya baharini na wanafanya mawasiliano navyo. Sisi Mamlaka ya usafiri baharini ina *radiocall* tu haina vyombo vya kisasa vya kuangalia vyombo baharini. Katika huo mchakato mpya wa kuijenga Mamlaka ya Usafiri Baharini ni kupatiwa eneo ambalo watakuwa na zana za kisasa za kufuatilia utaratibu wa nyenendo za vyombo baharini baina ya Unguja na Dar-es-Salaam na Unguja na Pemba. Hapo sasa ndio tutaingia karne ya kweli ya teknolojia ya kisasa na digital.

Mhe. Spika, la tatu katika Wizara hii ni juu ya tatizo la *exit* ya *stand* Pemba Chakechake. Suala hili Mhe. Spika, mara baada ya kuingia katika Baraza hili katika kipindi hichi cha 2010, kamati ilipoanza tu kazi tulilianza suala hili kulizungumza. Bahati nzuri Mhe. Naibu Waziri alilijibu uzuri juzi katika suala aliloulizwa na Mhe. Mbwana, namshukuru sana. Tatizo kuna kitu kimoja tu kilichotanza, basi Wizara zote mbili kwa ushirikiano kitu hicho kimoja kiwe ni tatizo. Tuliwaambia kama mlikwama basi tuambieni siye kamati, tutatafuta njia ya kukwamua ni suala la nyumba moja tu, ambalo lilikuwa na watu wawili katika kipindi tofauti. Tulipoanza kazi za kamati na kulifuatilia hili jambo alikuwepo mtu mwengine, ndani ya shughuli zetu akapasiwa mtu mwengine. Sasa ile *delaying* iliyotokezea ndiyo yaliyotokezea haya, kila tukichelewa huenda akapasiwa wa tatu.

Mimi nawaomba sana Waheshimiwa Mawaziri wote wawili, Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano na Wizara ya Maji, Nishati, Ardhi na Makaazi, tulitizame hili suala. Pele nimeambiwa zinaingia gari za abiria tu lakini kuna gari za *private* zinaingiza gari za mizigo zinaingia lakini *entrance* ni moja na *exit* ndiyo hiyo hiyo. Bahati nzuri Wizara ya mawasiliano ilikwishatoa ahadi kwamba wao watafanya ujenzi kupitia mfuko wa barabara, lakini hili ni letu sote Wizara zote mbili. Nawaomba Waheshimiwa walifuatilie sana.

Mhe. Spika, mwisho kabisa katika wizara hii. Juzi niliuliza swali lakini kwa bahati sikupata maelezo ya kina. Suala la njia ya Mkoani mpaka Wete ile barabara miye siikumbuki ilijengwa lini lakini tokewa nizaliwe miye sijaona kuongezwa zaidi ya zile njia za mjini Chakechake, Wete na Mkoani, lakini ile inayopita baina ya miji haijawahi kuongezwa na traffic sasa hivi wameongezeka sana, upanda wa wingi wa magari yameongezeka lakini barabara inabakia ile ile.

Hivi Karibuni tulikwenda na mwenzetu mmoja yeye ni dereva mzuri hapa, lakini akasema miye kuendesha gari njia ya Mkoani siwezi. Alikuja ndugu yangu mmoja hapa akanambia kwa kule Arabuni njia kama zile zinaitwa *twariqqil maut* yaani njia za kifo. Maana yake wewe katika kila dakika basi unaweza kutokeana na mwenzako uso kwa macho. Kidogo nilisikitishwa sana na jibu la Mhe. Waziri akasema kwamba hawajawa na mpango wa kuitanua barabara ya Mkoani /Chake na hali iliyo ile. Naomba sana katika hiyo *master plan* ya Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano basi ifikirie suala hilo. Kwa sababu bila ya kulifikiria wakati plan halitotokea mpaka lifikiriwe liwe *planed,* halafu ndio litatokea baada ya bajet kuruhusu la ikiwa hawawezi kuitanua basi wajenge juu, gari zinazokwenda zipite chini zinazorudi zipite juu, *solution* lazima ipatikane.

Mhe. Spika, mwisho kabisa nafurahi kusikia kwamba Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano inalishughulikia kwa karibu kabisa suala la upatikanaji wa meli. Naomba kasi izidishwe ili wananchi na wao wapate nafuu ya kuweza kuona kwamba wamepata meli kwa muda ambao sio mrefu.
Mhe. Spika, baada ya hayo nakushukuru sana na naomba kuunga mkono ripoti ya kamati yetu wenyewe. Ahsante.

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kupata nafasi hii ya kuchangia machache juu ya kamati hii. Kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa asubuhi hii kutuwezesha kufika hapa tukiwa na uzima wetu tulionao na kuja kufanya kazi zetu za kawaida za Baraza. Pia nimpongeze Mwenyekiti wa Kamati hii kwa kuwasilisha kwake uzuri ripoti ya Kamati yake.

Mhe. Spika, ripoti hii imekusanya utekelezaji wa kazi za Wizara mbili kubwa na muhimu, wizara ambazo kila moja ukiangalia utaikutia kuwa ni muhimu kuliko nyengine ni kama kiwili wili cha mwanadamu, kila sehemu ni muhimu kuliko nyengine. Mwanadamu anapoumwa popote pale anasema ni hatari anapoumwa na jicho anasema hili linauma zaidi, mwengine anaema aah bora kidole, mwangine anasema bora tumbo. Hii inaoneshea kuwa kila sehemu ni muhimu kuliko nyengine au sawa na nyengine. Kwa hivyo na Wizara mbili hizi zina majukumu makubwa na muhimu katika maisha ya watu wetu.

Mhe. Spika, mimi sitaki niseme sana lakini nataka nianze kidogo na Mamlaka ya Maji. Zamani nilipokuwa nasoma *Primary* tulitunga insha ya kiingereza inasema *importance of water* yaani umuhimu wa maji. Maji yakatajwa vyanzo vyake na umuhimu wake lakini mwisho mtungaji wa insha hii kwa sababu ilikuwa imetungwa sisi tumeipokea tu alisema “ni wale tu wanaoishi katika majangwa ndio wanaojua umuhimu wa maji katika thamani yake halisi” kwa kiingereza alisema *“It is only those who live in desert areas that know region of water at its raw worse*”.Wazanzibari hatupo jangwani lakini tunaujua umuhimu wa maji kuliko wanaoishi jangwani. Kwa sababu paipu za maji zimesambaa ulimwengu mzima lakini upatikanaji wa maji ni mdogo mno. Maji katika sehemu nyingi ya Zanzibar yameekewea mpango wa kupatikana.

Mheshimiwa mipango mengine ni kinyume na utaratibu. Haiwezekani kuwa mwananchi apate maji leo lakini kesho na kushokutwa awe hana maji, maji ni jambo la lazima ni jambo la kila siku. Kwa hivyo kuweka utaratibu wa maji ni kinyume na utaratibu wa maisha. Maji hayana utaratibu kwamba leo mtu apate maji na halafu siku ya pili sio zamu yake, kwani mtu anataka maji ya kunywa, maji ya kukoga kama unavyotaka kila siku. Kwa hivyo, mimi naiomba mamlaka hii ijitahidi ili iweze kuhakikisha kwamba mwananchi kila siku anapata mahitaji ya maji kwani ni lazima katika maisha yetu. Mhe. Spika, wako watu wenye uwezo wa kuhifadhi maji hata ya mwezi mmoja, lakini kuna watu hawana uwezo wa kuyahifadhi hata yale ya siku moja.

Mhe. Spika, mimi naona kwamba kungeliwekwa utaratibu mzuri kwani hawa wa chini hizi siku nyengine ambazo sio zamu yao maji watayapata wapi? Kwa hivyo, utaratibu mwengine mimi naona ni kinyume na taratibu za kimaisha hapa kwetu hua hazifai.

Mhe. Spika, sasa nije katika Jimbo langu la Mtambile, ni kwamba jimbo langu lina matatizo makubwa ya maji pamoja na kua pengine kila kijiji ziko *pump* za maji lakini maji hayo hayapatikani na visima vya maji havitoshi, *machine* za kusukuma maji ni chache. Kwa hivyo, mahitaji ni makubwa kuliko uwezo wa miundombinu ya maji iliyopo, hivyo hali hii sio ya jana wala ya juzi.

Mhe. Spika, kule Kengeja kuna majumba yale ya maendeleo yaliyojengwa tokea enzi za Mhe. Rais wa kwanza, hapo mwanzo maji yalikua yanafika ghorofa ya tatu leo pale chini basi maji hayapo. Hii ni kuonesha kwamba badala ya sisi kwenda mbele na maendeleo basi tunarudi nyuma katika sekta hii ya maji. Kwa hivyo, mimi naomba marekebisho ya haraka ya kuweza kudhibiti hali hii ya maji inahitajika na Mhe. Spika, maji ardhini yamo. Kwa hivyo, imani yangu mimi ni kwamba bado hatujakua na upungufu wa maji kiasi hicho ikawa watu hawapati maji.

Mhe. Spika, sasa niingie kidogo katika Mahakama ya Ardhi. Mhe. Spika, katika nchi yetu hii kila sehemu ndogo ya ardhi ina mmiliki wake. Mhe. Spika, hebu toka siku moja uje kwetu kuna sehemu hii ni pori haina mwenyewe ujaribu kulima na kupanda miti, basi atatokea mtu akuulize ee bwana mkubwa namna gani, nani amekuruhusu hapa, basi akikuuliza hivyo ujue ni mmiliki.

Mhe. Spika, Mahakama hii imepewa kazi kubwa, ngumu na nzito kwa sababu inahusiana na kutenda haki katika hukumu za ardhi. Imani yangu kwa Majaji kwa sababu ni Mahakama itakua ni wana sheria, lakini pia Mahakama hii ina wazee wa Mahakama. Mhe. Spika, kwa kua wanashughulikia jambo zito kabisa basi wazee hawa wa Mahakama wanahitaji kupatiwa maposho na marupurupu ambayo yatawawezesha kufanya kazi zao vizuri.

Mhe. Spika, Mahakama hizi zina mrundikano wa kesi kwa mfano hapa imeelezwa kwa Pemba katika kipindi cha Julai/Novemba kuliwasilishwa kesi 30, lakini zilizopatiwa maamuzi ni kesi 3 tu. Je, mpaka lini kesi hizi zitamalizika ikiwa kwa miezi 5 kesi zilizomalizika ni 3 kwa wakati huu ni 30 lakini huko nyuma ziko nyengine, hivi sasa Mahakama hiyo ya Pemba ina jumla ya kesi 222 ambazo zinangoja kupatiwa ufumbuzi.

Mhe. Spika, sina hakika Mahakama hii inafanya kazi vipi kwa kila siku au wiki mara moja au mwaka mara mbili. Lakini kwa hali yoyote wanayofanya kazi kama juhudu za makusudi nyengine hazijachukuliwa matatizo haya ya ardhi hayatomalizika na hapa itakua ni serikali kwa sababu Mahakama ipo lakini pengine haina uwezo wa kutosha kuweza kuzimaliza hizi Mahakama. Sina hakika ukiacha hao Mahakimu hawa wazee wa Mahakama wanayo taaluma angalau ya hii sheria, au wapo tu pale wameteuliwa kwa sababu nyengine zozote. Mhe. Spika, hili ni jambo la kisheria la Mahakama ni vyema kila atakayekuwepo pale basi awe na taaluma angalau ndogo ya ile kazi anayoifanya.

Mhe. Spika, kwa upande wa Unguja ziko kesi 86 za Mahakama ya Ardhi na kwa kipindi hicho ni kesi 2 tu ndizo ambazo zilizopata ufumbuzi. Mhe. Spika, tunafanya nini, tunakwenda wapi sisi tunaunda Mahakama ambazo utendaji wake wa kazi ndio huo.

Mhe. Spika: Mheshimiwa Mjumbe, malizia dakika zako tano.

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Mhe. Spika, nije kwenye sehemu ya miundombinu na mawasiliano kidogo juu ya barabara. Mhe. Spika, ni kwamba barabara zimejengwa nyingi Unguja na Pemba na mashirika pamoja na makampuni mbali mbali. Lakini Mhe. Spika, ziko barabara unapotembea zaidi ya jimbo langu chombo kinakwenda mtumbwi baharini hua kinapanda na kushuka. Mhe. Spika, ina maana katika hali hii baadhi ya barabara zimekosa kiwango na ubora wa barabara kwa sababu vyombo vinakwenda katika hali ya mawimbi. Halafu kuna *feeder road* moja ndogo Mhe. Spika, kwenye jimbo langu kutoka Kangani kwenda Kuukuu kuna kipindi Mhe. Waziri aliahidi hapa kua ile barabara ataitia kifusi ili angalau iweze kupitika kwa wakati wote. Mhe. Spika, naomba nimkumbushe Mhe. Waziri ile barabara aishughulikie kwa sababu Kuukuu na Kangani ni kugumu wakati wa mvua.

Mhe. Spika, baada ya hayo machache naunga mkono hoja hii, ahsante sana.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, labda nielekeza jambo moja tunachangia ripoti, hatuchangii kama vile tuko kwenye bajeti tumejaribu kwenda kwenye ripoti hii tutapozungumzia baadhi ya matatizo ya kijiji kimoja kimoja, hii imekua kama ni mfumo tunajadili bajeti. Lakini kwa kweli tunachangia ripoti hii ambayo hatimae mwenyekiti afanye majumuisho baada ya kupata maelezo kutoka kwa mawaziri wanaohusika. Kwa hivyo,

niwaombe basi tuwe tunakwenda kwenye ripoti moja kwa moja na tujitahidi sana tutumie muda mfupi kwa sababu muda kwa kweli umekwenda mno. Nashukuru ahsanteni sana.

Mhe. Hassan Hamad Omar: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa fursa hii kuchangia Ripoti ya Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi, na mimi kama ulivyoniambia mheshimiwa nitatumia muda mfupi kwa sababu mimi mwenyewe ni mjumbe wa kamati hii, nataka kuweka msisitizo tu katika yale maeneo yaliyonigusa zaidi.

Mhe. Spika, kwanza nichukue fursa hii kumpongeza Mhe. Mwenyekiti wa Kamati yetu ya Mawasiliano na Ujenzi kwa uwasilishaji wake mzuri aliowasilisha pale. Mhe. Spika, baada ya kumpongeza Mhe. Mwenyekiti, niende moja kwa moja katika mchango wangu ili kujali muda wetu.

Mhe. Spika, niende kwenye ukurasa wa 220 katika Shirika la Bandari. Mhe. Spika, kwa kweli Shirika la Bandari linafanya kazi zake vizuri lakini limekabiliwa na changamoto ambazo ni muhimu sana kuzifanyia kazi. Kwanza kabisa ndani ya bandari yetu ya Unguja katika upande wa Kusini bandari hii inaanza kujifukia, mchanga umekua mwingi na bado wataalamu wameshaifanyia utafiti na inajikweza siku hadi siku. Mhe. Spika, itafikia mahali tutakuja kukwama moja kwa moja. Kwa hivyo, naiomba wizara husika jambo hili walishughulikie kabla hatujapata madhara makubwa sana.

Mhe. Spika, vile vile katika Shirika hili la Bandari kuna mambo ambayo tunakosa vitendea kazi vya kisasa ikiwemo tagi ya kufanyia kazi pale. Mhe. Spika, kuna wakati mwengine wanapata usumbufu mkubwa meli kutoka nje zinashindwa kufunga gati pale kwamba tagi iliyopo haikidhi haja. Lakini tagi hizi ninazozitaja ni za bei mbaya sana, lazima shirika hili lijipange vizuri pamoja na kushirikiana na wizara ili waweze kulitatua tatizo hili. Mhe. Spika, haitoshi katika Shirika hili la Bandari tumepata kutembelea kama Mhe. Rashid Seif Suleiman alivyotembelea pale bandari ya Dar es Salaam mazingira yake ni mazuri mno kwa wasafiri. Lakini ukiangalia bandari yetu ya hapa Unguja mazingira yake yako finyu vibaya sana, hasa ukilinganisha wakati huu wa mvua.

Mhe. Spika, hivi juzi nimetembelea pale bandarini kuna vyombo visivyopungua kama vinne, vyombo viwili vilikuwa vinakwenda Pemba na vyombo viwili vilikuwa vinakwenda Dar es Salaam, basi huo msongomano wa watu ni mkubwa mno na wakati huu wa mvua hakuna mandhari nzuri ile sehemu iliyopo ya kukaa abiria kusubiri usafiri haitoshi kabisa. Kwa hivyo, tunawaomba Shirika la Bandari kwa kushirikiana na wizara walishughulikie hilo, kuna banda pale linatiwa pikipiki pale basi kama litatengenezwa basi tunaweza kuishinda hata Dar es Salaam kwa mazingira mazuri. Mhe. Spika, mimi nathubutu kusema kwamba ni afadhali ya Pemba kuna banda zuri la kukaa abiria kuliko hapa Unguja.

Mhe. Spika, tukenda katika ukurasa wa 210 Mahakama ya Ardhi, katika Mahakama ya Ardhi tulipotembelea kuna matatizo makubwa na usumbufu mkubwa wanaoupata wananchi wetu kutokana na mambo ambayo ni usumbufu. Mhe. Spika, kwanza katika Mahakama ya Ardhi ilioko Wete ina upungufu wa Hakimu, pale Hakimu ni mmoja tu na anakuja kwa siku maalum kwa sababu anashughulikia kesi za Wilaya. Kwa hivyo, wana Mahakama nzuri sana ya Ardhi lakini ukosefu wetu ni Hakimu na usumbufu unatokea siku hadi siku na kesi hizi za ardhi kila siku ya Mwenyezi Mungu zinawasilishwa jambo ambalo inakua ni matatizo. Kwa hivyo, tunaiomba wizara na hili ilishughulikie kwa kina ili kesi ziendelee siku zote isipokua siku za mapumziko tu.

Mhe. Spika, ukiangalia Mahakama ya Ardhi hapa Unguja wana sehemu ndogo sana utafikiri sehemu ya mama ntilie tu, ile sehemu inatisha kweli kweli pamoja na kwamba ofisi sio lazima iwe kubwa lakini sio ufinyu kama ule. Halafu kunakua na upungufu wa bajeti hapa, bajeti ni kwamba haikidhi haja mpaka mwenyekiti au Hakimu yule anasema anashindwa kununua karatasi za kuendeshea kesi, hilo ni tatizo kubwa sana na linaleta usumbufu mkubwa sana. Kwa hivyo, tunaomba wizara husika ilishughulikie tatizo hilo na kulipatia ufumbuzi pale katika Mahakama ya Pemba kuanzia mwezi wa Julai mpaka Januari kuna kesi 30 za Mahakama ya Ardhi, lakini zilizoshughulikiwa na kupewa hukumu ni 2 tu, hili ni tatizo na zilizowasilishwa ni nyingi kuliko zilizotolewa hukumu.

Mhe. Spika, ukiangalia kwa upande wa Unguja kesi 86 zilizowasilishwa kutoka Julai mpaka Januari zilizotolewa hukumu ni kesi 3 ni usumbufu wa kutosha. Mhe. Spika, kuna haja ya kujipanga vizuri na kuweza kutatua mambo haya ili wananchi wetu wapate mafanikio kutokana na madai yao au kesi wanazozipeleka.

Mhe. Spika, vile vile tulitembelea katika Mamlaka ya Viwanja vya Ndege hapa Unguja kwa kweli hali sio mbaya sana, lakini kulikua na sehemu ambazo zilikua zinahitaji matengenezo. Mhe. Spika, lakini nashukuru mpaka nazungumza hapa kuna yale tuliyoyaona kwamba wameshayafanyia kazi, moja ikiwa ni *parking* ya gari za abiria tayari nimepata taarifa kwamba taa zimeshawekwa. Mhe. Spika, kwa hivyo, tunawashukuru sana Mamlaka ya Viwanja vya Ndege kwa hatua walizozichukua na tunawapongeza sana kwa jambo hili.

Mhe. Spika, tukija kwenye ukurasa wa 226 Idara ya Ujenzi na Utunzaji wa Barabara (*UUB*). Mhe. Spika, tunatoa tamko kwamba tunapojenga barabara zetu lazima ziwekewe mitaro kwamba hizi zinaimarisha zile barabara kuwa makini na halafu wananchi hawaathiriki. Lakini kama barabara zetu hatutoweka mitaro basi wananchi hata yale majengo yao huwa yanaathirika kwa wingi wa maji yanayokuja kule bila ya kupata kizuizi. Kwa hivyo, tunawaomba washirikiane jambo hili pamoja na wizara hivyo walione au wakandarasi wetu wanavyokua wanafunga mkataba hili liwepo ambalo litasaidia barabara zetu kuhimili kwa muda mrefu na wananchi wetu kutopata usumbufu. Kwa sababu tunajali muda wako natilia mkazo mambo haya nasema ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Asha Bakar Makame: Ahsante sana Mhe. Spika, kwanza nichukue nafasi hii ya kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametuwezesha siku hii ya leo kufika katika hali ya afya njema. Lakini pia nikushukuru wewe kwa kunipatia nafasi hii Mhe. Spika, na mimi nitakua mwizi wa fadhila kama sikuipongeza kamati hii pamoja na mwenyekiti wake kwa taarifa yao mwanana ambayo ni nzuri.

Mhe. Spika, pia nichukue nafasi hii nimpongeze Mhe. Waziri ambaye ameteuliwa hivi karibuni na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Nimpongeze lakini nimpe na pole kwa mujibu wa wizara hii ilivyo nyeti na ilivyo na uhasama na watu. Lakini kwa ninavyomjua Mhe. Waziri kwa imani yangu imefika pahala pake wizara hii kwa kupewa waziri huyu. Mhe. Spika, jambo kubwa nitaomba watendaji tumpe mashirikiano ya hali ya juu Mhe. Waziri ili kuhakikisha tunawapa matumaini wananchi wetu, kusema kweli Mhe. Spika, wananchi katika wizara hii wametokwa na matumaini. Kwa hivyo, ni imani yangu kwamba watendaji wa wizara hii pamoja na Wizara ya Mawasiliano niwaombe wampe mashirikiano Mhe. Waziri ili kuwapa matumaini wananchi wetu.

Mhe. Spika, pia niiombe wizara hii ifanye utafiti ni ardhi gani na gani ambayo kwa kweli wananchi wamedhulumiwa ardhi zao. Kwa hivyo, nawaomba sana wizara hii wawape matumaini wananchi wetu kuhakikisha wale wote ambao wamedhulumiwa kwa namna moja au nyengine katika ardhi basi warejeshewe ardhi zao kwa mujibu wa taratibu na sheria ambazo zimewekwa. Mhe. Spika, sasa nije katika maji hapa ripoti imeeleza lakini nangojea katika bajeti suala la maji ni suala nyeti, sijui kwa nini hatufanyi utafiti wa kina wakati tunapochimba visima au katika vile visima vyetu vikubwa ambavyo vinasukuma maji kuna mijini na vijijini. Mhe. Spika, ni kila wakati mara *transformer* imeharibika, mabomba yamepasuka, hebu tujaribu kufanya ni kitu gani ambacho kinasababisha yote haya ili wananchi waweze kupata maji salama.

Mhe. Spika, pia nije katika Mahakama ya Ardhi ukiangalia ripoti hii imeeleza wazi kwamba Mahakama ya Ardhi kwa kweli ina ufinyu wa bajeti. Sasa kama ina ufinyu wa bajeti haiwezi kununua karatasi, haiwezi kulipia pesa za umeme, mimi nashangaa sijui tunakwenda wapi na ndio maana ukaona kesi nyingi zinashindikana. Mhe. Spika, Mahakama ya Ardhi haina ofisi hivyo ninaiomba sana wizara hebu sasa hivi tujaribu kuiweka vizuri Mahakama hii. Mhe. Spika, lakini sishangai kwa sababu ripoti imesema kwamba haina wataalamu, kila sehemu wataalamu wake ni kidogo. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri sasa hivi ajikaze atafute wataalamu asomeshe, tena namuomba sana akifika ofisini kwake aangalie ni idara ipi na ipi haina wataalamu wa kutosha.

Mhe. Spika, sishangai kwa sababu haina wataalamu ndio maana ardhi ikawa haina mwenyewe kila mmoja amehusika na ardhi, Mkuu wa Mkoa, Mkuu wa Wilaya, Diwani, Sheha wote hawa wao ni kwa sababu idara hii haina wataalamu wa kutosha. Kwa hivyo, naomba wale wanaohusika kwa kweli na ardhi wawe macho, na wale ambao hawasuki na ardhi basi tuwaachie wenyewe wanaohusika. Mhe. Spika, ndio maana nikasema hapa kwamba watendaji tuwache kumanga manga sasa tumsaidie Mhe. Waziri kuhakikisha kwamba ardhi inatumika ipasavyo.

Mhe. Spika, nije moja kwa moja kwenye Zimamoto bandarini, hiki ni kitu muhimu sana hivyo naiomba sana serikali ichukue jitihada ya hali ya juu kuwa na Zimamoto bandarini. Mhe. Spika, tunayaona matokeo mbali mbali ambayo yanatokea mwisho wake tunaanza kulalamika. Kwa hivyo, naiomba serikali sisemi iko mbioni ata maana yake itakua haishi mbio, naiomba serikali ikae itafakari ili kuhakikisha kwamba bandarini kunakua na Zimamoto ya uhakika kwa bandarini tu.

Mhe. Spika, vile vile niiombe sana serikali najua kwamba sasa hivi serikali changamoto yake iko katika usafiri kwa kutoka Unguja kwenda Pemba. Naiomba sana serikali Mhe. Spika, ihakikishe ili tuwapatie usafiri wananchi wetu wa kutoka Unguja kwenda Pemba na kutoka Pemba kuja Unguja, tunayaona matatizo mbali mbali Mhe. Spika, najua kwamba serikali iko katika mchakato huo lakini naiomba iharakishe.

Mhe. Spika, jambo la mwisho niseme tu kwamba nimtakie kila la kheri Mhe. Waziri wa Ardhi ili aweze kushirikiana na watendaji wake kuiweka sawa wizara hii, maana hii wizara kwa kweli mimi naweza kusema

haina mwenyewe. Kwa hivyo, ni matumaini yangu waziri aliyewekwa itapata mwenyewe. Mhe. Spika, baada ya kusema hayo na mimi nashirikiana na wenzangu naunga mkono ripoti hii, ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Michango ya wajumbe wangu wawaone Mhe. Hassan Hamad Omar na Mhe. Asha Bakar Makame itasaidia sana na wengine kufuata mtindo huu tukamaliza haraka. Ninawachangiaji pamoja na huyu anayekuja sasa hivi 24 sasa inakua ni kazi kubwa kweli kweli. Kwa hivyo, tujitahidi ili tupunguze muda wengine wameomba dakika tano tano, nawashukuru lakini muda kwa kweli ni mfupi mno na mwengine huwa anatetereka kwa utaratibu usiokua sahihi.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Nakushukuru sana Mhe. Spika, kunipa na mimi fursa nichangie ripoti hii ya Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi ya Baraza la Wawakilishi. Mhe. Spika, mimi nina mengi lakini nitayapunguza nitachangia kwa uchache ili na wenzangu wapate muda.

Mhe. Spika, kwanza mimi nataka nianze hii Wizara ya Ardhi na nataka nianzie hapo walipopaacha wenzangu. Mhe. Spika, kwa kweli Mahakama ya Ardhi ina changamoto nyingi sana, kwa hiyo namuomba Mhe. Waziri aone kama Mahakama ya Ardhi kwanza kwa sasa hivi hakuna asiyejua kama ardhi ndio tegemeo la watu wote katika ulimwengu. Kwa maana hiyo aone kama Mahakama ya Ardhi ina changamoto ya matatizo ya kesi za kila leo. Na Mahakama ya Ardhi kwa kweli ina upungufu wa Mahakimu, Hakimu aliyepo kwa Unguja ni mmoja. Kwa hivyo, nakumbuka kama tuliahidiwa kua kila Mkoa kutakua na Mahakama ya Ardhi na kutakua na Hakimu wake ili kupunguza hili tatizo la kesi.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri aone kama sasa wakati umefika kwa wale Mahakimu walioahidiwa basi afanye kila inavyowezekana aombe kwa serikali kila kinachowezekana ili Mahakimu hawa wapatikane na waanze kufanya kazi zao. Mhe. Spika, kwa sababu bila hivyo basi huyo Mwenyekiti wa Mahakama ya Ardhi aliyepo hapa Unguja anakwenda mpaka yeye mwenyewe anasema anafika hadi hajui aanze wapi wala amalizie wapi. Kwa hivyo, naomba hili alione Mhe. Waziri ili aweze kulifanyia kazi.

Mhe. Spika, kwa haraka haraka nikitoka hapo niende kwenye ukurasa 212 kwenye nyumba na makaazi. Kwenye hotuba yetu Mhe. Mwenyekiti amezungumza kuhusu suala la nyumba zilioko Kengeja na hapa Unguja nyumba za vijiji zilioko Mpapa. Mhe. Spika, hizi nyumba za Kengeja kwa kweli ziko katika hali mbaya sana ambayo inatishia maisha, na wakati wowote ule kunaweza kutokea hatari. Zile nyumba zilijengwa kwa fedha za walipa kodi yaani serikali, kwa hivyo zinaweza kutoweka na kupata hasara kubwa.

Lakini sasa kuna na hizi nyumba ambazo zinataka kumaliziwa, sasa zile fedha zilizotengwa kwa ajili ya kumalizia majengo haya ndizo zinazotakiwa zichukuliwe kwa ajili ya kumalizia majengo hayo. Tunaiomba serikali na hapa ione kuwa kufanya kitu chochote kile usikimalizie ni sawa na kuwa hujafanya, kwa maana hiyo majengo yale ambayo yanataka kumalizwa ili wananchi wakae kama fedha zake zichukuliwe, tena zikatengenezwe, tena kule itakuwa sawa sawa za kule zitaporomoka na hizi huku zitaporomoka. Kwa hivyo na hili nalo naona lifikiriwe na wizara ione kuwa kuna haja ya kufanya kila njia kupatikana pesa za matengenezo ya nyumba za Kengeja, lakini na hizi za kumalizia ziachiwe zimalizwe.

Mhe. Spika, suala jengine nitalozungumzia ni suala la nishati, ukurasa wa 215 kwenye kitabu hiki cha ripoti. Mhe. Spika, sote ni mashahidi kwamba hivi karibuni tulikuwa na tatizo la mafuta, tatizo ambalo ni sugu na limesababisha mpaka baadhi ya vyombo vya wananchi pamoja na sisi wenyewe baadhi ya wawakilishi humu vyombo vyao vimeharibika kwa kupata mafuta yenye maji. Sasa Mhe. Spika, suala hili nalo linataka kuangaliwa kwa kina, suala la nishati tuna chombo ambacho kuwa ni Wizara ya Kilimo, Makaazi, Maji na Nishati.

Lakini sasa tatizo ninaloliona mimi ni kwamba, sheria zetu zina upungufu, tunatunga sheria lakini sheria zetu zinakuwa zinaingiliana, kuna wizara zinakuwa zinabeba kazi za watu. Kwa hivyo, mamlaka ambayo kuwa tuna Idara ya Nishati lakini kazi zake zinafanywa *ZRB*, hiyo ndiyo inayopanga bei za mafuta, ndiyo inayosimamia mambo hayo ya mafuta ambapo mafuta ni nishati, sasa hichi chombo chetu cha nishati kazi yake ni ipi, ambacho kuwa tuna Idara.

Kwa hivyo, naona hapa kuna utata wa kisheria na namuomba Mhe. Waziri na hili alione, kama nishati isimamiwe na Idara ya nishati, *ZRB* kazi yake ni kukusanya kodi za mapato ya nchi yetu, hivyo wabaki na kazi yao ya kukusanya mapato lakini sio wapange bei wao, wapewe mamlaka ya kuwa wao ndio wapange bei za mafuta na mambo mengine. Na tatizo kama hili lipo kwenye Mamlaka ya Mawasiliano, kwa sababu nako kuna mambo ya leseni na wakati kuna Idara ya leseni, lakini leseni zinatolewa *ZRB*. Kwa hivyo, tuone kwamba kuna upungufu wa sheria zetu zinapandana, hivyo kila pale penye upungufu wa sheria basi tuziweke sawa sio kwamba kila idara ichukue mamlaka ya mwenzake. Mhe. Spika, naona hili nalo linataka kushughulikiwa.

Haraka haraka Mhe. Spika, naomba sasa niende kwenye Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano. Mhe. Spika, naomba nizungumze kuhusu suala la Shirika la Anga. Mwenzangu amezungumza kuwa kuna haja ya kuona kile Kiwanja cha Ndege cha Pemba sasa hivi kinafanyiwa kazi. Sasa hivi Mhe. Spika, tunaingia kwenye mvua za masika inaweza ikaruka ndege kukawa kuna mvua kubwa sana, kwa sababu kiwanja cha ndege hakina taa ikashindwa ndege kutua. Kwa hivyo hili tuliona kama ni muhimu kwa sababu suala hili ni la muda mrefu kila siku tunaambiwa patatengenezwa lakini imekuwa kama yule mtoto wa kuku anavyoambiwa na mama yake utanyonya kesho na kila kukicha maziwa hapati. Kwa hivyo, naomba hili suala lichukuliwe hatua hata kama ni kwa dharura, hata kama kuna taa za dharura basi zichukuliwe zifanywe hasa kipindi hiki tunachoingia.

Mhe. Spika, kwa haraka niende katika Shirika la Meli. Mhe. Spika, kama tunavyozungumza sasa hivi ni mabadiliko ya upepo wa kusi na kaskazi, sasa tunaingia kwenye upepo wa kusi. Bahari yetu sote ni mashahidi kwamba upepo wa kusi unakuwa na nguvu zaidi kuliko wakati wa kaskazi kwa sababu kusi anakuwa na nguvu na dharuba zaidi.

Kuna suala hili la upatikanaji wa meli Mhe. Spika, sisi Waunguja na Pemba ni visiwa, na kila siku tunazungumza kwamba kuna haja ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuwa na meli zake, sasa hivi serikali haina meli, mimi nasema haina kwa sababu Meli ya Maendeleo kila siku inakwenda kwenye chelezo kutengenezwa, kwa maana hiyo ni sawasawa na kuwa hatuna. Kwa hivyo, jamani kama kuna kampuni zinazoonesha dalili za kuwa tupate meli, basi na tuzisimamie tupate meli, kipindi kama hichi tunachoingia cha Kusi na Wapemba meli wanayoitegemea ni Serengeti, nayo hivi sasa mtu anaingia kwa sababu hakuna meli nyengine tu, lakini kama kungekuwa na meli nyengine basi watu wasingeipanda.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, naiomba Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano ione kama kuna haja ya kusimamia kwa kina kabisa suala hili ili upatikanaji wa meli ipatikane kwa ajili ya kuwasaidia wananchi wetu, tusije tukafika tena hali tukaja tukaoneshana vidole. Mhe. Spika, hali ni mbaya sana Wapemba na Waunguja hawana meli ya kusafiria ya uhakika ya kwenda Pemba na Unguja, kwa hivyo hili suala lionekane kuwa ni changamoto ya serikali hii na ione kuwa kuna haja ya kupatikana kwa meli ambayo itakuwa ya uhakika hasa ukizingatia kwamba kusafiri ni lazima. Kwa sababu huwezi kwenda Pemba kama huna usafiri wa aina yoyote ile, hivyo hili ni lazima Mheshimiwa naiomba serikali ione kama hii ni changamoto na ifanyiwe kazi kwa haraka haraka.

Mhe. Spika, naona ushakuwa unatizama saa naomba kuunga mkono hoja hii.

Mhe. Farida Amour Mohammed: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi na mimi ya kuchangia machache katika ripoti hii. Pia nimshukuru Mwenyekiti wa Kamati hii pamoja ya wajumbe wake kwa kufanya kazi ngumu na nzito ya ufuatiliaji katika taasisi zote.

Mhe. Spika, mimi naomba moja kwa moja niingie katika suala la Shirika la Umeme. Shirika la Umeme bado kuna matatizo ya watendaji wake, baadhi ya watendaji wa shirika hili hawafanyi majukumu yao ipasavyo kwa ajili ya kuwatendea haki wananchi wao kwa kuwapatia umeme wa uhakika ndani ya vijiji au miji. Pamoja na kuwa umeme unakuwa si wa uhakika, pengine haupatikani kutokana na matatizo huko kwenye taasisi zao, lakini pia wale watendaji kama kuna mtu anataka kuunga umeme baada ya kulipia vifaa na kupita katika taasisi zote pamoja na sheria zote, inachukua muda mrefu sana kupatiwa umeme ule.

Sasa naomba wahusika wa wizara hii wajitahidi kadiri iwezekanavyo kulifuatilia suala hili, kwani wananchi wetu wengi wanalilalamikia suala hili ambalo Mhe. Rais mwenyewe katika maagizo yake alilitilia uzito na akalipa kipaumbele kwa kuwapatia wananchi umeme wa uhakika. Kwa hivyo, naomba sana wahusika walifuatilie suala hili ili kuwapatia wananchi wetu umeme kwa kufanyia shughuli zao.

Moja kwa moja niende kwenye Idara ya leseni. Mhe. Spika, katika idara hii kuna uchakavu wa vyombo muhimu kwa ajili ya kuendeleza karakana zetu. Karakana hizi zinaonekana ni moja kati ya vitu vinavyotuingizia fedha katika taasisi zetu au katika wizara yetu. Lakini kwa bahati mbaya pesa hizo ambazo zingeingia katika karakana za serikali zikaingia kwenye mfuko wetu, basi zinaingia katika karakana za watu binafsi kwa sababu ya kukosa vifaa muhimu ndani ya karakana hizo. Kwa hivyo, naomba sana Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake walishughulikie sana suala hili la karakana zetu, moja iliyoko Pemba na moja Unguja kuweka sawa ili hizi pesa zinazokwenda katika taasisi binafsi zije kwetu.

Pia ningependa kuuliza swali kama ikiwezekana nijibiwe au lifanyiwe utaratibu wowote. Je, ni kiasi gani cha fedha ambazo zingeingia katika karakana zetu kwa mwaka.

Jengine nije kwenye Idara ya Ujenzi na Utunzaji wa Barabara. Mhe. Spika, kwanza niipongeze serikali kwa kuamua kwa makusudi kutujengea barabara zetu Pemba na Unguja, lakini kuna changamoto nyingi zilizojitokeza ambazo hata wenzetu katika kamati wameziona, ni baadhi ya wale watu wanaovunjiwa au kuharibiwa vitu vyao baada ya ujenzi wa barabara zile, inachukua muda mrefu sana kumaliziwa yale madeni yao jambo ambalo linawapa wananchi wetu kulalamika, na kuilalamikia serikali inakuwa si jambo zuri. Kwa hivyo ninaiomba Idara husika washughulikie suala hili walione na watilie maanani, kwani wale walioharibiwa vitu vyao au nyumba zao kwa ajili ya barabara kweli barabara ni muhimu, lakini pia na wao wanataka pahala pazuri pa kujistiri. Kwa hivyo, naomba sana suala hili lifuatiliwe kwa umakini ili wenzetu hawa waliovunjiwa nyumba zao wapatiwe malipo yao mara moja.

Nikiendelea hapa hapa kwenye hizi barabara kuna tatizo gani linalosababisha hizi barabara kuchelewa kukamilika, kuna barabara zinajengwa kwa muda mrefu hazimaliziki hasa katika kipindi hichi cha mvua. Kwa mfano, kuna barabara za Wete/Gando zimefanyiwa kazi muda mrefu lakini wakandarasi wanaojenga barabara ile wanaonesha hawana umakini wa kuziendeleza na kumaliza kwa muda unaotakiwa. Kwa hivyo, naomba Mhe. Waziri husika alifuatilie suala hili kwa zile barabara ambazo zinachukua muda mrefu, ikionekana pengine huyu mkandarasi kutokana na mikataba mliyowekeana umepita muda basi pachukuliwe hatua zinazofaa.

Mhe. Spika, naomba nije kwenye Mamlaka ya Usafiri Baharini. Kamati katika matembezi yake ilijuilishwa kwamba taasisi hii ni changa iliyoanzishwa muda mfupi tu uliopita. Lakini juu ya uchanga wake ina majukumu ya kusimamia mambo mengi tena muhimu, pamoja na mambo hayo muhimu yaliyoko sasa, Idara hii inakabiliwa na ukosefu wa wataalamu. Sasa naiomba wizara husika wataalamu hawa kwa sababu hii taasisi inatakiwa kushughulikia mambo mazito, ikiwemo kusimamia shughuli za usajili wa meli, ukaguzi, utoaji leseni wa vyombo vidogo vidogo, ukaguzi wa meli za ndani na za nje, sasa hapa lazima wataalamu wapatikane.

Nyuma palikuwa na wataalamu watatu, lakini badala ya tatizo kubwa lililojitokeza la MV. Spice Islander, baadhi ya wataalamu wake wameondoshwa kutokana na matatizo, sasa hivi kuna mtaalamu mmoja tu. Sasa katika idara muhimu kama hii inayofanya mambo makubwa na mazito kuwa na mtaalamu mmoja ni tatizo. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kadiri ya uwezo wake pamoja na watendaji wake walifuatilie hili na kutafuta wataalamu angalau waonekane wakidhi haja ya suala hili.

Pamoja na kusema hayo Mhe. Spika, sitaki kuchukua muda wako mwingi naomba kuunga mkono ripoti hii kwa asilimia mia moja.Ahsante sana.

Mhe. Bikame Yussuf Hamad: Ahsante sana Mhe. Spika, nakushukuru na mimi kunipa fursa hii nikachangia ripoti hii ya Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi. Kwanza Mhe. Spika, naomba nimpongeze sana Mhe. Mwenyekiti wa Kamati hii ya Mawasiliano kwa ripoti yao waliyoiwasilisha hapa Barazani ikiwa ndio mwangaza na mwelekeo wa ufanisi wa serikali kwa ujumla.

Mhe. Spika, ningeiomba sana serikali ripoti hizi zinazoletwa za kamati saba, basi wazizingatie sana kwa sababu ni ripoti muhimu na ambazo zitaongoza mwelekeo mzima wa serikali katika kipindi cha bajeti kijacho, na kuelekeza masuala mazima ya kuleta ufanisi kwa mipango ya serikali, *MKUZA* na *Bangokitita*.

Mhe. Spika, mimi nataka niende katika Idara ya Ardhi na Usajili katika suala zima la *Master Plan* hasa katika vijiji. Mhe. Spika, ni kweli katika vijiji vyetu vingi hasa huko katika maeneo ya mashamba, basi ujenzi wa *master plan* hauzingatiwi kwa kiasi fulani, ni baada tu ya kupewa kibali cha ujenzi kujenga vile anavyotaka yeye, na hii hupelekea usumbufu kuwa kutatokea mgonjwa katika kijiji Fulani, basi labda achukuliwe kwa kitanda kwa ajili ya kuwa hata gari haiingii. Kwa hivyo, naiomba serikali ilishughulikie sana suala hili la ujenzi holela.

Jengine Mhe. Spika, nataka niende katika Idara ya Usajili katika eneo la mashamba ya serikali yanayovamiwa na wananchi, hasa ukitilia maanani suala zima la eka. Mhe. Spika, suala la eka limekuwa ni suala ambalo halifuatiliwi sana, kwa sababu baada ya watu kupewa eka hizi, kuna eka nyengine zilikuwa ni eka za minazi na mashamba mengine ni ya mikarafuu. Lakini imefika hatima kwa vile karafuu haikuwa na thamani, basi eka zile za mikarafuu zimefika pahala kuwa jangwa sasa hivi. Kwa hivyo, mimi ningeiomba serikali kupitia eka zile zilizopandwa mikarafuu, wazingatie sana maeneo yale na kuzitafuta ili wale wananchi walionazo basi wawahamasishe katika kuipandikiza tena mikarafuu ile iliyomo mule kwa ajili ya maslahi yao wenyewe binafsi, lakini na maslahi ya serikali kwa jumla.

Mhe. Spika, niende katika suala la Mahakama ya Ardhi, ingawa lishazungumzwa lakini na mimi nataka nilitilie mkazo.Katika Mahakama ya Ardhi kuna changamoto nyingi ambazo zimeikabili mahakama hii, ukizingatia

kwamba Mahkama ndio chombo muhimu au ndio muhimili mkuu wa serikali, lakini changamoto zilizomo katika mahakama hii ni nyingi na moja ni ufinyu wa bajeti na ufinyu huu uko kila wizara. Lakini sasa Mhe. Spika, kuna taasisi nyengine zinataka zizingatiwe, kama suala zima la mahakama ambalo kuwa katika changamoto zao wanasema hata karatasi ya kuendeshea kesi inashindikana, na hii ni Mahakama ya Ardhi ambayo watu wengi wanaitegemea, sasa sijui shughuli hizi zitafanywaje.

Katika ripoti ya kamati wamesema kuwa kuna tamko la waziri alilolitoa kwamba zitafunguliwa mahakama nyengine tatu, ili kuweza kusaidia kutatua matatizo yaliopo hivi sasa, lakini hizi zilizopo, matatizo yaliyopo ni mengi je, zikifunguliwa nyengine tatu yatakuwa hali gani, si tutazidi kujitia matatizo? Kwa hivyo, naiomba sana serikali wazingatie mambo ambayo yatakuwa na mwelekeo katika serikali.

Halafu nije katika Idara ya leseni. Kamati walitoa ushauri kuhusu gari zinazobeba wanafunzi kuwa gari hizo zinabeba wanafunzi kupita kiwango, lakini mimi nataka niseme kuwa si wanafunzi tu hata hizi gari za abiria nyengine hususan kule Pemba, basi hubeba abiria kupita kiwango kinachoruhusiwa kuchukua, na ile inapelekea usumbufu mkubwa kwa wananchi lakini hata inapotokea ajali. Kwa sababu hao abiria wanaozidishwa si kwa sababu angalau wataingia mle ndani ya gari wachuchumae, abiria wale huwa wanalewalewa kwenye kibao karibu watu 10 au zaidi. Sasa kwa hili namuomba Mhe. Waziri nalo pia serikali izingatie si matatizo ya wanafunzi tu kubebwa pasi na mpangilio, lakini hata sisi abiria tunaoingia katika gari hizo hupata usumbufu mkubwa.

Lakini nataka niseme Mhe. Spika, katika changamoto nyingi zinazoelezwa katika ripoti huwa kuna ukosefu wa wataalamu, kitu ambacho bila ya mtaalamu hamuwezi kufanikisha suala lolote. Kwa hivyo, naiomba serikali izingatie sana suala zima la wataalamu.

Halafu Mhe. Spika, kuna suala zima la ujenzi wa barabara, kuna wakandarasi ambao washazungumzwa. Lakini mimi ningemuomba Mhe. Waziri achukue mfano wa Mhe. Waziri anayeshughulikia ujenzi wa Jamhuri ya Muungano kipindi kilichotokea mafuriko Dar es Salaam, alikwenda akawazuia wakandarasi wasiende kwenye sherehe zao za *Christmas* na warudi kwenye *site* ile kutengeneza barabara na jioni zipitike, na wafanyakazi wale hawakwenda popote walirudi wakenda kushughulikia barabara zile. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri na yeye anapowaona wakandarasi hawafanyi kazi nzuri, basi aweze kuamua la kuamua maamuzi magumu aamue. Kwa hayo machache Mhe. Spika, naunga mkono ripoti hii ya kamati ahsante sana.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe nafikiri muda ulivyo tutashindwa hata kumaliza ripoti hii, na leo tulipaswa kumaliza ripoti tatu. Sasa michango tuendelee mpaka saa sita baada ya hapo tuwaite Waheshimiwa Mawaziri wanaohusika na wizara chini ya kamati hii, na hatimaye tumuombe mtoa hoja aje afanye majumuisho. Kwa hivyo, Mhe. Ali Abdalla kwa bahati mbaya hayupo, Mhe. Fatma Mbarouk Said na baadae kama muda upo Mhe. Salim Abdalla Hamad.

Mhe. Fatma Mbarouk Said: Ahsante Mhe. Spika, kwa kupata fursa hii sasa hivi na mimi kuchangia ripoti hii. Kwanza sina budi kumshukuru Mwenyekiti wa Kamati ingawaje aliingia mitini juzi lakini leo kawasilisha vizuri nashukuru kwa hilo.

Mhe. Spika, niende katika Idara ya Nyumba na Maendeleo ya Makaazi. Kwa kweli idara hii ni kwamba ina nyumba ambazo imezikodisha, lakini mpaka hivi sasa kodi zake bado hazijajitosheleza kulingana na wakati wa sasa. Kwa hivyo, ningeomba kwamba idara hii sasa ibadilishe zile kodi zake ili kuiletea serikali mapato zaidi.

Vile vile limejitokeza jambo ingawa kwenye hii ripoti sijaliona, kwa sababu hili *kabrasha* ni kubwa na tunalipitia haraka haraka, lakini kuna nyumba ambazo zina kumbukumbu zimejengwa juzi lakini ukipita utaambiwa nyumba hizi waliopewa wamepewa kwa idhini ya Mhe. Karume Muasisi wa nchi hii. Kwa hivyo, mpaka leo nyumba zile utakwenda kwenye *block No. 9* lakini utakuta kwamba watu wale wamepewa nyumba zile na Marehemu Karume, lakini huyo Karume mwenyewe tumemuacha tangu mwaka 1972 hatunaye. Kwa hivyo hizi ni changamoto ambazo pia tunazikuta katika Idara hii ya Makaazi.

Tukienda kwenye Mamlaka ya Mji Mkongwe, huu ni mji ambao ni *very heritage site* ya ulimwengu. Kwa hivyo, ni lazima uhifadhiwe na twende na *standard* ile ya kimataifa, na tuheshimu kwamba huu ni mji ambao uko katika uhifadhi wa kimataifa.

Nikiendelea nije kwenye Mamlaka ya Maji. Kwa kweli mamlaka hii kama walivyosema wenzangu kuwa, mamlaka hii ya maji ni muhimu na wala haiwezekani kuekewa siku au kiwango maalum kwamba siku upate na siku usipate. Wananchi wetu wanahangaika na sisi wenyewe kwa ujumla, tatizo lipo na mimi nathubutu kusema

katika Baraza lako hili tukufu kwamba, wale wafunguaji wa maji waliowekwa katika maeneo mbali mbali nitasema ni *wanyambi* na ni *wanyambi* sana. Kwa sababu siku moja tulichukua juhudi mimi na majirani zangu wawakilishi akiwemo Mhe. Ali Salum na Mhe. Salmin Awadh tulikwenda, na tukawaambia tunataka *physical* tuone namna gani maji yanafunguliwa, lakini walitufanya kama watoto wadogo wakasimama na funguo zao mpaka tulipoondoka pale wakafungua vile walivyoona wao inafaa.

Ni kweli kwamba maji yapo, na haiwezekani kwamba ukichimba katika ardhi kwenye kisiwa chetu hiki unapata maji, lakini ikawa maji bado ni tatizo kubwa kwa nchi hii na nimuombe Mhe. Waziri aliyeko sasa hivi alichukulie uzito suala hilo, na kuwafanyia utafiti mpaka wale wafunguaji wa maji awatizame wana tatizo gani. Hili ni tatizo kubwa na hawa nasema hawawajibiki ipasavyo. Kwa hivyo tatizo la maji kila siku juu ya miradi mingi ambayo imeanzishwa, pesa nyingi zimeteketea lakini bado tatizo la maji lipo katika mji wetu huu. Kwa hivyo, niseme kwa hilo Mhe. Spika, lazima Mhe. Waziri afanye kazi ya ziada. Shirika la Umeme. Shirika hili ni shirika ambalo linajiendesha kibiashara. Juzi nilibahatika kusikiliza vyombo vya habari kuna mtendaji mmoja alisema kwamba kwa kweli sasa hivi tatizo la umeme litakuwepo kwa uzalishaji, kwa sababu huko nyuma tulikuwa wakizalisha *Mega Watt* 17, lakini hizo hizo zilikuwa zinauzwa kwa nchi jirani. Lakini sasa hivi tunazalisha *Mega Watt* 800 na zaidi, lakini bado kutokana na maendeleo labda na watu wengi kuwa tunahitaji umeme. Kwa hiyo hili suala linakuwepo lakini vile vile kuna changamoto.

Shirika la Umeme wale watu wao ndio wanaohusika na usambazaji wa nguzo, lakini nguzo watakuwa hawana na vile vile baada ya kuwa hawana, wewe unapotaka kuungiwa umeme unagharamika kutafuta nguzo, lakini baadae wewe unafidiwa na wenzio. Kwa sababu baadhi ya watu wanakaa, huduma ile anaitaka lakini labda pesa hana au vipi, lakini pale inapotokea mtu anakuja kuungiwa kwenye nguzo yangu mimi hata ile taarifa labda ndio wanasema kwamba ni wao. Sasa madhali wanakwenda kibiashara, hizi nguzo sasa hivi kuna matatizo huko majumbani, vile vile wanakuwa hawawatumii wale wafanyakazi wao waliokuwa *registered* wanaunga umeme kiholela.

Mhe. Spika, utakuta nyaya zinaning'inia chini wanataka kutugombanisha na wapiga kura wetu. Kwa sababu mtu kama pana mita 10 ikiwa hukuweka nguzo unahitajia nini, ni kwamba nyaya zinashuka chini watoto wanavuta vuta. Kwa hivyo hili suala ni lazima wawajibike, sekta hizi ni lazima ziendeshwe kitaaluma, ziendeshwe kiushindani kwa sababu hizi sekta ni za kibiashara.

Kwa hayo machache sitaki nichukue muda wako nashukuru na naunga mkono ripoti hii.

Mhe. Spika: Mhe. Salim Abdalla Hamad una dakika sita tu za kuweza kuchangia kufikia saa sita nimwite Waziri.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, nashukuru kwa kupata dakika sita kwa hivyo na mimi nitachangia kwa kutumia dakika ulizonipa. Mhe. Spika, kwanza nitoe shukrani kwa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi kwa kazi kubwa waliyoifanya kupitia Wizara mbili hizi, kuwa makini katika kufanya kazi zao, kuziandika changamoto mle na maoni yao mazito. Nawapongeza kwa hilo.

Lakini kwa ufupi sana nitaomba nipate maelezo. Tukitazama katika hichi kitabu kikubwa ukurasa wa 207 katika changamoto zilizoikabili Idara ya Ardhi na Usajili ni kuwa, katika utekelezaji wa haki inakumbana na tatizo la baadhi ya wananchi kukosa vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi.

Japokuwa hii haimo katika mamlaka ya kamati hii, lakini kwa sababu ya kuwa inaingia katika kupatikana kwa hizi hati mimi ningeliiomba Wizara inayohusika kwa sababu hili tatizo ni gumu, na ukosefu wa vitambulisho hivi unasababisha watu kukosa haki zao katika kila sehemu, kwenye kupiga kura, kwenye hati za usafiri na kadhalika. Kwa sababu sheha ndiye anayesababisha matatizo haya, na kuwa kuna wengine wanapewa si haki yao, kwa hivyo naiomba Wizara ifanye kila inavyowezekana hili suala kuliweka sawa, vyenginevyo litatufikisha pabaya sana.

Mhe. Spika, ukurasa wa 212 kuna Idara ya Nyumba na Maendeleo ya Makaazi, hapa pana utekelezaji na katika utekelezaji hapa ni kuwa hii idara katika mwaka wa fedha 2011/2012 ilipangiwa kukusanya jumla ya shilingi milioni 100, lakini kwa nambari zilizowekwa hapa ilikusanya shilingi 10,912,201 na hii wanasema walivuka lengo kwa asilimia 109.

Kwa hivyo, naomba marekebisho katika hesabu kwa sababu hizi walizokusanya na asilimia ilivyo ilikuwa iwe asilimia 10.9 tu, *to the nearest whole number*. Sasa hii hesabu sio sahihi kuna nambari imepungua au maelezo

siyo, kwa hivyo naomba nipata maelekezo. Kwa maana hiyo, kifungu cha pili kinachosema kuwa walifanikiwa mimi nasema kwa hesabu hizi kuwa ndivyo zilivyo hawakufanikiwa badala yake walirudi nyuma sana.

Mhe. Spika, jengine Mamlaka ya Maji, naipongeza sana kamati kwa shughuli zake kwenye mamlaka hii, na naipongeza Mamlaka ya Maji kwa utekelezaji wa shughuli zake za kueneza maji katika sehemu kadhaa. Isipokuwa katika maoni na maagizo ya kamati kwenye ukurasa wa 213 kifungu cha kwanza ni kuwa Kamati imeshauri mamlaka iwakopeshe wananchi hasa wasiokuwa na uwezo kwa kuwasogezea karibu huduma hii ya maji na watakapofunga huduma hizo tena wawe wanalipa kidogo kidogo.

Hii mimi naunga mkono kwa sababu Wizara ilisema hata umeme itawasaidia kuwakopesha wananchi wale waliokuwa hawana uwezo, lakini wanaonesha nia ya kulipa kuungiwa umeme. Kwa hivyo nachanganyisha, pamoja kuwa naungana na kamati kwa hili na kwa sababu Wizara haijatekeleza ahadi yake sasa hili lichukuliwe kwa sehemu zote mbili.

Lakini katika kifungu cha 5 katika maoni hayo ya maagizo ya kamati ni kuwa, kamati imeipongeza sana idara kwa sababu ya kueneza maji katika sehemu hasa nyingi za mkoa wa mjini magharibi. Wamesahau kuwa kuna wananchi wa vijijini wengi tu mpaka leo hawajapata huduma ya maji, kwa hivyo naomba pia na vijijini kuangaliwe tusiangalie pongezi kwa sehemu za mjini tu na vijijini ndio kwenye watu wengi na wanahitaji hii huduma.

Mhe. Spika, ukurasa wa 215 kuna Idara ya Nishati, nakuja moja kwa moja katika ukusanyaji. Idara kama ingelikusanya fedha kwa *unit* moja shilingi 173 ilitarajiwa ikusanye shilingi bilioni 57 na kuendelea. Lakini kwa sababu ilitumia uungwana kwa kujua hali ya wananchi wakatumia ile *unit* moja shilingi 120 walikusanya chini ya kiwango, na kwa vyovyote kuna hasara ya bilioni 2. Mhe. Spika, mimi nashukuru Wizara kwa kuwaonea huruma wananchi lakini tujue tunapata hasara kubwa sana.

Mhe. Spika, ushauri wangu kwa hili kwa haraka haraka, hakuna sababu kwa nini sasa hivi Wizara haitafuti njia ya kuhakikisha kuwa tunapata umeme wetu wenyewe na umeme huu unaotoka Bara tuchukue kama umeme wa akiba au mbadala. Vyenginevyo si vizuri kuwa kila siku tunakwenda kwa hasara za mabilioni katika kisiwa hichi kidogo.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, niwaombe radhi wachangiaji wamekuwa ni wengi, lakini kuna wachangiaji kama 10 pamoja na huyu ambaye wala hakumaliza kuwaomba radhi sana, kwamba hatukupata muda wa kutosha muda mwengine umekuwa unavurugika kati kati. Kwa hivyo, niwaombe radhi Mhe. Abdalla Juma Abdalla, Mhe. Suleiman Hemed Khamis, Mhe. Hamza Hassan Juma aliomba dakika tano, Mhe. Abdalla Mohammed Ali, Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa, Mhe. Mohammed Mbwana Hamad, Mhe. Ismail Jussa Ladhu aliomba dakika tano baadae tatu namuomba radhi sana, Mhe. Nassor Salim Ali na Mhe. Rufai Said Rufai kwamba wamekosa muda wa kuchangia. Itoshe na tukubali basi hawa waliochangia wamewakilisha wengine.

Naomba sasa nimkaribishe Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati anaanza Naibu Waziri. Tumia dakika chache sana ili Waziri amalizie pale palipobaki.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, kwanza nikushukuru na mimi kwa kunipa nafasi ya kuweza kuzungumza mawili matatu juu ya haya yaliyoelezwa na wachangiaji. Vile vile niwashukuru wachangiaji wote ambao waliochangia ripoti hii naamini kwamba lengo na madhumuni ni kutukumbusha katika shughuli za utendaji ndani ya Wizara yangu. Lakini mimi naomba niyazungumze mambo mawili tu hususan kupitia Shirika la Umeme na nianzie na hili la matatizo yanayojitokeza katika uunganishwaji wa umeme.

Mhe. Spika, ni kweli kuna matatizo ndani ya Shirika la Umeme, aidha wakati wa kuwaunganishia wananchi wake huduma hii ya umeme. Lakini ningeomba kwanza ieleweke kwamba Shirika la Umeme ni taasisi kama taasisi nyengine za serikali, kwa vile kasoro ndogo ndogo haziachi kujitokeza. Hili kwanza naomba lieleweke.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, katika uunganishwaji huu, ni kweli wananchi wengi huwa wanafika katika Shirika la Umeme na kujaza fomu zao kwa ajili ya kuunganishiwa umeme. Lakini vile vile wananchi baada tu ya kwishafika Shirika la Umeme na kulipia huduma hiyo ya kutaka kuunganishiwa, basi wananchi hujisahau kwamba Shirika la Umeme linahitajika na wananchi wote wa Zanzibar. Yule anayefika katika kipindi cha mwisho hupendelea zaidi kwamba yeye aunganishiwe umeme huo kabla ya kuunganishiwa wenzake waliotangulia. Lakini kiutaratibu wa shirika hilo ni kwamba yule aliyekuja mwanzo basi ndie tunayemshughulikia, ikisha inafuatia kwa yule ambaye anayekuja kuomba kuunganishiwa katika kipindi cha

mwisho. Vile vile tunalo tatizo la upungufu wa wafanyakazi pamoja na vitendea kazi. Hilo tumeliona na Wizara yangu kupitia Shirika la Umeme tunajiandaa kufanya utaratibu wa kuwaajiri mafundi ili kuliondoa tatizo hili kwa wananchi wetu.

Mhe. Spika, sitaki nichukue muda mrefu kwa vile Mhe. Waziri atakuwa na nafasi kubwa zaidi ya kuyazungumza haya, naomba nizungumzie suala la pili kuhusu kupanda au kuwepo kwa bili ambazo hazina mpangilio kama linavyozungumzwa.

Mhe. Spika, ni kweli mara nyengine hujitokeza tatizo kama hilo kwamba huwa tunawapelekea wateja wetu bili ambazo pengine zimepanda kiwango. Lakini vile vile tunawaomba wananchi na wao wawe waangalifu sana kwa sababu kwanza tuna utaratibu wa kuwauzia wananchi huduma hii ya umeme, aidha kutoka *unit* moja hadi *unit* 50 na kutoka *unit* 51 hadi *unit* 100 na vile vile kutoka *unit* 150 mpaka kuendelea hivi ni vitu ambavyo vina bei tofauti. Hili naomba lizingatiwe, na wananchi wengi naamini kwamba hili bado hawajalifahamu. Kutoka *unit* moja hadi *unit* 50 tunauza kwa kila *unit* moja shilingi 50. Lakini kutoka *unit* 51 mpaka *unit* 100 tunauza *unit* bei ya shilingi 120, na kutoka *unit* 150 na kuendelea au tutasema watumizi wa viwanda vile vile kuna bei ambayo inatofautiana kabisa na bei hiyo.

Sasa ningeomba wananchi walielewe hili.Wateja mara nyingi hutumia umeme, kwa vile mteja kasikia kwamba tunauza *unit* shilingi 50 anaweza akatumia *unit* 200 akakivuka kiwango cha *unit* 50 aelewe kwamba anapofikia *unit* 60 tu basi ile bei ya shilingi 50 tayari inakuwa imeshabadilika. Vile vile tumeligundua tatizo jengine kwamba katika nyumba wanazotumia wateja wetu, basi nyingi sana zina matatizo ya *wiring*, hususan kwamba wanatumia umeme lakini katika *fitting* wanazozitumia hujitokeza kushikana kati ya nyaya za moto na waya wa *earthing*, kitu ambacho kwa kweli kinasababisha mzunguko mkubwa sana wa mita. Inawezekana pengine hujatumia kifaa chochote cha umeme kwa muda ule, lakini mita ikawa ina *reading* kama kawaida kama unatumia vifaa vyenginevyo.

Sasa tatizo hili huwa linatusababisha kwa kweli kupata matatizo makubwa, kwa sababu kama itakuwa mita inakwenda katika misingi kama hiyo, basi mteja lazima atalalamika yeye anachoamini kwamba mimi nimetumia taa tano, lakini kiwango kilichoshuka cha bili ni kikubwa zaidi, lakini pengine katika *wiring* zake zina matatizo kama haya. Kwa sababu waya wa moto unaposhikana na waya wa *earthing* ina maana tayari mzunguko wa mita unapatikana na umeme unapotea. Tofauti na waya ya moto unaposhikana na waya ya *neutral* kwa sababu unaposhikana na waya ya *neutral* ina maana hiyo ni *short* tayari ni kwamba litatokea tatizo. Lakini je, unaposhikana na waya ya *earthing*, umeme utapotea na mita itazunguka na tayari *reading* unayoitumia ya kawaida wakati hapana matatizo itakuwa imebadilika kwa hapo.

Sasa hili nalo ningewaomba wenzetu waliangalie sana, ili tuliondoe tatizo hili kwa pamoja. Ni kweli matatizo ya utoaji wa bili huwa yanajitokeza, lakini hili tutalifanyia marekebisho tutakaa na shirika letu kufanya usahihi na kuhakikisha wateja wanalipa umeme kwa mustakbali wa kile wanachokitumia.

Mhe. Spika, sitaki nitumie muda mrefu kama nilivyoeleza mwanzo kwa vile Mhe. Waziri na yeye anataka aelezee kiurefu zaidi. Mhe. Spika, nakushukuru sana.

Mhe. Spika: Naibu Waziri tunakushukuru. Mhe. Naibu Waziri amekuwa fundi mkubwa amejibu maswali vizuri.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, kwanza namshukuru sana Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi pamoja na kamati yote, kwa kufanya kazi nzuri ya kutengeneza ripoti ambayo kwa kusema kweli itakuwa ni dira yangu ya kuanzia kazi katika kutatua mambo mengi yaliyomo katika ofisi hii.

Mhe. Spika, nataka kusema kwa jumla jumla tu kwa sababu muda wenyewe ndio mfupi, najua na wenzangu nao wanataka kujibu. Kwa hivyo, kwa kuwa sijibu bajeti nitazungumzia yale mambo ambayo ya msingi yameguswa na kuyaelezea nini tutafanya kwenye masuala hayo.

Mhe. Spika, suala la kwanza ambalo limezungumzwa sana, ni suala la kuzingatia *master plan* ya miji yetu. Mhe. Spika, hili ni kweli na kwa kweli tuna wajibu wa kujenga nyumba kwa kutumia *master plan*, na miji yetu ndiyo hasa itakuwa miji ya kisasa. Sasa hili ni suala ambalo kusema kweli tutalifanyia kazi katika wizara, na wananchi wasituone wakali wakati wanapokuwa wanajenga nyumba zao mwengine kaelekeza kusini, mwengine kaelekeza kaskazini, pahala pa kiwanja cha mpira anapatumia, pahala pa skuli anapatumia, haya matatizo yapo yanafanyika na yanaharibu. Hivi sasa tunatayarisha *master plan* mpya kwa ajili ya mji wa Unguja, lakini itakapokuwa tayari nafikiri katika suala hili wizara itakuwa wakali sana katika usimamizi wake.

Mhe. Spika, jengine ni suala la kuandaa yale maeneo ambayo yameshapimwa kwa ajili ya ujenzi, kuweka miundombinu inayohitajika. Hili suala tunalichukua na tutalifanyia kazi. Ni kweli baada ya eneo kupimwa, basi lazima pajulikane pale pahala ambapo hapa ni njia, hapa msikiti, hapa skuli na patengenezwe ile miundombinu, na hata kufikisha nguzo za umeme kabisa kama wenzetu wanavyofanya kule Tanzania Bara. Tunamuomba Mwenyezi Mungu atuwezeshe na hilo tulifanye tufike katika kiwango hicho.

Mhe. Spika, kuna matatizo ya eka kujengwa nyumba, kugeuzwa kuwa ni maeneo ya ujenzi. Nadhani hapa kuna haja ya wananchi kupunguza tamaa, kwa sababu kinachotokezea hivi sasa ni kwamba wananchi ndio wanaouza eka kwa ajili ya watu kujenga nyumba. Kwa kweli madhumuni makubwa ya kupewa eka wananchi ni kwa ajili ya kilimo, lakini sasa watu wanauza ardhi kwa kujenga nyumba. Hili ni suala letu sote viongozi, si suala la wizara peke yake. Najua Mhe. Spika, lipo tatizo la baadhi ya wafanyakazi wetu wa kupima nao vile vile kwenda wakaamua maeneo hayo kuyapima nyumba. Hili tutashirikiana wizarani kule tuache utaratibu huu wa kusema kwamba tunaongeza maeneo ya kuishi na tunapima nyumba. Hili tunataka tulifanyie kazi na tuone kwamba tunalitekeleza katika hali halisi. Lakini haya masuala ya eka wananchi wanawajibika kabisa kuona kwamba eka wanazitumia kwa ajili ya kilimo na wanazilima sio wanavuna.

Maana tatizo liliopo Mhe. Spika, ni kwamba kwenye eka wananchi wetu wanavuna badala ya kuvuna, minazi aliyoikuta tangu siku aliyogaiwa ndiyo hiyo hiyo, na anaivuna ndiyo hiyo hiyo mpaka inakwisha, mikarafuu aliyoikuta ndiyo hiyo hiyo na anaivuna hiyo hiyo mpaka mikarafuu inakwisha. Utalikuta shamba lina mikarafuu pengine 200 au 300 leo ukitembelea lina mikarafuu 16 yote imeshapotea. Lakini nadhani ni vizuri maeneo hayo tukayatumia kwa ajili ya kilimo kama ilivyokusudiwa katika utaratibu wa kugawa ardhi.

Mhe. Spika, kuna suala la matatizo ya uajiri katika Idara ya Nishati. Mhe. Spika, hili tatizo tunakubali kwamba tutaendelea kufanya jitihada, tumepeleka vijana kusoma kwenye masuala ya nishati kwa kushirikiana na wenzetu hawa wa *Ras gas,* ambao hivi sasa tunaendelea nao na mazungumzo ili tuongeze kupeleka wanafunzi zaidi katika kusoma nishati. Kwenye bajeti tutataja hasa tumeshafanikiwa kuwapeleka wangapi na tunatarajia kupeleka wengine wangapi, maana yake tunataka kupeleka wengi kwenye bajeti ya mwaka 2012/2013 kwa ajili ya kusoma masuala haya ya *gas*.

Tunajitahidi kufanya utafiti juu ya hali ya maji katika nchi yetu, lakini nataka Waheshimiwa Wajumbe wakubali kwamba tatizo la maji katika nchi yetu ni kubwa hata huko kwenye hiyo ardhi. Huko chini yalikojificha hayo maji nako kuna matatizo ya upungufu mkubwa wa maji, na yanasababishwa wakati mwengine na uharibifu wa mazingira yetu sisi wenyewe.

Mhe. Spika, Mwanyanya pale palikuwa pana maji mengi, leo ukienda ukitembelea pale ile sehemu ya maji utakuta sehemu kubwa sana sasa hivi haina maji yako chini sana. Hili ni tatizo tunaharibu mazingira, ule msitu wa Kijichi ulikuwa ukiteremsha maji ya kutosha pale katika maeneo yale, lakini msitu ule watu wameuvamia wanaukata, matokeo yake maji yanapungua ardhini. Tunalo tatizo na tusipoangalia tutalazimika kwenda kutafuta maji baharini, na hii ndio itakuwa hatari zaidi. Kwa hivyo, Mhe. Spika, tuna wajibu wa kutunza vianzio vya maji tusiharibu misitu, tusivamie katika maeneo ya misitu ile ambayo ni chanzo cha maji kwa kujenga nyumba. Hilo ni tatizo jengine tunaweza tukalipata katika maeneo mbali mbali ya vianzio vyetu vya maji.

Mhe. Spika, hali ya maji vijijini haijaenea vijiji vyote, lakini hali ya maji inaonekana ni nzuri vijijini hata kuliko mjini. Sasa tatizo linakuja wapi, tumeanzisha miradi mipya ya maji lakini bado haijawafikia wananchi kwa sababu miradi ni mipya, lakini miundombinu ya kufikisha maji nayo ina matatizo katika maeneo ya wananchi. Kwa hivyo, hili nalo tunalishughulikia *inshaallah*.

Mhe. Spika, uhaba wa wataalamu hili ndio tatizo na hata nakumbuka nilipokuwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali nilisema kwamba watu wa mipango wanajaribu kutazama upungufu uko sehemu gani. Ndio maana katika kutoa elimu ya juu wameweka mambo maalum ya kupewa kipaumbele, kwamba watu wasomee hili na hili ili tuweze kupambana na matatizo ya wataalamu katika wizara zetu zote za serikali.

Mhe. Spika, kuna suala la nyumba za Kengeja. Mhe. Spika, hizi nyumba ziko katika hali mbaya sana, na zinahitaji kufanyiwa matengenezo. Lakini hata hivyo, wajumbe wa kamati walipokuja kuzungumza na wizara wakasema hawaungi mkono suala la kuondoa pesa za Bambi kuzipeleka Kengeja kwa ajili ya kufanya matengenezo. Hilo limekubalika katika wizara na hatutazipeleka tena. Mimi ilikuwa kuzipata kwenye bajeti ijayo pesa tuzilipe kule kule Bambi tukamilishe nyumba za Bambi, lakini kwa sababu kamati imeona si wazo zuri, basi tunangojea tuanze bajeti mpya tukatafute pesa kwa ajili ya kupeleka katika nyumba za Kengeja.

Mhe. Spika, katika ugawaji wa nyumba za maendeleo, kweli wapo watu ambao mzee wetu Marehemu Mzee Abeid Amani Karume aliwapa nyumba baadhi ya wazee katika hizi nyumba za kawaida. Sasa ulipokuja kushamiri ujenzi wa nyumba za maendeleo, nyumba zile nyengine zimevunjwa kwa hivyo imelazimika wafidiwe katika hizi nyumba ambazo zimejengwa hivi sasa mpya. Hiyo ni kweli kabisa na hata kuna maeneo mengine mengi. Kulikuwa kuna wale vijana wenye umri wangu nafikiri wanakumbuka zile bendi zilizokuwepo *Zanzibar Jazz*, na wengineo walikuwa na nyumba zao wamekodi pale Mpirani ambazo zimevunjwa, imelazimika wale sasa hivi walipwe katika maeneo ya nyumba hizi mpya ambazo zimejengwa. Kwa hivyo, hili nalo nakubali kwamba limetendeka.

Mhe. Spika, tunakubaliana kwamba tutajitahidi kulifanyia kazi suala la ufungaji na ufunguaji wa maji, kwa sababu unasababisha matatizo katika baadhi ya maeneo. Tutazungumza na maofisa wenzetu hawa tuwe pamoja katika hili tusijenge tamaa ya kumuuzia maji mtu kumpelekea kwake na tukawakosesha wengine wengi. Ni vizuri tuweke utaratibu unaoeleweka katika suala la ufungaji na ufunguaji wa maji katika hali yetu hii tuliyonayo hivi sasa ya uchache wa maji.

Mhe. Spika, tatizo la umeme ni kubwa Naibu ameshalizungumza. Lakini tumshukuru Mwenyezi Mungu Mhe. Spika, huu umeme tunaoutumia sasa hivi tuna *megawatt* 45 tu ambazo inapofika saa 12:00 tunakaribia kuvuka matumizi yetu, maana matumizi ya umeme ni makubwa watu wameendelea wanajua kutumia umeme, na kila mtu anataka umeme katika nyumba yake, na umeme umeenea mpaka mashamba. Waya wetu ule unaweza kuchukua hizo *megawatt* 45 lakini tukifika jioni tunavuka yale matumizi ndio maana tunaweka ule mgao ili kuhifadhi ile kuvuka.

Pamoja na kutumia yale majenereta bado utakuta watu wanavuka zile *megawatt* 45, huu umeme mpya unaotaka kujengwa kupitia *Millenium Challenge* ni *megawatt* 100, tukipata umeme mpya wa *megawatt* 100 na waya wetu huu bado ukaendelea kutumika nafikiri tatizo la umeme litapungua. Najua halitaondoka kabisa kwa sababu bado watu wanatumia umeme kwa matumizi makubwa sana. Mhe. Spika, hapa mimi napenda kutoa wito kwamba, wananchi wanapotumia umeme watumie kwa uangalifu wasiache umeme ukawa unawaka bure, unapotea bure ovyo katika maeneo yale. Hili tatizo lipo, tuna *megawatt* 100 tutazipata nyengine na *megawatt* 45 ndio tunazo hivi sasa Mwenyezi Mungu akipenda tunaweza kuzipata.

Hati za kumiliki ardhi na Uzanzibari. Mhe. Spika, mimi naona bora tungeshauri kuhakikisha kwamba Wazanzibari wote kama ilivyo sheria wanapata vitambulisho vya Mzanzibari katika njia zozote zitakazowezesha kutatua tatizo la Uzanzibari, halafu hapo ndio twende kwenye masuala ya usajili wa ardhi. Kwa sababu kuna matatizo unaweza kumpa mtu ardhi lakini si Mzanzibari, sasa hiyo itakuja kuleta matatizo makubwa zaidi na malalamiko yatakuja kuwa makubwa zaidi.

Mimi nadhani sasa hivi wale wazee wetu ambao wameshakuwa watu wazima hawakuwa na vitambulisho, basi sheria inaruhusu utaratibu gani ufuatwe ili na wale wapate hizo hati za Uzanzibari. Nafikiri tutekeleze hiyo sheria ya kuwapatia hawa wazee wetu watu wazima nao vitambulisho vya Mzanzibari wavipate. Sheria ipo wazi namna gani utafanya mpaka hata huyo mtu mzima apate hicho kitambulisho cha Uzanzibari. Tunaomba masheha wasaidie sana katika suala hili, ili watu wetu wapate vitambulisho vya Mzanzibari wote kabisa na tutumie vitambulisho vya Mzanzibari kwa ajili ya kugawa maendeleo ya wananchi wetu.

Mhe. Spika, masuala yaliyozungumzwa ni mengi naahidi kuyachukua na kuyafanyia kazi kwa sababu ya muda naona nimalizie hapa. Mhe. Spika, nakushukuru.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, awali ya yote na mimi sina budi kukushukuru kwa kunipatia nafasi hii. Lakini pia na mimi nichukue nafasi hii kwa kumpongeza kwa dhati kabisa Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi mwanasheria mwenzangu Mhe. Makame Mshimba Mbarouk. Lakini pia kuchukua nafasi hii kwa kumuomba Mwenyezi Mungu amlaze pahala pema mjumbe mwenzetu wa kamati hii Mhe. Salum Amour Mtondoo. Amin.

Mhe. Spika, maswali mengi yameulizwa kuhusu Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano, na kama tunavyojua kwamba muda umebaki mchache kwa hivyo mimi nitatumia muda mdogo sana katika kutoa ufafanuzi wa baadhi ya hoja zinazohusiana na ripoti hii ya kamati husika.

Mhe. Spika, limezungumziwa suala la *stendi* ya Chake Chake, suala hili tumelitolea ufafanuzi katika kipindi cha maswali na majibu, na tumeeleza kwamba kikwazo kilichoko ni kuweza kuivunja nyumba. Lakini kama sote tunavyotambua kwamba serikali haina utumizi wa mabavu katika kuzichukua mali za wananchi wake, hivyo mategemeo yetu kwamba mwananchi yule ameona umuhimu wa kuongeza *stendi* ile pale katika eneo la Chake

Chake. Kwa msingi huo, nakubaliana kwamba ataona umuhimu wa kushirikiana nasi hasa idara husika ya upimaji, ili kuweza kukubali kulipwa fidia na kupisha utanuzi wa stendi ile ya Chake Chake ili kuweza kutoa huduma kwa wananchi wengi zaidi. Mategemeo yangu kwamba mwananchi huyu atakuwa amesikia kilio cha wananchi na serikali yake kwa ujumla.

Mhe. Spika, limeelezwa pia suala la minara ya simu kwamba haitoi huduma stahiki. Mhe. Spika, suala hili tumelichukua na sisi kama *coordinator ministry*, tutawaita wahusika Kampuni ya Tigo pamoja na watu wa Zantel kuhusiana na dhana nzima iliyojengeka ya kukatwa makato kwa watumiaji wa kampuni hii pasi na kutakwa ridhaa zao.

Mhe. Spika, pia kuna suala la mitaro ya barabarani. Mhe. Spika, kama tunavyokumbuka kwamba barabara zetu zote mpya zinazojengwa hivi sasa suala hili la mitaro linazingatiwa, kwa kuamini kwamba maji ya mvua ndio adui nambari moja wa uharibifu wa miundombinu ya barabara. Tuna mategemeo kwamba tukijenga mitaro itakayoweza kuchukua maji ya mvua ndio adui nambari moja kwa uharibifu wa miundombinu ya barabara. Tuna mategemeo kwamba tukijenga mitaro itakayoweza kuchukua maji ya mvua basi tutaweza kuzinusuru barabara zetu.

Lakini kwa upande wa barabara za mjini, tayari tuna mradi mkubwa chini ya usimamizi wa manispaa Zanzibar itakayoweza kujenga mitaro kwa barabara zetu za mjini na barabara za vijijini zinazojengwa hivi sasa, tayari utaratibu huo tumeshauzingatia na kwa zile barabara ambazo zimejengwa zamani vijijini, suala hili la mitaro ambalo halikuzingatiwa, basi napenda kulihakikishia Baraza lako tukufu kwamba wizara yetu italichukua suala hili na kulifanyia kazi hatua kwa hatua ili kuona barabara zetu hizi tunazinusuru na kuzipa muda mrefu wa maisha ya kuweza kuishi kwa kuweza kuwahudumia wananchi wetu.

Mhe. Spika, pia limeelezwa suala la uimarishaji wa kiwanja chetu cha ndege cha Zanzibar, maeneo ya wasafiri wanaosubiria safari zao. Tunazichukua pongezi hizo na tunahakikishia kwamba pongezi hizo hazitokua pongezi za mgema, kwa kulitia maji tembo. Tunazichukua pongezi hizo kwa kuchukua kwamba ni chachu na changamoto ya kuharakisha hatua zetu za maendeleo katika kiwanja hicho cha ndege.

Lakini pia lilizungumziwa suala la kituo cha zimamoto katika eneo letu la bandarini. Mhe. Spika, Shirika la Bandari pamoja na wizara husika ya Miundombinu na Mawasiliano, tumefanya mawasiliano na wenzetu wa idara husika ya zimamoto na uokozi, tuliwataka tujenge kituo pale wakatupa *request* yao ya kuwapatia eneo la kuweza kujenga kituo pale. Tumeshafanya hivyo, lakini changamoto iliopo ni kwamba eneo tulilowapa wamesema ni dogo na hoja yao ni kwamba wangependelea katika eneo lile la bandari, kua na kituo ambacho kitakua kinafanyakazi masaa 24 kwa kuzingatia miundombinu, mali, ukubwa na umuhimu wa kuwepo kituo kama kile.

Hivyo, basi tunategemea kwamba tutajaribu kuona uwezekano katika eneo letu la bandari ile, kutafuta eneo ambalo litakua linaweza kuakisi, sote tukizingatia kwamba tayari hivi sasa eneo letu la bandari limekua finyu. Lakini katika kipaumbele hiki cha masuala haya ya zimamoto, tutatafuta namna ya kuweza kukidhi kuwapatia eneo litakaloweza kutosheleza.

Mhe. Spika, pia lilizungumziwa suala la kituo cha Kivukoni kilioko Dar es Salaam katika harakati za usalama wa vyombo baharini, kama tunavyotambua kwamba kituo kile kiko kwa ajili ya msaada na kwa ajili ya kusaidia watu takriban wa ukanda mzima wa *East Africa*, ni sawa sawa na kile kituo kilichopo *Djibout* kinachohudumia karibu nusu ya watumizi wa Bahari ya Hindi.

Lakini aidha, mategemeo yetu ni kwamba kifaa chetu cha *GMDSS* kikimaliza kufungwa katika mnara wetu wa *Beit Al Ajaib* basi tunaamini kwamba mahusiano na mawasiliano kati yetu kituo hiki cha Zanzibar na kile cha kule Dar es Salaam yataimarika na hivyo kurahisisha taarifa za upatikanaji wa wasafiri wa baharini pale watakapopatwa na tatizo lolote.

Mhe. Spika, lilizungumzwa pia suala la magari ya abiria pamoja na magari yanayopakia wanafunzi kupakia watu zaidi ya idadi iliyoruhusiwa. Mhe. Spika, napenda nichukue nafasi hii kutoa wito tena kwa vyombo vyetu husika hasa Jeshi la Polisi, kitengo cha usalama barabarani, kuzichukulia hatua kali madereva na wale wanaohusika wanaokiuka sheria, kwa sababu sheria ipo na wajibu wa vikosi hivi ni kuzitekeleza zile sheria ambazo zimetungwa na vyombo hivi halali.

Mhe. Spika, lilizungumziwa suala la kujifukia kwa bandari yetu, hasa kwa upande wa Magharibi Kusini. Ni kweli kwamba taarifa hizo zipo na ni uthibitisho kwamba bandari wakati wa maji yanapojaa, ilikua na urefu wa

mita 14, lakini sasa hivi *tide* yake imeshuka hadi mita 11 mpaka mita 9 kutokana na bandari kujifukia. Tayari wizara na Shirika la Bandari tuliona hilo, tumeshafanya mawasiliano na kampuni husika wanakuja. Lakini tulichokizingatia ni kwamba kwa kutambua jambo hili, bandari ile haijajengwa muda mrefu, ili jambo kama hili lisiweze kujirejea, basi tumewapa muda kwamba kwanza wafanye uchunguzi kugundua sababu na chanzo ya bandari ile kujifukia, baada ya kugundua hilo ndio iendelee na utaratibu wa kuchimba ili kurejesha hadhi bandari yetu.

Mhe. Spika, lilizungumzwa pia suala la uchache wa wataalamu katika mamlaka ya *Zanzibar Maritime Authority*. Ni kweli Mhe. Spika, suala hilo lipo, lakini sisi kama wizara na taasisi husika tumeliona hilo. Kwa kuanzia tayari tumeshapata mtaalamu mmoja.

Lakini suala hili Mhe. Spika, wataalamu tunaowahitaji hapa ni lazima wawe watu ambao wana uzoefu, sio tu wale ambao watakua ni *fresh* kutoka katika vyuo vikuu au sehemu nyengine walizojipatia taaluma. Hivyo, basi ni imani yangu kwamba suala hili tutalichukua na kulifanyia kazi kwa kutambua uzito na umuhimu wa taasisi ile katika usalama wa vyombo vyetu na usalama wa wananchi wetu.

Mhe. Spika, suala jengine lililozungumziwa ni uimarishaji wa karakana yetu. Napenda nitoe wito kwa wamiliki na watumiaji wa vyombo vya serikali kuendelea kukiunga mkono kituo chetu cha karakana kule. Pia ni kweli kwamba karakana yetu ina upungufu wa vifaa na watendaji kazi, kwa maana kwamba mafundi katika mawizara. Tumejipanga na hilo na ikiwezekana hata tutafungua milango ya kuimarisha karakana ile kwa kushirikiana na wabia na wahisani wengine ambao watakua tayari kutusaidia.

Mhe Spika, la mwisho ninaloweza kuchangia ni kuhusiana na suala la *ZRB* kutoa huduma ya utoaji wa leseni. Ni kweli kwamba makubaliano yaliyopo kati ya wizara yetu na kitengo hiki cha *ZRB*, ni kiwamba *ZRB* ni *agent* wetu atakayepokea mapato na utoaji wa leseni. Taratibu zote zilizobakia za kitaalamu zinafanywa chini ya idara yetu husika ya usafiri na leseni na tunaamini kwamba hakuna mtu atakayekwenda *ZRB* kupewa leseni pasi na kupita katika ngazi husika zikiwa ni za kitaalamu, ili kukamilisha kuona kwamba madereva wetu hawa wanakamilisha taratibu kwa mujibu wa sheria ziliopo.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo machache nasema kwamba na mimi naunga mkono hoja hii pamoja na ufafanuzi tulioutoa. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, kwa heshima kubwa na mimi nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia taarifa au ripoti hii ya kamati ya Mawasiliano na Ujenzi ya Baraza lako tukufu.

Kwanza kabisa Mhe. Spika, nataka nimshukuru Mwenyekiti, wa kamati hii Alhaj mtarajiwa, Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, nimshukuru kwa namna ambavyo yeye na wajumbe wake wamekua wakifanya kazi katika wizara hii ya Miundombinu na Mawasiliano. Wamefuata taratibu, wameelekeza, wamekosoa, pakukemea wamekemea na kwa kweli hii ndio miongoni mwa kazi ambazo walitakiwa wafanye.

Mhe. Spika, nataka pia niwashukuru wajumbe wa kamati hii, kwa kazi nzuri ambayo wamefanya na nikiri hapa kwamba kamati hii inafanyakazi kwa mashirikiano makubwa na uongozi wote wa Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano.

Katika kufanya kazi hizi Mhe. Spika, kuna mambo mengi kama binadamu pengine yamejitokeza. Nataka niwaombe radhi wafanyakazi wote wizara hii kwa kamati hii kama kuna jambo lolote ambalo limetokea. Hawakufanya kwa makusudi wala kwa kudhamiria, lakini ni katika ufanyaji wa kazi. Kwa hivyo, wasichukulie kwamba kama lilitokea lilipangwa.

Mhe. Spika, nimshukuru Mhe. Naibu Waziri, kamanda Gavu kwa ufafanuzi wake wa yale mambo ambayo ameyafafanua. Ni imani yangu kwamba Waheshimiwa Wajumbe wamemsikia na wamemuelewa. Lakini pia nikiri Mhe. Spika, kwamba hata mimi kwa kunipa fursa hii sitamaliza kiu ya wajumbe wako, kama ulivyosema wajumbe ambao wamebakia ni karibu 20, ambao wamechangia ni kama 10 au 11. Kwa hivyo, kamati hii taarifa yake ingechangiwa na zaidi ya wajumbe 30, basi naamini kwamba kuna mambo mengine hayatarejea hapa kwa sababu pengine wajumbe hawakuyazungumza. Lakini nataka nikiri kwamba haya ambayo tutakua tunayajibu hapa, sio kwamba ni ufumbuzi wa moja kwa moja au wa kudumu, au niseme kwamba sio majibu ambayo yanatoa ufumbuzi kamili wa matatizo ambayo yameelezwa.

Mhe. Spika, mimi niende katika mambo mazito sita. Kwanza ni ucheleweshaji wa malipo ya fidia kwa wale ambao mali zao zimeathiriwa wakati wa ujenzi, na huu sio ujenzi wa barabara tu. Mhe Spika, sera ya serikali ni

kwamba kuna mali za namna mbili. Kuna mali kama jengo ambalo wananchi wanakaa na kuna mali kama miti, vipando na mambo mengine. Sera ya serikali ni kwamba hatuvunji nyumba ya mtu yeyote kwa ujenzi wowote, kabla ya mwenye nyumba ile kulipwa fidia inayostahiki. Kwa hivyo, katika suala hili la kuvunja nyumba, hadi sasa hakuna nyumba iliyovunjwa kwa ujenzi ambayo haijalipwa.

Mhe. Spika, nifafanue zaidi, ziko nyumba zimeathirika wakati wa ujenzi, hazikuvunjwa kabla ya ujenzi, pengine zimevunjika wakati wa ujenzi, kwa sababu tuna ma-*bulldozer* mazito, wakati yanapita yanashindilia ardhi, ardhi imeungana. Kwa hivyo, utakuta nyumba zimepasuka na mambo mengine. Kwa kawaida baada ya barabara kufunguliwa, ujenzi umekwisha tunafanya tathmini ya uharibifu uliopo na tunamlipa mwenye nyumba kwa uharibifu uliotokea.

Mhe. Spika, kwa vipando, miti na mimea. Hivi tunawaomba wananchi tena kwa kuwaelimisha kwamba katika *zone* hizi wasubiri na ndio utaratibu ambao tumeendelea nao kwa miaka mingi sasa. Ninachoahidi ni kwamba serikali katika hili hatufumbi macho na tumeanza kulipa vipando katika barabara ambazo tumetengeneza kwa Unguja na Pemba. Kwa mfano, barabara ya Mkwajuni Nungwi vipando vimelipwa, Makunduchi, Paje mpaka Michamvi na barabara kama hizo. Kwa hivyo, hili nataka nifafanue mapema kwamba hakuna nyumba ambayo imevunjwa kabla ya ujenzi haijalipwa fidia.

Mhe. Spika, kwa nini ujenzi wa barabara unachelewa kukamilika. Hili Mhe. Spika, wewe ni shahidi, nimekua nalieleza mara kwa mara katika kujibu maswali ya wajumbe wako. Nasema ziko sababu nyingi, nitoe mfano wa hivi karibuni kabisa. Mhe. Spika, ujenzi wa daraja zile nne, njia ya Mahonda Mkokotoni. Moja katika sababu iliyochelewesha, ukiachilia mbali kuchelewa kwa malipo ni hali ya hewa.

Mhe. Spika, imejengwa daraja karibu inataka kumalizika basi imekuja mvua isiyotegemewa, ardhi imechimbika, msingi ule ambao umejengwa kwa ajili hiyo yote iko nje na nusu ya daraja ile imekwenda. Sasa bila shaka ni hasara ya mjenzi, lakini maana yake ni kwamba ile kazi uliofanya mpaka kufikia pale uirudie tena. Sasa hiyo haikuhesabiwa katika mikataba ya ujenzi. Kwa hivyo, sababu nasema ziko nyingi. Moja ikiwa hiyo ya hali ya hewa kukata barabara.

Mhe. Spika, barabara ya Amani Dunga, kuna wakati lami ilimwagwa urefu wa mita 300, baada ya lami ile kumwangwa ilinyesha mvua kubwa mno, kwa hivyo lami yote ile ikawa haifai tena, ikatolewa na ikawekwa lami nyengine. Kwa hivyo, sio suala ambalo linapangwa ni suala ambalo linatokea. Suala jengine vile vile ni ucheleweshaji wa malipo, ama kwa mkandarasi kutokana na wanaofadhili au hata serikali.

Lakini vile vile na serikali uwezo wake, tunatakiwa sisi tuondowe vikwazo kama nguzo za umeme na mabomba ya maji, katika mikataba hii ni shughuli ya serikali, sasa serikali haiwezi kuondoa kama hana fedha za kuondolea na tunakwenda kwa mujibu wa bei. Fedha zipo lakini pengine hazijapatikana kwa ajili ya kufanyiwa kazi hii, serikali haina kazi moja, haina kazi ya barabara tu, ina kazi chungu nzima na wanaangalia sasa hivi tufanye nini ili tuonekane kwamba kila mahali tunafanya na kila mahali panaridhika. Mhe. Spika, ucheleweshaji una sababu nyingi.

Mhe. Spika, suala la taa za uwanja wa ndege wa Pemba. Mhe. Spika, hili ni suala vile vile tulikua tukilifafanua, lakini hivi ninavyokuambia ni kwamba tayari tuna ripoti kamili iliyotayarishwa hivi karibuni na kampuni moja ya *South Africa*, juu ya kuweka taa uwanja wa ndege wa Pemba, ili ndege ziweze kuruka usiku na mchana.

Mhe. Spika, kama alivyosema Mhe. Mjumbe hapa, hata kama kuna mvua, lakini suala la mvua sio suala la taa. Mimi nazungumzia kwamba kutakua na taa ambazo zitaruhusu ndege kuruka usiku na mchana. Mhe. Spika, inawezekana taa zipo, lakini ndege isiruhusiwe kuruka kama mvua ni kubwa mno. Ndio tukasema kwamba suala la taa na mvua ni vitu sio tofauti, lakini huwezi ukavikumbanisha. Kwa hivyo, tunatafuta fedha kwa ajili ya kukamilisha ripoti hiyo ya kuweka taa za barabarani kwa uwanja wa ndege wa Pemba.

Mhe. Spika, ufinyu wa bandari. Ufinyu wa bandari sasa hivi ni ajenda ndio maana serikali ikaona kwamba kuna umuhimu wa kujenga bandari mpya na hatua za ujenzi huo zinaendelea vizuri. Serikali ina mpango wa kujenga bandari mpya ambayo itaitwa Maruhubi au wengine wanasema Mpigaduri, jina madhubuti litaonekana baada ya ujenzi, lakini ama ni Maruhubi au Mpigaduri ni bandari itakayokua kubwa baada ya ujenzi huu kukamilika basi itakua ni bandari kwa ukanda mzima wa Afrika ya Mashariki. Sikusudii Afrika ya Mashariki kama Kenya, Uganda na Burundi. Lakini nakusudia kuanzia pembe ya Afrika ya Kaskazini mpaka pembe ya Afrika ya Kusini, ukanda wote wa Mashariki bandari hii kwa mahali ambapo ipo wataalamu wanasema kwamba hapa ni *the most strategic area* kwa ajili ya bandari kama hiyo. Meli zinazotoka Kaskazini ya Afrika zitaishia hapa, zitaweka mizigo hata kama inakwenda Afrika ya Kusini na meli zinazotoka Afrika ya Kusini zitaishia hapa

kuchukua mizigo inayotoka Afrika ya Kaskazini na kutua mizigo inayokwenda Afrika ya Kusini ni kitu kama hichi. Mwenyezi Mungu atujaalie dhamira hii ikamilike, imefikia hatua nzuri.

Mhe. Spika, juzi Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko hayupo. Mhe. Spika, watu wote wanajua kwamba mchele umepanda bei kutoka Shs.50 mpaka Shs.60. Kwa hivyo, katika miji kwa Unguja na Pemba hakukua na mchele wa kutosha. Juzi imekuja meli, nazungumzia ufinyu wa bandari. Imekuja meli ina tani 9,000 za mchele na ilipokuja meli ile tayari pale palikua na meli nyengine ya makontena. Sasa kwa sababu ni kwamba hakuna mchele katika nchi, basi tukaiondoa meli ya makontena ili kuiweka meli ya mchele na ni siku mbili tu wameweza kuteremsha tani 5,000 za mchele. Kwa hivyo, hakuna sababu sasa hivi, kama sababu ilikua mchele haupo ndio maana ukapanda bei, kwa sababu sasa hivi tayari kuna tani 5,000 katika miji tayari kwa kuuzwa.

Mhe. Spika, hizi tani 5,000 kwa hesabu za hapa zinaweza zikatuchukua zaidi ya miezi mitano, lakini mchele huu inaonekana mwingi unasafirishwa kwenda Bara. Tunawaomba wafanyabiashara, kama ni suala la kupeleka mchele Bara, basi waagize mchele na waupeleke Bara moja kwa moja, kwa sababu wanapouleta hapa, hapa kodi ya chakula ni ndogo mno. Au waseme kwamba huu tutaupeleka Bara ili serikali itoze kodi kwa ile bei ya kupeleka Bara, lakini serikali hapa imepunguza kodi ya chakula kwa makusudia ili Wazanzibari wanufaike, sasa Wazanzibari hawanufaiki.

Kwa hivyo, wafanyabiashara ni vizuri hili mulijue. Pia wananchi vile vile wajue kwamba sio suala la kua kuna ushuru mkubwa ni kwamba wafanyabiashara wengine mchele huu ukifika hapa wanautoa kwa kodi ndogo, wanauzungusha na kuusafirisha pahala pengine, sidhani kama hii ni tabia nzuri. Hivyo, wasitake serikali ikachukua hatua ambazo sio nzuri sana kwa wafanyabiashara.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, ingekua sio ufinyu wa bandari basi meli zote mbili au tatu zingeweza kujipanga pale na kuweza kuteremsha mizigo kwa wakati mmoja. Kwa taarifa tu ya wananchi ni kwamba zile *crane* mbili ambazo ziliagizwa na Shirika la Bandari, tayari zimewasili ni mpya na wakati wowote kuanzia sasa hivi zitafanyakazi. Tunategemea kwamba kutakua kuna ufanisi mkubwa sana wa uteremshaji wa mizigo, lakini bado bandari ni finyu, kuna meli tatu zinakuja za makontena karibu 1,800 na hayo tunaangalia wapi tuyaweke. Vinginevyo tukiendelea kuchelewa basi makontena haya yataweza kupelekwa Mombasa.

Kwa hivo, wafanyabiashara wa hapa na wenye mali zao hapa wanaweza wakachelewa zaidi, hivyo ni vizuri kabisa wananchi wakafahamu kwamba ufinyu wa bandari yetu unasababisha serikali kuhakikisha kwamba inapata nyengine.

Mhe. Spika, kwa heshima yako, na kwa ruhusa yako nasema na kwa sababu ya wakati nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kufafanua machache ambayo wananchi wanayasikia, nakushukuru sana.

Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunirudisha tena hapa ili kuweza kutoa majumuisho ya hoja za wajumbe, mawaziri wangu pamoja na manaibu wangu.

Mhe. Spika, kwanza nawashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe waliochangia kamati hii kwa ufanisi mzuri. Kama mimi mwenyewe nilivyoiwasilisha hii ripoti hapa, niliitoa kwa ufanisi mzuri hata nyinyi wenyewe mmeifurahia.

Mhe. Spika, kwanza niwapongeze wale ambao wamechangia akianzia na kamanda wangu mkuu;

Mhe. Hija Hassan Hija
Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi
Mhe. Rashid Seif Suleiman
Mhe. Mohammed Haji Khalid
Mhe. Hassan Hamad Omar
Mhe. Asha Bakar Makame
Mhe. Subeit Khamis Faki
Mhe. Farida Amour Mohammed
Mhe. Bikame Yussuf Hamad
Mhe. Fatma Mbarouk Said
Mhe. Salim Abdalla Hamad
Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati
Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati
Mhe . Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano

Mhe. Spika, nawashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe, katika michango yao, wengi masuala yao yamejirejea, lakini na mimi nawaunga mkono pia. Vile vile niwashukuru sana Waheshimiwa Mawaziri, kwa kweli nimefarijika sana katika wizara zangu hizi mbili pamoja na manaibu wao. Wamejibu hoja vizuri na zenye muelekeo wa utekelezaji.

Mhe. Spika, na mimi watanipa faraja kubwa sana katika hoja zao ziwe za utekelezaji ili mara nyengine tena nisipate tatizo wakati wa bajeti. Vile vile nimuambie Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano, kua ni kweli nina dhamira ya kwenda Hijja, ndio maana najaribu sasa kufuta yale yaliyokua yatanikwaza ili nisiende Hijja ndio maana ninasema ukweli. Naomba kwa hili wazidi kuniombea dua, najua Mhe. Spika, wewe ukesharudi na mimi niko njiani nitakwenda tena ili nipate na mimi kwenda kuhiji.

Pia nisisahau kua neno Hija na neno Makka niliambiwa na mtaalamu wangu kua Makka ni nchi, lakini kwa vile wenzangu wananitabiria niende Hijja basi nakubaliana nao niende Hijja. Kwa kumalizia Mhe. Spika, kuna mambo kidogo ningeomba kwamba tuna ukosefu wa ku-*acting* unaibu kwa muda mrefu sana katika shirika la bandari, ningemuomba sana Mhe. Rais hili alione kwa kupitia kwa Mhe. Waziri kua yule Naibu Katibu Mkuu halafu ana- *acting* tena katika nafasi ya ukurugenzi basi atusaidie upesi, kwa sababu kuondoa mzigo ule, kama tunavyoelewa bandari ni sehemu ambazo ni za harakati sana hasa ni za kuleta uchumi. Kwa hivyo, tungeomba hili tusaidiwe ili kuweza kuekeza pale.

Vile vile tungeomba kwa upande wa Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati kuna mwenyekiti yule wa bodi ya uhaulishaji, mpaka sasa hivi bado hajapatikana. Tungeomba na hili tuharakishiwe haraka sana ili zile ardhi ziweze kuhaulishwa na kuweza kupata mapato.

Lakini la mwisho namuomba sana Mhe. Fatma Mbarouk Said, asitumie kauli ile mwenyekiti hajaingia mitini, isipokua mwenyekiti kuna mambo yamemkwaza tu ndio mambo ya kibinadamu tu. Kwa hivyo, namuomba sana kua hilo jambo afute mara moja mjumbe. La kama katumwa sawa, lakini hakuna tatizo Mwenyezi Mungu ndiye mwenye uwezo. Mhe. Spika, naomba kutoa hoja, ahsante sana.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, hoja imetolewa, niwahoji basi wale waliopokea ripoti hii wanyanyue mikono. Wanaokataa ripoti. Waliokubali ripoti wameshinda. Ripoti sasa iko tayari ifanyiwe kazi na serikali.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, nakushukuruni. Nilikua napendelea sana kwamba tupate muda wa kutosha wa kuwasikiliza wajumbe, ili kuchangia ripoti hizi ambazo ndio hasa kazi ya usimamizi kwa serikali na kamati inapofanyika. Lakini muda unatukwaza kidogo. Narudia tena kuwaomba radhi juu ya jambo hilo.

Waheshimiwa Wajumbe, mara baada ya kuakhirisha kikao hichi wanaombwa wajumbe wa Baraza hili kutoka upande wa CCM wabaki kidogo kuna jambo muhimu, ambapo mjumbe wa kamati kuu mnadhimu mwakilishi wa CCM anataka kuzungumza nao. Nashukuru ujumbe huo umefika.

Waheshimiwa Wajumbe, baada ya hayo machache tuelewe tu kwamba jioni tunaanza na Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii. Kwa hivyo, ningewaomba wahusika wote wakawa tayari ili tukaifanya kazi hiyo kwa ufanisi mkubwa.

Baada ya hayo Waheshimiwa Wajumbe, naakhirisha kikao hichi hadi saa 11:00 leo.

(Saa 7:00 mchana Baraza liliakhirishwa hadi saa 11:00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Hija Hassa Hija (Makamo Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii): Mhe Spika, awali ya yote nachukua nafasi hii jioni ya leo kukushukuru kwa ajili ya kunipatia nafasi ya

kuwasilisha muhtasari wa hotuba kuhusu Ripoti ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii kwa mwaka wa fedha 2011/2012.

Mhe. Spika, awali ya yote napenda kumkushuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uwezo wa kusimama mbele ya Baraza lako tukufu nikiwa mzima wa afya, ili kuwasilisha muhtasari wa hotuba ya Ripoti ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii kwa mwaka 2011/2012.

Mhe. Spika, shukrani zangu pia ziwafikie Wajumbe wa Kamati, watendaji wa Wizara ya Afya,Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali pamoja na Wizara ya Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto kwa mashirikiano ya kutosha waliyotupa wakati wa utekelezaji wa kazi za Kamati.

Mhe. Spika, baada ya utangulizi huo, ni vyema kuwataja Wajumbe wa Kamati ambao walihusika katika kazi za Kamati. Wajumbe hao ni:-

1. Mhe.Amina Iddi Mabrouk - Mwenyekiti
2. Mhe Hija Hassan Hija - Makamo Mwenyekiti
3. Mhe.Asha Abdu Haji - Mjumbe
4. Mhe Ashura Sharif Ali - Mjumbe
5. Mhe Mwanaidi Kassim Mussa - Mjumbe
6. Mhe Jaku Hashim Ayoub - Mjumbe
7. Mhe Nassor Salim Ali - Mjumbe
8. Mhe Saleh Nassor Juma - Mjumbe
9. Nd. Talib Enzi Talib - Katibu
10. Nd. Asha Said Mohamed - Katibu

Mhe. Spika, Majukumu ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii yameelezwa na kuainishwa katika Kanuni ya 110 ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi Toleo la mwaka 2011.

Miongoni mwa majukumu hayo ni kufuatilia utekelezaji wa sera na mipango ya Wizara husika kwa mujibu wa malengo yaliyowasilishwa Barazani wakati wa usomaji wa bajeti na hotuba nyengine za Waziri alizotoa Barazani.
Aidha kufuatilia mapato na utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya kitaifa na miradi ya wananchi iliyo chini ya wizara husika, pamoja na kuchunguza na kufuatilia mapato na matumizi ya kila mwaka ya serikali kwa wizara husika, ambazo kwa upande wa kamati yetu inasimamia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Wizara ya Afya na Wizara ya Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Wanawake, Vijana na Watoto.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2011/2012 kamati yetu iliweza kutekeleza majukumu hayo niliyoyataja katika kipindi cha wiki sita Unguja na Pemba. Kamati ilipokea taarifa za utekelezaji wa malengo ya wizara hizo, mapato na matumizi pamoja na miradi ya maendeleo na ile ya wananchi.

Aidha kamati ilitembelea baadhi ya taasisi zilizo chini ya wizara hizo tatu, kwa lengo la kufuatilia utekelezaji na hatimae kutoa maoni na maagizo, ambayo kamati imeona yatafaa katika kuisaidia serikali kufikia malengo yake ya kuleta maendeleo kwa wananchi wote wa Zanzibar.

Mhe. Spika, nianze na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kuhusu Ufuatiliaji wa Suala la Matokeo ya Mitihani Tanzania:

Hali iliyojitokeza:

Mhe. Spika, kamati yetu imehuzunishwa sana na tokeo la udanganyifu wa mitihani ya kidato cha nne kwa mwaka uliopita, hali iliyopelekea kufutiwa matokeo ya mitihani zaidi ya wanafunzi elfu tatu, ambao kutoka Zanzibar ni zaidi ya asilimia 70 ya watihaniwa wote waliofutiwa mitihani hiyo. Kwa kweli ni jambo la kusikitisha.

Hatua zilizochukuliwa:

Kamati yetu haikuridhika kiurahisi baada ya kupata taarifa za tukio hilo. Hatua zilizochukuliwa na kamati ni tulionana na wadau wote wa suala hili, yaani Wizara ya Elimu na Mafumzo ya Amali, Baraza la Mitihani Tanzania pamoja na Kamati ya Wazee wa Watoto waliofutiwa matokeo ya mitihani hiyo. *(Makofi)*

Mhe.Spika, miongoni mwa agenda zilizochukua muda katika vikao vya Kamati na Uongozi wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, ilikua ni suala hilo na baadaye Kamati iliridhika kutokana na ushahidi wa vielelezo mbali mbali vilivyothibitisha kutokea kwa udanganyifu huo, ambao uliokua na mbinu za ufundi wa hali ya juu.

Mhe.Spika, kamati inaipongeza wizara kuona umuhimu wa kuipeleka Kamati yetu hadi Dar-es-Salam na kuweza kukutana na Baraza la Mitihani Tanzania, ili kufahamu undani wa kadhia hiyo.

Mhe. Spika, Baraza la Mitihani kwa mashirikiano ya hali ya juu na Kamati yetu iliweza kutuonesha hadi ushahidi wa baadhi ya majibu halisi ya mitihani hiyo, kwa lengo la kufahamu mbinu na namna ya udanganyifu huo jinsi ulivyofanyika.

Mhe. Spika, Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii inalishukuru Baraza la Mitihani Tanzania kukubali wazo la Kamati la kutaka kupunguziwa adhabu wanafunzi waliofutiwa matokeo hayo, kwa kutoweza kurejea mitihani kwa kipindi cha miaka mitatu na badala yake adhabu hiyo iwe chini ya hapo. Baraza la Mitihani Tanzania linakusudia kukaa, ili kupitia pendekezo hilo.

Kamati imeona ingawa kosa limetokea lakini hicho ni kipindi kikubwa kwa vijana wetu kubaki bila ya kusoma, hali ambayo inaweza kupelekea madhara mengine ya vijana hao kujiingiza katika vitendo vya uhalifu vikiwemo dawa za kulevya.

Hali iliyojitokeza hivi sasa:

Mhe. Spika, licha ya kuwepo kwa ushahidi wote huo niliouleza kabla ambao ulipelekea kamati yetu kuridhika kutokea kwa udanganyifu huo wa mitihani. Hivi sasa Mhe. Spika, kumejitokeza hali ya utatanishi baada ya kamati yetu kukutana na Kamati ya Wazee wa Wanafunzi wa Zanzibar, ambao wameathirika na kufutiwa matokeo ya mitihani hiyo.

Mhe.Spika, miongoni mwa hoja za msingi za Kamati hiyo ya wazee ni:-

1. Kujitokeza hali isiyo ya kawaida kwa Baraza la Mitihani Tanzania hivi sasa kutoa tena matokeo mazuri ya mitihani hiyo katika baadhi ya skuli ambazo hapo awali zilifutiwa matokeo hayo.

2. Utata mwengine Mhe. Spika, ni ule wa baadhi ya wanafunzi wa masomo ya Sanaa kuletewa matokeo ya mitihani ya Sayansi, ambapo wanafunzi hao hawakufanya mitihani hiyo kabisa kabla.

3. Mhe. Spika, hivi sasa kuna baadhi ya wanafunzi wenye uwezo wamekuwa wakipata matokeo yenye viwango vya divisheni nzuri vya kufaulu baada ya kukata rufaa.

4. Mhe. Spika, ni kwa wanafunzi wengine ambao hawana uwezo wa kuweka mawakili na kukata rufaa, ambapo matokeo yao hivi sasa yamekua yakiendelea kutolewa bila ya utaratibu unaostahili yaani bila ya hata kukata rufaa baada ya kufutiwa, ambayo ni ya viwango vya *Division Four* hadi *Zero*. Kwa mfano, Skuli ya Hamamni jumla ya wanafunzi 35 hivi sasa wamepata matokeo yao bila ya kuomba.

5. Mhe. Spika, ni kuhusu lalamiko la wanafunzi wa skuli nne za binafsi za Zanzibar za *Philter Federal*, *Lauriet*, *Highview* na Sufa kwa Baraza la Mitihani Tanzania kuhusu kutoletewa matokeo ya somo la *Fine Arts*.

   Mhe.Spika, skuli hizo lililiarifu Baraza hilo kua hawakupata matokeo ya mitihani hiyo kwa somo hilo, na jibu la Baraza la Mitihani lilikua ni kwamba mitihani hiyo haikufika katika Baraza. Kilichoendelea baadaye Mhe. Spika, Baraza hilo limeziandikia skuli hizo hoja ya kutaka kurejea tena mitihani ya somo hilo.

Mhe. Spika kwa kweli hizo ni baadhi tu ya hoja ambazo Kamati yetu inaona ni za msingi na kutokana na uzito wa suala hili zinahitaji kufuatiliwa zaidi.

Ushauri wa Kamati:

Mhe. Spika, kamati yetu hivi sasa imepata mashaka juu ya jambo hili, hivyo kutokana na uzito wa suala hili, Kamati inalishauri Baraza lako tukufu kuona umuhimu wa kuunda Kamati Maalum, ili kuchunguza jambo hili

kutokana na hali iliyojitokeza hivi sasa, kwani wazee walio wengi hawakuridhika na maamuzi yaliyotolewa na Baraza la Mitihani na hali halisi inayoendelea hivi sasa juu ya suala hilo.

Aidha, kwa kua kuna tuhuma za baadhi ya maafisa wa taasisi nyengine wakiwemo wa vyombo vya ulinzi kushiriki katika udanganyifu wa mitihani hiyo, kuna haja pia hali hiyo kufanyiwa uchunguzi, ili kuwabaini watuhumiwa hao na kuchukuliwa hatua za kisheria. Mhe. Spika, kuendelea kuachia kuwa na mfumo wa mitihani, ambao mara nyingi huhusishwa na madai ya kuwepo kwa udanganyifu ni tatizo katika maendeleo ya elimu nchini.

Wakati umefika Mhe. Spika, kupitiwa upya Sheria za Mitihani, ili kuepuka kuwabana wanafunzi pekee kwa adhabu wakati unapotokea udanganyifu, ambapo wakati mwengine hata vyombo husika vya usimamizi wa mitihani hiyo hupaswa kuwajibika.

Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii ya Baraza la Wawakilishi inawataka Wazanzibari kuiamini Kamati yetu kama ni chombo cha wananchi, kwa kweli udanganyifu wa mitihani ulifanyika licha ya hivi sasa kujitokeza kwa baadhi ya madai na hoja ambazo pia zinahitaji mazingatio kutokana na umuhimu wa suala hili. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kamati yetu inaipongeza sana Skuli ya Sekondari na ya Msingi ya Mtopepo kwa mafanikio yaliyopatikana na kua ni skuli iliyotoa mfano katika kujenga nidhamu ya ufanyaji wa mitihani pamoja na matokeo mazuri kwa kidato cha pili na cha nne kwa mwaka 2011.

Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (State University of Zanzibar - *SUZA*):

Mhe. Spika, kamati haikuridhika na utekelezaji wa malengo ya Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (*SUZA*) katika kipindi cha awamu mbili za mwanzo za utekelezaji wa malengo ya bajeti ya 2011/2012, kutokana na kushindwa kufikia malengo hayo kwa karibu asilimia 70. Kutokana na umuhimu wa maendeleo ya Chuo chetu Kikuu katika mustakbali wa Sekta ya Elimu Zanzibar.

Kamati yetu imeishauri Wizara kufuata utaratibu wanaoutumia Wizara ya Ustawi wa Jamii wanaposhindwa kufikia malengo yao hasa katika mambo ya msingi, kumuona Mhe. Rais ili kujenga hoja juu ya changamoto za msingi zinazozikabili chuo hicho pamoja na athari zake katika maendeleo ya baadaye ambazo kwa kiasi kikubwa zimechangia kutofikiwa kwa malengo ya chuo. Aidha Mhe. Spika, kamati inaishauri serikali kutumia zaidi vyuo vyake vikuu vya ndani katika uendeshaji wa tafiti, kongamano na semina mbali mbali, ili kupunguza gharama za uendeshaji wa tafiti hizo pamoja na kuwapa nafasi zaidi wataalamu wetu.

Mamlaka ya Mafunzo ya Amali Zanzibar:

Mhe. Spika, utakumbuka Baraza lako tukufu lilipitisha sheria, ili kupata uhalali wa kuanzishwa Mamlaka ya Mafunzo ya Amali nchini kisheria kwa lengo la kutoa fursa kwa vijana wetu chini ya usimamizi wa chombo hiki kupata elimu ya amali na kuweza kujiajiri.

Jambo la kusikitisha Mhe. Spika, kamati yetu imebaini kua chombo hiki kinadharauliwa. Kutokana na kuendelea kwa hali hiyo kuna uwezekano mkubwa wa Mamlaka hiyo kupoteza malengo yake na hatimaye kushindwa kufanyakazi hapo baadae.

Mhe. Spika, katika utaratibu wa uendeshaji wa Mamlaka ya Mafunzo ya Amali kuna ruzuku ambayo hutolewa na Serikali kuu na Kodi ya "*Skill Development Levy*" ambayo hutolewa kupitia waajiri binafsi kwa lengo la kusaidia shughuli za uendeshaji wa Mamlaka hiyo.

Mhe. Spika, kwa utafiti mdogo ambao kamati yetu imefanya, kodi hizo za *Levy* zimekuwa haziingii kwa ufanisi katika Mfuko wa Hazina. Wizara ya Fedha inapatiwa kwa wastani shilingi milioni 350 kama ni "*Skill Development Levy*" lakini kwa misingi ile ile ya Wizara ya Fedha, hudharau ama kutoona umuhimu katika kutekeleza wajibu wake wa kuzipatia mafungu yake kama yalivyoidhinishwa na Baraza lako, taasisi muhimu kama Mamlaka hiyo na kupelekea usumbufu kwa wataalamu katika kufikia malengo ya kitaasisi.

Mhe. Spika, kiasi cha miaka miwili sasa tangu kuanzishwa kwa Mamlaka ya Mafunzo ya Amali, serikali imeshindwa kuchangia licha ya kuwepo mchango wa kodi hiyo kutoka kwa waajiri binafsi, ambao unasimamiwa na *TRA*.

Mhe. Spika, Maendeleo ya Taasisi ya *VETA* kule Tanzania Bara yametokana na Serikali ya SMT kujali na kuzingatia umuhimu wa taasisi hiyo, ambapo imekua ikiipatia asilimia 2 ya asilimia 6 ya kodi, hali ambayo imepelekea *VETA* kufanya vizuri hata kuliko Vyuo Vikuu na kusaidia vijana wetu kujiajiri na kupunguza tatizo la ajira nchini.

Mhe. Spika, kamati yetu inaitaka Wizara ya Fedha kulielewesha Baraza lako tukufu, kuna tatizo gani linalozuia Wizara yetu ya Elimu kupatiwa mchango wa kodi ya *Levy*, ili iweze kusaidia katika uendeshaji wa Mamlaka ya Mafunzo ya Amali Zanzibar kwa mujibu wa utaratibu uliowekwa. Hivyo ni muhimu kwa Wizara ya Fedha kukaa na Mamlaka husika, ili kuelewa malengo yake likiwemo la kupunguza tatizo la ajira kwa vijana nchini.

Mhe. Spika, lazima serikali ikubali kua uendeshaji wa Elimu ya Ufundi ni gharama, lakini ikiendelezwa ipasavyo itasaidia mara moja kuleta maendeleo ya nchi. Gharama za Elimu ya Ufundi ni mara nne ukilinganisha na gharama za uendeshaji wa Elimu ya Sekondari, ndio maana karibu nchi zote duniani hutumia kodi za *Levy* kuimarisha Elimu ya Ufundi.

Mhe. Spika, kamati yetu imebaini kua kuna tatizo la *Scheme of Service* katika Mamlaka ya Mafunzo ya Amali. Kamati imegundua kua licha ya kufanyiwa mabadiliko ya mishahara ya walimu na wafanyakazi katika Mamlaka hiyo, bado Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kupitia Mamlaka ya Mafunzo ya Amali inaendelea kuwalipa walimu na wafanyakazi hao mishahara ya zamani. Wakati kamati ilipokutana na Mamlaka na taasisi zake, Mamlaka ilikiri kuwepo kwa tatizo la *Scheme of Service* kwa wafanyakazi na walimu wake.

Kwa taarifa Mhe. Spika, Wizara ya Fedha imeanza kuwaingizia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali fedha kwa ajili ya malipo ya mishahara mipya ya walimu na wafanyakazi wa Mamlaka miaka miwili sasa. Lakini la kushangaza kuna malalamiko ya kutokulipwa mishahara mipya kwa wafanyakazi hao. Mhe. Spika, kamati inamtaka Waziri wa Elimu atueleze fedha hizo zimetumika kwa malengo yepi, ili kuepuka tuhuma zilizopo kua wizara imefanya maamuzi ya kutumia fedha hizo kwa ununuzi wa vifaa.

Kuhusu Wizara Kusita Kujiunga na Mfumo wa Pamoja wa Udahili Wanafunzi wa Vyuo Vikuu:

Mhe. Spika, kamati yetu imeona kua hakuna athari kwa Wizara yetu ya Elimu na Mafunzo ya Amali kujiunga katika mfumo huo, ambao unasimamiwa na Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (*TCU*).

Jukumu kuu la Tume hii Mhe. Spika, ni kufanya udahili wa wanafunzi kwa vyuo vyote vikuu nchini ambavyo vimejiunga na mfumo huo, ili kuweza kupata wanafunzi wenye sifa za kujiunga na vyuo hivyo kupitia Mikopo ya Serikali, ambayo hutolewa na Bodi ya Mikopo Tanzania baada ya kupokea majina ya wanafunzi wote wenye sifa yaliyofanyiwa udahili na Tume hiyo ya Vyuo Vikuu Tanzania.

Mhe. Spika, miongoni mwa madai ya msingi ya Wizara ya Elimu dhidi ya mfumo huo, ni kwamba baada ya *TCU* kukamilisha utaratibu wa udahili katika kuwapata wanafunzi wenye sifa na Bodi ya Mikopo kuthibitisha udhamini wa mikopo, Chuo Kikuu chetu cha *SUZA* hupatiwa wanafunzi wengi kutoka nje ya Zanzibar, ambapo malengo ya *SUZA* ni kuchukua wanafunzi zaidi wa Zanzibar.

Hivyo, Mhe. Spika kamati yetu inaishauri wizara kujenga hoja kwa Tume juu ya madai yao na sio wizara kuendelea kusita kujiunga na mfumo huo wa udahili. Kwa taarifa Mhe. Spika, Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania baada ya kukutana na kamati yetu imekiri kua Wizara ya Elimu ina madai ya msingi na imeonekana kukubali kuzingatia madai ya wizara kwa ajili ya kufikia malengo ya maendeleo ya Chuo Kikuu cha *SUZA*.

Kwa maana hiyo, ipo haja kwa Wizara kufikiria kujiunga katika mfumo huo wa pamoja wa udahili, ili kuwawezesha wanafunzi wa Zanzibar wenye sifa za kujiunga na elimu ya juu kupata fursa zaidi ya kupatiwa mikopo kupitia Bodi ya Mikopo Tanzania.

Hata hivyo kamati yetu imeihimiza Bodi ya Mikopo Tanzania Bara kutoa mikopo kwa wanafunzi wa Zanzibar wenye sifa kwa uiano hasa kwa kuzingatia kua Zanzibar ni sehemu ya pili ya nchi badala ya kuendelea na utaratibu uliopo wa kutoa mikopo hiyo kiujumla jumla.

Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu Zanzibar:

Mhe. Spika, ingawa serikali imeamua kuweka vipaumbele vyake katika kuwapatia mikopo zaidi wanafunzi katika kada ya sayansi. Hata hivyo, kamati yetu inatoa rai kua kuna umuhimu pia kuzingatia hali ya usawa katika kufaidika na rasilimali za nchi zilizopo.

Hivyo, ipo haja kwa serikali kutenga asilimia maalum ya mikopo kwa ajili ya wanafunzi wa kada ya sanaa (*Arts*) na nyenginezo kwa lengo la kuleta usawa katika kufaidika na rasilimali zilizopo.

Aidha Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii inaishauri Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu Zanzibar kutafuta njia muwafaka za kukabilina na changamoto ya urejeshwaji wa madeni ya zamani pamoja na namna ya ulipaji wa mikopo kwa watu binafsi.

Kamati pia inaiagiza wizara busara zitumike, ili mikopo iliyotolewa kwa wanafunzi wa elimu ya juu ambao sasa ni waajiriwa katika taasisi za serikali iweze kurejeshwa. Deni la shilingi bilioni nane kwa waliokopa ni kubwa na linaathiri maendeleo ya Bodi.

Baraza la Mitihani la Zanzibar:

Mhe. Spika, kamati yetu inalipongeza Baraza lako tukufu kuona umuhimu wa kuwa na Baraza letu la Mitihani Zanzibar baada ya kupitisha sheria hivi juzi ya kuanzisha baraza hilo. Aidha iwapo tutaanzisha utaratibu wa kuwa na mitihani ya darasa la 12 Zanzibar tutaweza kuokoa fedha nyingi za walipa kodi kulipia mitihani ya darasa la 12 kule *NECTA* (Baraza la Mitihani Tanzania).

Mhe. Spika, hivi sasa Zanzibar tunalipia kila mwaka si chini ya milioni 600 kwa ajili ya mitihani ya darasa la 12. Kwa hivyo, tukiwa na Baraza letu la Mitihani, basi fedha hizo zitaweza kurudi ndani ya chombo chetu ambacho ni Baraza letu la Mitihani la Zanzibar.

Aidha kamati imebaini kua serikali inaendelea kutumia gharama nyingi za nje kwa ajili ya uchapishaji wa mitihani. Kamati inaishauri serikali kuwa na kiwanda chake cha uchapishaji mitihani, ili kuepuka kuendelea kutumia gharama hizo pamoja na kuondoa wasi wasi wa kuwepo kuvuja kwa mitihani na kupelekea udanganyifu.

Mradi wa Ujenzi wa *Campus* ya Chuo cha Ualimu cha Benjamin Mkapa:

Mhe. Spika, kamati inaipongeza Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa hatua nzuri iliyofikiwa ya Mradi wa Ujenzi wa *Campus* ya Chuo cha Ualimu cha Benjamin Mkapa Pemba. Hata hivyo, inaishauri serikali kuanzisha skuli ya mazoezi (maandalizi na msingi) ndani ya chuo hicho, ili kurahisisha upatikanaji wa mafunzo ya vitendo kwa walimu.

Wizara ya Afya

Mradi wa Chuo cha Madaktari cha Zanzibar

Mhe. Spika, Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii inaishauri serikali kukifanyia mapitio na kutafuta namna ya kukiimarisha Chuo cha Madaktari cha Zanzibar, ili kiweze kutoa madaktari wenye uwezo kitaaluma na kusaidia Sekta ya Afya nchini.

Chuo hichi kina umuhimu wa aina yake kwa vile ni tegemeo la Madaktari Wazalendo wa baadaye. Eneo la chuo linalotumika hivi sasa ni dogo sana kiasi ambacho ni vigumu kuweza kuchukua wanafunzi wapya kutokana na upungufu wa majengo. Aidha kamati imebaini kua miongoni mwa eneo jengine la msingi ambalo kuna haja kwa serikali kulizingatia, ni ukosefu wa wafadhili katika Mradi wa Chuo, hali ambayo hupelekea chuo kutegemea fedha za serikali tu ambazo kwa kweli hazitoshelezi.

Mradi wa Ujenzi wa Bohari Kuu ya Dawa na Afisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali Zanzibar

Mhe. Spika, kamati imeridhika na hatua ya maendeleo ya Mradi wa ujenzi wa Bohari Kuu ya Dawa Zanzibar chini ya washirika wa maendeleo *USAID* na *DANIDA* pamoja na mchango wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Serikali imechangia jumla ya shilingi milioni 100 kati ya shilingi milioni 200 zilizopangwa kutolewa.

Jumla ya shilingi bilioni moja nukta mbili zimepangwa kutumika katika mradi huu ambao unatarajiwa kumalizika mwezi May 2012 na kukabidhiwa June 2012. Kamati inaisisitiza wizara kuendelea kuimarisha ufuatiliaji, ili kuhakikisha kua ujenzi huo unamalizika kwa wakati kama ilivyokusudiwa. Hata hivyo, kamati yetu inaiagiza Wizara ya Afya kuharakisha kuanza ujenzi wa jengo la Afisi za Mkemia Mkuu wa Serikali, ili chombo hicho muhimu kiweze kufanya kazi zake kwa ufanisi.

Hospitali ya Mnazimmoja kuwa Hospitali ya Rufaa

Mhe. Spika, kamati yetu inaipongeza wizara kwa kushirikiana na Shirika la *ICAP* kufanya matengenezo makubwa katika maabara ya Hospitali ya Mnazimmoja. Kufuatia matengenezo hayo kutasaidia kuifanya maabara hiyo kuweza kufanya vipimo vingi na hata kuwa katika kiwango kizuri chenye kulingana na maabara nyengine. Aidha kamati inapongeza serikali kwa kufanya uwamuzi wa kufanya matengenezo katika Kitengo cha Meno katika Hospitali ya Mnazimmoja na kuwekwa vifaa vipya vya kisasa kupitia ufadhili wa *Miracle Coners of the World*.

Kitengo cha Wagonjwa Mahututi

Mhe. Spika, kamati ilitembelea Kitengo cha Wagonjwa Mahututi (*ICU*) katika Hospitali ya Mnazimmoja. Kamati ilielezwa kua tayari Bodi ya Zabuni ya Wizara ya Afya imewateua wakandarasi wawili walioshinda ambao ni Kampuni ya *LAB EQUIP* kwa ajili ya kuleta vifaa na Kampuni ya *TOL GASES* kwa ajili ya kusambaza bomba za hewa safi (*centralized oxygen system*).

Mkandarasi wa *TOL GASES LIMITED* aliiomba wizara kumtangulizia asilimia 20 ya malipo sawa na Tsh. 59,910,046 na tayari wizara imefanya hivyo. Kampuni ya *LAB EQUIP* imeahidi kukamilisha na kukabidhi kazi kwa wizara ndipo apatiwe malipo yake yote kamili. Baada ya kufikia makubaliano hayo, wakandarasi wote wameahidi kukamilisha kazi na kuikabidhi wizara kabla ya mwezi wa Julai 2012. Mhe. Spika hiyo ndio hali inayoendelea katika hatua za awali za matengenezo ya *ICU* katika hospitali ya Mnazi Moja.

Kitengo cha Kupambana na UKIMWI

Mhe. Spika, katika kufanikisha juhudi za mapambano dhidi ya maradhi ya UKIMWI, kamati yetu imeitaka Wizara ya Afya kuvishauri Vituo vya Afya vya Binafsi kuwa tayari kupeleka wauguzi wao kupata mafunzo ya "*Nurse Assistance*", ili waweze kusaidia katika utoaji wa huduma za dawa za *ARV* kwa mujibu wa utaratibu wa Kitengo cha Huduma za Maradhi ya UKIMWI.

Kitengo cha Kupambana na Malaria

Aidha kamati inakipongeza Kitengo cha Kupambana na Malaria katika juhudi zake za kupambana na malaria nchini.

Hata hivyo, imekishauri kitengo hicho kujenga hoja za kitaalamu, ili kuweza kupatikana dawa mbadala na mchanganyiko ambazo zitaua mbu wanaosababisha malaria na maradhi mengine.

Hospitali za Wilaya na Vijiji. (*Cottages Hospitals*)

Mhe. Spika, kwa kua wizara imekamilisha muongozo wa tathmini wa kubaini kasoro katika ngazi ya hospitali za wilaya na vijiji - *cottages hospitals*. Kamati inaishauri serikali kuzitafutia ufumbuzi wa haraka vikwazo vya msingi vinavyoikabili hospitali nyingi za wilaya na vijiji Unguja na Pemba, ili kusaidia upatikaji wa huduma za msingi za afya katika maeneo hayo.

Miongoni mwa changamoto hizo ni pamoja na tatizo la upungufu na ukosefu wa huduma ya maji safi, kukosekana kwa baadhi ya dawa muhimu, upungufu wa wauguzi na madaktari,vifaa muhimu na sehemu za kuhifadhia mashine muhimu kama vile *Ultra-Sound* katika Hospitali ya Makunduchi,

Chuo cha Taaluma za Sayansi za Afya

Mhe. Spika, kamati inakipongeza Chuo cha Taaluma za Sayansi za Afya kwa kua na ubunifu na kuweza kuimarisha maendeleo ya chuo hicho. Miongoni mwa mafanikio ya chuo ni pamoja na kua na mpango wa kuanzisha utoaji wa mafunzo ya afya kupitia mtandao "*E-Learning*" chini ya msaada wa wataalamu kutoka Uingereza na Ujerumani, ujenzi wa uzio wa chuo, kuzishauri taasisi binafsi, ili kusaidia kuwapatia mikopo wanafunzi wa *Diploma* wa chuo.

Pia chuo kimeweza kuanzisha utaratibu mpya wa teknologia ya kisasa kupitia "*Website*" ambao utatumiwa na wanafunzi wakati wa kujiunga na chuo. Aidha kimeweza kuanzisha ujenzi wa jengo jipya la Elimu ya juu pamoja na dahalia mbili za wanawake ikiwa ni msaada kutoka Serikali ya Oman.

Mhe.Spika, kamati inaiagiza Wizara ya Afya kuhakikisha kua inashirikiana na Chuo cha Taaluma za Sayansi za Afya katika kukipatia ruzuku chuo hicho kama inavyopatiwa vyuo vyengine, ili kiweze kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma.

Mhe. Spika, kuhusu Mradi wa Mabadiliko ya Sekta ya Afya, kamati yetu inaishauri serikali kuijengea uwezo zaidi *Secretariate* inayosimamia Mabadiliko ya Sekta ya Afya Zanzibar, ili iweze kukabiliana na changamoto za mahitaji ya msaada wa ushauri wa kitaalamu kutoka Taasisi za Kimataifa ambao umeonekana kuwa na gharama kubwa.

Mhe. Spika, mwisho kwa upande wa Wizara ya Afya, kamati yetu inaelezea kusikitishwa kwake na kuwepo kwa mchango mdogo wa fedha za serikali katika maeneo mengi ya Sekta ya Afya katika utekelezaji wa miradi ikilinganishwa na makisio yaliyopangwa.

Iwapo serikali itaendelea na utaratibu huu kuna uwezekano wa kutokuwepo kwa ufanisi katika sekta hii muhimu ya afya na pia katika utekelezaji wa miradi husika.

Wizara ya Ustawi wa Jamii

Mhe. Spika, kamati yetu inaipongeza wizara kuweza kutekeleza malengo yake iliyojipangia kwa ufanisi katika vipindi vya kota mbili za mwanzo za Julai hadi Disemba katika utekelezaji wa Bajeti yake

Kamati imeweza kujionea wenyewe yaliyofanywa na wizara pamoja na mipango yake ya baadae ambayo yenye kuleta matumaini kwa maendeleo ya nchi yetu.

KUHUSU WATOTO WANAOISHI KATIKA MAZINGIRA MAGUMU ZAIDI

Mhe. Spika, miongoni mwa mambo yanayochangia kuwepo kwa watoto wanaoishi katika mazingira magumu zaidi ni kukosekana kwa huduma muhimu za kijamii ikiwemo huduma za afya. Kamati itahakikisha inashirikiana na Wizara ya Afya ili huduma za afya ziweze kufikishwa katika maeneo yaliyoathirika kutokana na kutokuwepo kwa huduma hiyo kama eneo la Kinuni.

Kamati imebaini kuwa bado hakuna muamko wa kutosha wa uanzishwaji wa vikundi vya uzalishaji vya kiuchumi katika maeneo yenye watoto wenye mazingira magumu zaidi .Kamati inatoa rai kwa wizara kushirikiana na wizara ya uwezeshaji wananchi kiuchumi kuelimisha kinamama ili waweze kuunda vikundi vya uzalishaji ili viweze kuwasaidia katika kukabiliana na hali ngumu ya maisha katika maeneo yao.

UDHALILISHAJI WA WATOTO KIJINSIA

Mhe. Spika, katika utafiti wa haraka Kamati yetu imeona kuwa taarifa za kutisha za udhalilishaji wa watoto hivi sasa zimepunguwa. Hali hii tunaweza kusema inaashiria pia kupungua kwa vitendo hivyo dhidi ya watoto wetu.Hata hivyo Mhe. Spika, Kamati inaishauri Wizara kwa vile Mhe. Rais wa Zanzibar aliunda Kamati maalum kufuatilia masuala ya udhalilishaji wa watoto ni vyema Kamati hiyo ingeleta ripoti yake mbele ya Baraza lako tukufu ili wananchi waweze kuelewa namna ya serikali yao inavyolifuatilia kwa karibu suala hilo.

USHIRIKIANO NA VYUO VYA MAFUNZO

Mhe. Spika, Kamati inaishauri Wizara kuimarisha ushirikiano na chuo cha mafunzo kwa lengo la kuhakikisha kuwa haki za watoto, wanawake na jamii kwa ujumla zinalindwa kwa kuzingatia misingi ya haki za binaadamu.Ipo haja kuanzisha miradi maalum ambayo itasaidia kutoa huduma muhimu kwa jamii hasa watoto na wanawake katika vyuo hivyo.

Aidha Mhe. Spika,Wizara kwa kushirikiana na Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka ishauri kuendelea kupitiwa sheria zote za makosa ya jinai na madai ili kuondokana na hali iliyopo sasa ya kuwekwa mahabusu watoto, wanawake pamoja na vijana wengi kwa tuhuma za makosa ambayo suluhu yake ingeweza kupatikana katika jamii husika.

Mhe. Spika, Kamati inaipongeza wizara kwa ubunifu wa kuanzisha Mpango maalum wa mikopo kwa vijana kwa kushirikiana na benki wa *CRDB*.Hatua hii imesaidia katika kuvijengea uwezo wa kiuchumi vikundi mbali

mbali vya kiuchumi nchini. Vikundi hivyo vimeweza kuunda *SACOSS* moja ya *Zanzibar vijana Sacoss* itakayotoa mikopo kwa wafanyabiashara na wazalishaji wadogo.

UJENZI WA JENGO LA WIZARA PEMBA

Mhe. Spika, Kamati inaishauri Serikali kuharakisha kuanzisha ujenzi wa jengo la kudumu la afisi za wizara ya Ustawi wa jamii na maendeleo ya wanawake na watoto Pemba ili kuepuka kutumia fedha nyingi kwa ajili ya kuendelea kutumia majengo ya kukodi.

Mhe. Spika, Kamati yetu inaipongeza wizara kuona umuhimu wa kuanzisha kituo cha One Stop Center kilichopo Chake Chake Pemba. Kituo hiki kitasaidia katika kupambana na udhalilishaji wa watoto katika jamii.Kamati inaisisitiza Wizara kuongeza nguvu katika kutoa muamko hasa kisiwani Pemba ili wananchi waweze kukitumia ipasavyo kituo hicho.Nchi jirani zilizoanzisha vituo kama hivi zimeweza kufanikiwa kutokana na kuwepo kwa muamko mkubwa kwa jamii katika kuvitumia vituo hivyo.

Mwisho, Mhe. Spika, Kamati yetu inapenda Serikali ielewe kuwa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi alitamka mbele ya Baraza hili tukufu kutoa vipaumbele katika sekta ya Elimu, Afya na Ustawi wa watu lakini Kamati yetu inaona kuwa hilo bado halijafanyika kwa namna ambavyo serikali imedhamiria.Bado sekta hizo tatu Mhe. Spika, zinakabiliwa na changamoto muhimu ya ufinyu mkubwa wa kibajeti hali ambayo kamati yetu imebaini kuwa imechangiwa na utaratibu unaoendelea wa kuwekewa ceiling kwa bajeti za wizara, ambayo ni dhahiri haiwezi kutoa ufanisi hasa katika utekelezaji wa sekta hizo tatu.Kamati yetu haipingi utaratibu huo, lakini itafikia wakati kwa mazingira tuliyonayo sekta hizo zitashindwa kutoa huduma ipasavyo kwa watu. Kuna haja kwa serikali kuzingatia ceiling inayoitoa kwa ajili ya bajeti za wizara zinazosimamia sekta hizo kwa mustakbali wa maendeleo ya nchi yetu na jamii kwa jumla. Kuendelea kutegemea mchango mkubwa wa kibajeti kutoka kwa wahisani kuna athari zake hasa katika utekelezaji wa malengo katika sekta hizo tatu za kijamii.

Naomba kuwasilisha.

Mhe. Spika, nataka nisisitize tu kwamba muda wetu ni finyu tupange point zetu vizuri tutumie muda mfupi ili tuweze kuanza angalau na kamati nyengine kuwasilisha ripoti yake.

HOJA ZA SERIKALI

Mhe. Suleiman Hemed: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi nakushukuru kwa kuweza kunipatia nafasi kidogo ya kuweza kutoa michango yangu katika kamati hii, mimi nilitaka niseme kwamba katika kamati hii pamoja na kazi kubwa waliyoifanya katika kutupa maelezo mbali mbali, lakini bado kuna mapungufu makubwa ambayo tulitegemea katika kutoa taarifa sisi tuliomo humu ndani ya baraza ili tuweze kupata taarifa ya kutosha na wananchi waweze kupata taarifa hii kutoka kwetu, lakini bahati mbaya mambo yamekwenda kwa ufupi ufupi sana kiasi ambacho tunashindwa kuweza kuchangia sehemu kubwa sana ya sekta hii.
Mhe. Spika, kwanza nataka nizungumzie suala zima ambalo linazungumzwa mara kwa mara ambalo tunaambiwa kwamba kuna suala zima la utanuzi wa Mahospitali Wete, Chake na Mkoani na hapa Zanzibar vile vile, lakini katika kitu ambacho kitogo kinaturudisha nyuma ni suala zima ambalo tunalisikia mara kwa mara juu ya suala la vifo vinavyotokezea vya akina mama wajawazito. Hili suala ni muhimu na kubwa sana na limekuwa linaendelea kwa muda mrefu hivi sasa lakini bado utaratibu wake katika kunusuru maisha ya wazazi bado yamekuwa madogo.

Mhe. Spika, kila siku tunaambiwa kwamba labda kuna ADB wanasaidia, lakini mimi nataka niseme kwamba suala hili kama tunataka tuliweke sawa sawa ili tuweze kupunguza vifo vya wazazi, basi ni wajibu wa wizara ijikite katika mambo Fulani, mimi kwa upande wangu Wizara inakuwa inajikita kila wakati kwa kusema kwamba inaagizia madaktari mabingwa. Kwa nini kila siku sisi iwe tunaagizia madaktari mabingwa kwa nini, mimi nasema Zanzibar ni nchi kama nchi nyengine ni lazima iweze kujitegemea kwa madaktari wake wenyewe sio kila siku kuambiwa kwamba tutaleta madaktari bingwa na ukitizama hii Unguja na Pemba utaikuta sehemu kubwa ya madaktari ni madaktari ambao wanatoka sehemu mbali mbali kuja kutoa misaada kwa nini iwe hivyo.

Lakini mimi nataka nimwambie Mhe. Waziri kwamba ajipange tena zaidi badala ya kutoa wanafunzi wa kupeleka Mbweni hapa kwa kupata taaluma ya udaktari hii bado haijatosheleza kwa hali tunayoitaka, tunataka Zanzibar kama nchi iweze kutoa madaktari wake mwenyewe yaani hawa nakusudia wataalam, hivyo ndio tunavyotaka.

Jambo jengine nataka nieleze juu ya suala zima katikaq upungufu wa hawa madaktari kwamba tuelewe kwamba madaktari ni muhimu kwa njia mbali mbali, daktari huyo huyo mmoja badala ya kuonekana katika hospitali daktari huyo mmoja atakuwa daktari wa magonjwa yote hili sio jambo zuri, ni vyema Zanzibar kama ni nchi tuwe na madaktari ambao tunahakikisha tunao wakutosha kwa ajili ya uperesheni, kwa ajili ya shughuli za wanawake na vile vile tuwe na madaktari wengine ambao wanaweza kutusaidia katika mambo ya ugonjwa tulionao wa maradhi ya kisukari na maradhi ya *obesity*.

Mhe. Spika, tupate madaktari mbali mbali wa kuweza kuchangia madaktari wa pumu, madaktari wa kuweza kuona sehemu za koo, madaktari wa sehemu za kichwa na ugonjwa wa akili sasa hapa linalotendeka Zanzibar ni kwamba daktari mmoja anatembelea sehemu zote za Zanzibar hili sio jambo zuri, kwanza mnamchokesha yule daktari wakati na yeye kama binaadamu anahitaji mapumziko. Kwa hivyo hapa Waziri wetu ajitahidi kutupatia madaktari wa kutosha ili tuweze kujiendesha wenyewe.

Mhe. Spika, jambo jengine nataka niingie katika Wizara ya Elimu mimi niseme tu kwamba kwa taarifa hizi zilizotoka hapa hazikuweza kutosha na zilikuwa kwa muhtasari sana na mimi nilitegemea kwamba labda wizara ya elimu katika kuitolea taarifa zake ungezitolea kwa upana zaidi, lakini wamezikita kita sana. Sasa mimi katika suala la Wizara ya Elimu nataka nizunguzia suala zima la ukaguzi wa walimu, wizara imeandaa wakaguzi zamani ilikuwa kuna wakaguzi wa Wilaya lakini sasa hivi tumeambiwa kwamba itakaporejeshwa tena ukaguzi wa wilaya kwa maana hiyo ukaguzi wa wilaya haupo sasa hivi na wanataka kurejeshwa tena. Ambazo zamani ilikuwa ni jambo zuri kila Wilaya ilikuwa na mkaguzi wake lakini sasa hivi naambiwa inataka kurejeshwa tena ina maana kwamba hawa wakaguzi labda hawapo tena, kwa hivyo atakapokuja katika majumuisho aseme kwamba hilo suala linaendelea au mtindo mpya wa kutafuta wakaguzi wa wilaya.

Vile vile tulikuwa tupate taarifa za kutosha kwamba walimu wanahitaji kujulikana mambo ya ufundishaji na kujifunza katika maskuli yetu hayo ni mambo ya msingi, nataka suala hili inaonekana kwamba taarifa hapa hatukupata za kutosha kwamba wanapopita wakaguzi katika kukagua maskulini angalau tungeweza kujua kwamba wapo kwanza wakaguzi wa kutosha katika maskuli, au mkaguzi huyo wa skuli anatembea kiasi wilaya mbili au tatu na kama wapo wakaguzi wa kutosha basi angalau tungeweza kuambiwa kwamba katika ziara ya wakaguzi wetu tunapata taarifa zote kwamba walimu wanaweka rekodi zao sawa sawa, wanaweka *assessment* zao sawa sawa za wanafunzi, kila kitu kinakwenda kwa mujibu wa vile kilivyopangwa. Lakini taarifa hizi hatukupewa tumenyimwa na sisi tunataka tujue kama kweli katika ukaguzi unaendelea vizuri na walimu wanakaguliwa vizuri na taarifa hizo zinapatikana kwa walimu wote.

Lakini vile vile katika kukagua kuna matatizo ambayo ya mitaala yenyewe inawezekana kwamba katika maskuli yetu kuna upungufu wa *cur glum* hamna za kutosha, au pengine *curglum* zile zimeshachanika kwa muda mrefu na hazijafanyiwa uhamisho wa mitaala ile, kwa hivyo hilo vile vile hatukuekelezwa. Sasa Mhe. Waziri ni juu yako kuhakikisha kwamba suala la mitaala linapatikana na mitaala hiyo inakidhi haja kwamba kila mwalimu anapata mtaala unaohusika na walimu wanaufanyia kazi mtaala, sasa hapa baina ya mkaguzi na mtaala hapa ndio tunataka taarifa tuzipate je mkaguzi ameweza kuona mafanikio ya mitaala ile kwamba mwalimu ameweza kufikisha kiwango kinachotakiwa kwa muda wake, au yuko nyuma ya mtaala au amekwenda mbio sana kwa mujibu wa mtaala ule alionao.

Kwa hivyo hapa Wizara ina kazi kuhakikisha kwamba wakaguzi wake wanatoa ripoti rasmi kuanzia maendeleo ya wanafunzi pamoja na mitaala yao. Pia inahitaji kujua hii mitala katika mafanikio yake wastani wa mitaala hii je mafanikio yamepatikana au hayakupatikana, kwa sababu tunataka tujue kwa kuwa mbele yake mwisho tunataka suala la upimaji na tathmini, sasa kama mitaala hii haikaguliwi walimu wanachokisomesha haya yatakuwa mashaka ya kuona walimu wanafanya wanavyotaka hawapitiwi, mitaala haimalizwi kwa mujibu wa wakati wake, walimu hawaingii sawa sawa madarasani kwa mjuibu wa vipindi vyao hili suala ni muhimu sana walimu kuweza kukaguliwa.

Suala jengine Mhe. Spika, ni kwamba hawa walimu wanahitaji kupatiwa semina na semini ni kitu muhimu sana ku-*refresh* akili zao ku-*refresh* masomo yao lakini utakuta semina wanazotolewa ni za muda mrefu kiasi ambacho mwalimu wa ku-*rast* darasani, kwa hivyo hiyo ni juu ya waziri kuhakikisha tuweze kujua maendeleo ya darasa vile vile tuweze kujua mchanganyiko wa wanafunzi wanawake na wanaume katika darasa maendeleo yao yako je. Hawa watoto wanawake maendeleo yao yako vipi na watoto wanaume maendeleo yao yako vipi.

Mhe. Spika: Jitahidi na muda.

Mhe. Suleiman Hemed Khamis: Ahsante sana Mhe. Spika, jengine ninalotaka kuzungumzia kwamba katika kamati hizi za wazee katika mtihani ambao ulifanywa juzi juzi kidato cha nne, katika suala hili la mtihani huu

wa darasa la kumi na mbili Baraza la Mitihani *NECTA* lilitoa taarifa yake juu ya suala la mitihani Zanzibar. Lakini mimi pamoja na kwamba wao wametoka nataka kujua je Mhe. Waziri ameridhika na kauli ile bila ya kufanya utuafiliaji wa suala hili, sisi Zanzibar ni lazima tuweze kuridhika sio waseme wao tu kwamba wanafunzi hawa wamefutiwa matokeo ya mitihani, lakini je Wizara ya Elimu imeridhia na kauli hiyo.

Kwa sababu maana ya kusema hivyo wao baada ya kumaliza hili suala la kwamba watoto wamekwenda kinyume na utaratibu wa mitihani wamepewa adhabu ya kwamba wamefutiwa matokeo yao na hawatofanya mitihani mpaka baada ya miaka mitatu, hii ni athari kubwa sana kwa watoto wetu. Sasa ndio pale niliposema Je, Wizara ya Elimu hapa kuona hali ni kama hiyo kwa mujibu hizo sheria zao walizozitoa kwamba mwanafunzi atawajibika kubakia nyumbani kwa miaka mitatu na baada ya miaka mitatu ndio atapata nafasi ya kuendelea na mtihani. Hili suala kwanza linahitaji kufanyiwa uchunguzi na utafiti wa kutosha kabla ya wao kutoa na wao kwa kutoa haya matokeo walikutana na Wizara ya Elimu wakazungumza juu ya suala hili na wizara ya elimu ikakubali, lakini sisi tulisikia katika matangazo hali hiyo tuliona kwamba hapa mashirikiano labda yalikuja baadae, lakini awali walitoa matokeo yao kuna kwamba mitihani imekwenda kinyume.

Suala jengine niseme kwamba wazee hawakuridhishwa na suala hili kamati za wazee za skuli hazikuridhishwa na walitaka lazima Wizara ya Elimu watoe jibu rasmi kamati za wazee zinazoshughulika na maendeleo ya wanafunzi pamoja na mitihani hili suala sijui kama limefanyika. Lakini suala jengine ambalo ni muhimu

Mhe. Spika: La mwisho hilo.

Mhe. Suleiman Hemed Khamis: Hewala Mhe. Spika, namaliza ni vitabu mrejeo ambavyo ni *reference* tunahitaji Mheshimiwa tuwe na vitabu vya kutosha katika maskuli yetu ili watoto wetu wasipate tabu, kwa sababu wanahitaji vitabu vya *reference* na *reference* hamna vya kutosha watoto wetu wa vyuo vikuu na watoto wa Form IV na Form III na Form II hawana vitabu vya *reference* kwa hivyo naiomba Wizara suala hili ilishughulikie.

Mhe. Spika, kwa kuheshimu muda wako mimi naona hili suala ni muhimu na mimi naunga mkono maelezo yao ya dhati. Ahsante sana.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Nakushukuru Mhe. Spika, kunipatia nafasi hii na naomba niende moja kwa moja katika ripoti hii kwa kutoa maoni na kuuliza masuali machache.

Mhe. Spika, kiwanza naomba niangalie ukurasa wa 27 wa ripoti ambapo unazungumzia maagizo ya kamati kwa mwaka uliotangulia, buleti ya pili imezungumzia serikali itafute ufumbuzi wa haraka wa tatizo la kukosekana madaktari wa kutosha katika hospitali ya Wete, Chake Chake, Mkoani na vituo vya Afya. Yapo maelezo yaliyotolewa hapa lakini suali langu linahusu mbali ya vituo hivi vile vile kumezungumzwa mara nyingi suala la upungufu wa madaktari hata katika hospitali kuu ya Mnazi Mmoja, hata wakati mwengine katika nyakati za usiku kukosekana madaktari wa zamu ambae huwa anahitajika sana niapotokea dharura sijui katika hili serikali ina majibu gani, ningependa kumsikia Waziri katika suala hili zaidi ya maelezo yaliyopo hapa.

Pili naomba niende ukurasa wa 27 huo huo katika bullet ya tatu pamezungumzwa fedha zinazopatikana kupitia mradi wa ukimwi zionyeshwe katika bajeti ya serikali iliyopitishwa na Mkaguzi Mkuu wa serikali aweze kuzikagua, sasa hili naomba niliunganishe kabisa Mhe. Mwenyekiti na ukurasa wa 33 wa ripoti, ambapo hapa chini kabisa pamzungumzwa kitengo cha ukimwi na pamezungumzwa fedha ambazo zimetengwa ni fedha nyingi tu Mhe. Spika, ambazo zimetajwa pale. Hoja yangu ni kwamba inaonekana kuna malalamiko sana juu ya matumizi mabaya ya fedha zinazokuja kwa ajili ya miradi ya kupambana na ukimwi, iwe katika wizara ya Afya au katola Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais kupitia tume ya ukimwi. Inaonekana kwamba vile fedha hizi zinapokuja zinakuja kwa wingi kutokana na *intrest* za hawa wanaozitoa imekuwa zinaundiwa mambo tu ikiwa yana umuhimu au hayana umuhimu lakini mradi kuna malalamiko kwamba wakubwa wanaohusika na miradi hii wamekuwa wakijinufaisha kutokana na fedha hizi.

Nilikuwa naomba kwa sababu hapa tunajadili Wizara ya Afya kwa hizi ambazo ziko chini ya Wizara ya Afya tuelezwe kwamba kuna nini hapa hata kufika pahala ikawa wanaosimamia miradi hii, hawataki ziwe zinaingizwa katika serikali na zikawa zinakaguliwa na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali wakati ikijulikana fedha yoyote inayoingia katika nchi hata kama inatoka kwa wahisani ikiingia katika nchi imeingia katika hazina ya Zanzibar, ni msaada kwa wananchi wa Zanzibar kupiitia serikali yao nilikuwa naomba maelezo hayo.

Tatu Mhe. Spika, katika Wizara hiyo hiyo ya Afya naomba niende kwenye ukurasa wa 29 hapa pamezungumzwa juu ya hospitali ya wagonjwa wa akili, kwanza nipongeze hatua inayoendelea ya kujenga

hospitali ya wagonjwa wa akili Pemba, kwa sababu kunaonekana kuna tatizo kubwa sana lakini hakuna hospitali ya aina hii.

Kwa hivyo nafurahi kwamba suala hilo linafanyiwa kazi, lakini kadiri linavyofanyiwa kazi katika changamoto nadhani hii inahusu kote kote, Pemba hospitali hii haipo lakini hapa Unguja Kidongo Chekundu ambapo ipo pamezungumzwa hakuna uhakika wa upatikanaji wa dawa muhimu kwa wagonjwa wa akili, sasa tatizo hili linaongezeka kwa kazi limekuwa kama vile katika hospitali hii mpaka watoke wahisani kutoka nje waje wapake rangi na waje wasaidie lakini serikali yenyewe haionekani kwamba inaipa kipaumbele hospitali ya Kidongo Chekundu, sasa kwa nini tunafika hatua hii ya kutokuwa na dawa muhimu kwa wagonjwa wa akili ambao sio wengi ukilinganisha na wagonjwa wengine sasa sidhani kama kunahitajika madawa kiasi kikubwa kiasi hicho. Hapa nilikuwa nataka maelezo kutoka kwa Waziri kuhusiana na suala hili.

Mhe. Spika, naomba niende ukurasa wa 30 ambapo pana mradi wa kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi, hapa niempata wasi wasi tu kwamba fedha za mradi zilizotengwa kwa mwaka 2011/2012 ni Shs. 100, 040,000/= Sasa kutoka SMZ na ADB ni Shs. 227,705,000/= nilikuwa naomba nisaidie kwamba fedha zinazoingizwa kutoka Julai mpaka Disemba inaonekana ni shilingi 30,088,000/= sasa mradi muhimu kama huu ambao unagusa moja kwa moja upunguzaji wa vifo kutokana na uzazi kwa nini serikali haikuona umuhimu na kiasi cha fedha kilichotolewa kikawa ni kiasi kidogo kama hichi ambacho kimetajwa hapa.

Hilo Mhe. Spika, niliunganishe moja kwa moja na lile ambalo limetajwa katika ukurasa wa 37 wa ripoti ya Kamati juu pale kwenye hitimisho kwamba kamati hairidhiki kuwepo kwa mchango mdogo wa fedha za serikali katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo ukilinganisha na makisio yaliyopangwa, iwapo serikali itaendelea na utaratibu huu kuna uwezekano wa kukosekana kwa ufanisi kwa sekta muhimu ya afya.

Kwa sababu Mhe. Spika, kumekuwa na malalamiko mengi kwamba kasma nyingi za vifungu vya maendeleo zilizokuwa hazitolewi vile ambavyo ilipaswa, naomba maelezo na hasa kama nilivyosema kuhusiana na mradi huu muhimu sana wa kupunguza vifo vinavyotokana na uzazi.

Mhe. Spika, naomba katika ukurasa huu wa 30 vile vile nigusie kidogo kuhusu chuo cha taaluma za sayansi za afya kilichopo Mbweni, kuna suala hapa halikuguswa Mhe. Spika, lakini mimi namuomba Waziri hili alitazame kwa karibu sana mwaka jana tulipokuwa tunapitisha bajeti tulizungumzia suala zima la kuwepo kwa kukiukwa kwa taratibu katika kuchagua wanafunzi ambao wanajiunga na chuo hiki, tukasema kwamba kuna dalili kwamba kuna watu ambao wana sifa zaidi ya zilizowekwa na Chuo na wanaachwa na wengine waliokuwa hawana sifa wanapatiwa nafasi.

Mhe. Waziri na Mhe. Naibu waziri wakati ule wakatukatalia kata kata na wakasema kwamba kuna malimbikizo ya muda mrefu huko nyuma yalikuwa yamekaa kutokana na taratibu, lakini sasa mambo safi. Kuna jina moja Mhe. Waziri na Mhe. Naibu Waziri niliwapatia la mtu wa jimbo langu sikupata jawabu kutoka kwao tena, lakini baadae kuna mtu mwengine na naomba nimtaje kwa heshima zote hapa Mhe. Ali Abdalla Suleiman aliwahi kuwa Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Kiongozi alikwenda katika kile chuo akagundua jina lake lina sifa zaidi ya watu waliopitishwa na liliachwa na watendaji wa chuo kile walimuomba alifunike funike yule kijana baadae akaingizwa katika waliokubaliwa.

Sasa naomba hili kwa sababu Mhe. Spika, Mawaziri tunapowaambia hoja mara nyengine wasiwaamini mno watendaji wao wakayakataa tu yale ambayo wawakilishi wa wananchi tutakuwa tunayaeleza, yanapofuatiliwa yanajieleza na yanakuwa na ukweli na matokeo yanakuwa mabaya kwa wale ambao tunawajibu. Kwa sababu sisi tunapotoa hoja hapa tutakwenda kujibu kwa wapiga kura yale majibu ambayo waziri anatupa, lakini yanapofuatiliwa mengine kule yanaonekana ya kweli. Kwa hivyo namuomba Mhe. Waziri chuo hiki wakitizame sana kwamba kisitumike wakubwa waliopo pale kuweza kupitisha watu wasiokuwa na sifa na waliokuwa na sifa wakaachwa.

Mhe. Spika, kuna suala la mapato ambayo yalipaswa yaingizwe na Wizara ya Afya ule ukurasa siukumbuki sasa hivi, lakini ilitajwa kwamba Wizara katika kipindi hiki cha miezi sita imeingiza asilimia 21 tu ya mapato yaliyotegemewa kutoka Wizara ya Afya, nilikuwa naomba ukurasa wa 31 hapa asilimia 21 ni kiwango kidogo sana katika miaezi sita, nilikuwa nataka kujua kuna matatizo gani hata kukawa na upungufu huu.

La mwisho kwa Wizara ya Afya Mhe. Spika, naomba niende kwenye ukurasa wa 33 panapozungumziwa kitengo cha wagonjwa mahututi ICU hapa nataka niseme jambo moja dogo tu, kama ni nasaha kwa serikali. Mwaka jana katika kupitisha bajeti na leo ndio tunapitia ripoti za utekelezaji wa bajeti hapa wajumbe wengi walipiga kelele kuhusu kitengo cha ICU na ahadi ya serikali ilikuwa tusiwe na wasi wasi kwa sababu wachina

wameshakubali kutusaidia kukijenga. Leo tunakaribia kumaliza mwaka wa fedha Mhe. Spika, nilikuwa nawauliza wajumbe wa kamati wanasema suali hili kutoka kwa wachina ni kama vile halipo, kwa hivyo ingelikuwa sio kelele za wajumbe wawakilishi kutoa hizi shilingi milioni mia tano zilizotajwa hapa, milioni 300 kwa kampuni ya *LAB EQUIP LTD* na milioni 200 kwa kampuni *TOLL GASES LIMITED* maana yake suala hili lingekuwa halijashughulikiwa kabisa.

Kwa hivyo nilikuwa naomba tujifunze tu kama kwa upande wa serikali kwamba mambo mengine wanapopigiwa kelele yanayowagusa wananchi basi ni muhimu kuzingatiwa, kwa sababu unapochukua ahadi ya jumla tu kwamba litashughulikiwa halafu ikawa serikali haitengi fedha kutokana na kodi za wananchi za ndani, hasa kwa umuhimu wa ICU halafu ikawa isitekelezwe Mhe. Spika, itakutuletea madhara makubwa, naomba niachia hapo kwa Wizara ya Afya.

Mhe. Spika: Kwa muda mfupi kabisa.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Sasa niende haraka haraka kwa Wizara ya Elimu kwa muda mfupi kabisa, katika Wizara ya elimu nimeshtushwa katika ukurasa wa 45 wa ripoti ya Kamati imesema katika mapendekezo na maoni yao mwisho kwamba, Kamati haikuridhika na utekelezaji wa malengo ya Chuo Kikuu cha Taifa SUZA kutokana na kushindwa kufikia malengo hayo kwa karibu asilimia 70. Nilikuwa nataka kujua Mhe. Spika, kuna tatizo SUZA hata ikawa malengo hayafikiwi kwa asilimia 70, maana yake imefikiwa malengo kwa asilimia 30 tu. *This is very alarming*, nilikuwa naomba Mhe. Waziri hili au serikali kwa ujumla itusaidie, kuna tatizo gani.

Hapo hapo niunganishe na lile ambalo limetajwa kwa mujibu wa taarifa ya Kamati majengo yaliyojengwa Tunguu, majengo mapya ya Chuo hichi yalipaswa yakamilike na yakabidhiwe Serikalini ifikapo mwezi wa Juni mwaka 2012. Nataka kujua je, lengo hili bado linaweza kufikiwa ukilinganisha kwamba tumebakisha miezi michache tu kufikia Juni mwaka 2012.

Mhe. Spika, naomba pia niende kwa haraka haraka katika suala la ukaguzi, hili limetajwa katika ukurasa wa 37 mpaka 38 wa ripoti. Lakini pia limegusiwa katika ukurasa wa 45 kwenye majumuisho ya Kamati. Hapa naomba kutoa wito inaonekana bado tuna tatizo *serious* katika ukaguzi wa elimu. Katika mjadala uliopita hapa wa Mswada ambao hatimae umepelekea kuunda Baraza la Mitihani la Zanzibar, tulipendekeza baadhi yetu kwamba imefika wakati serikali ianzishe rasmi Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Elimu Zanzibar, waingereza wanamwita *(chief inspector of schools)* na iletewe sheria yake katika Baraza ili ofisi iwe *establish official* na ipewe kazi ya kusimamia elimu kwa ujumla wake. Nilikuwa naomba hilo Mhe. Waziri alitizame.

Mhe. Spika, mwisho kabisa naomba nigusie kidogo katika ukurasa wa 40 wa Kamati ya ripoti pametajwa hapa katika jumla ya skuli ambazo zinafanyiwa matengenezo, zimetajwa skuli za Fidel- kasro, Utaani, Forodhani na Tumekuja. Napongeza skuli mbili zipo katika jimbo langu, lakini nilikuwa naomba kupata maelezo kutoka kwa Waziri.

Mhe. Spika, Skuli ya Forodhani ndani yake kumegeuzwa hoteli nilikuwa naomba kupatiwa maelezo lile eneo la skuli ambalo limegeuzwa hoteli sasa, kwamba serikali ndio imeridhika kwamba skuli ile ya kihistoria moja katika skuli za mwanzo kabisa kuanzishwa Zanzibar, haina haja nazo tena sasa imefika pahala kwamba zinageuzwa hoteli kama ilivyokuwa majengo mengine ya serikali. Naomba maelezo Mhe. Spika.

Baada ya hayo niseme naishukuru na naipongeza Kamati kwa kazi nzuri, nategemea nitapata maelezo ya kuridhisha juu ya hoja ambazo nimezitoa. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante Mhe. Spika, na mimi kuweza kunipa nafasi hii ya leo kuweza kuchangia ripoti ya wanakamati. Kwanza nawashukuru sana wana kamati ambao jioni ya leo ikiongozwa na Mhe. Profesa Hija kwa kutoa ripoti yake nzuri sana yenye ufafanuzi wa kina na kuona hali halisi ya utendaji wa kazi wa Kamati hii.

Mhe. Spika, mimi sitaki kwenda mbali kabisa, katika kitabu hichi hasa katika mambo ya afya kuna mambo ambayo muhimu sana humu mimi sikupata kuyaona ningeweza kuwa na nguvu sana kuchangia, lakini hata hivyo nitumie nafasi hii ya kuweza kupenyeza hapo hapo.

Mhe. Spika, humu sijaona *department* ya kwanza ya kitengo cha wagonjwa wa Sukari, humu hamna na hili ni tatizo kubwa sana katika Wizara yetu, kitengo hiki mara nyingi sana kinakuwa kinapuuzwa. Nimejaribu humu kuangalia sana na kwa kweli kitengo hichi ni muhimu sana. Tatizo hili mara nyingi sana watu wa kitengo kama hichi huwa wanapuuzwa kusema la ukweli, hawapewi haki kana wanavyopewa vitengo vyengine ambavyo

wanatiliwa fedha na Waziri akapata kufaidika. Hili Mhe. Waziri naomba ulione kwa makusudi na wao wana haki wagonjwa hawa wa sukari kuweza kupewa kipaumbele katika mambo yanayostahiki. Hata kwenye ripoti wamesahaulika ni kitu kimoja ambacho kimenisikitisha.

Mhe. Spika, pili kwenye *department* ya chumba cha kufanyia upasuaji (*Operation*), humu namo pia sijaona kitengo hicho. Ukweli kwamba chumba cha kufanyia upasuaji cha Zanzibar hakistahili, kina ukosefu wa zana nyingi sana, chumba hicho tunategemea kuwa hii ni hospitali yetu ya Rufaa, lakini hasa ukiangalia vyumba vyenyewe tumevidharu sana havina vyombo vya kisasa, hata ile hali yake ya hewa ya ubaridi mle ndani kwa kweli ipo pungufu sana. Ukiangalia sasa hivi hata zile nguo sijui kama wamebadilishiwa, walikuwa wakivaa nguo mbovu, kama umefanya mabadiliko hayo nakupongeza sana kwa kuzisikiliza kauli zetu na kuweza kuzitekeleza.

Mhe. Spika, vile vile tuseme ukweli haki *lilahi taala* wataalamu wetu ndio maana kila siku ukicha wanapungua kutokana na mishahara midogo. Hili tulikubali na wala tusilipinge, tunawapa fedha kidogo sana wataalamu wetu. Yupo mwenyewe Mhe. Haji Omar Kheri lakini hili alione. Kusema ukweli hatujawatendea haki madokta wetu, tutahangaika tutakwenda tukirudi mambo yapo pale pale. Hebu tuamue hasa, serikali iwe *serious* kuwaangalia hawa wataalamu wetu, ili na sisi angalau tuwe na wataalamu hapa kwetu Zanzibar ambao tunaweza tukajiringia wenyewe wa asilia Zanzibar hapa. Lakini tunakwenda kutafuta wataalamu wa nje hatimae mtashindwa hata kuwalipa watarudi bila ya mafanikio yoyote.

Vile vile *department* nyengine ambayo ni muhimu sana ambayo na wao hatukuwatia kabisa humu kwenye ripoti ni sehemu ya *X-rays.* Na wao wale ilipasa na wao kuwaingiza kwa sababu mle mashine nyengine ni za kizamani nalo hilo hatujaliona. Kwa bahati nzuri ukienda katika sehemu ya *Utra- sound* pale kuna mashine sijui kama imeshatafutiwa kioo ilikuwa ya zamani sana imekaa bila ya kutafutiwa kioo. Mimi ningeomba hiyo nayo tuweze kuwatafutia haraka haraka kuweza kuwapatia.

Mhe. Spika, tuende katika majengo ya wagonjwa wa akili ukurasa wa 28. Mle ndani kunakuwa kuna sehemu za sero, sijui zile sero sasa hivi mmeshazitengeneza ili kwa wale wagonjwa waliokuwa wakaidi kuweza kuwahifadhi wasiweze kuwadhuru wenzao. Hili nalo nimeliona halijaingizwa kama kweli hicho kitu kipo na kimeshafanyiwa ukarabati ili kuweza kuwasaidia wale wagonjwa, mara nyingi sana tunakuwa tunazisahau.

Ukurasa wa 33 mwenzangu amezungumzia suala la *ICU,* kwa kusema la ukweli pamoja na kauli yako kwenye Bajeti, lakini bado kuna mashine zile ambazo mimi nimezisahau kuzitaja. Mashine zile ambazo zilikuwa zamani kuna kibanda au kisehemu ambacho mtu hana muda wa ku- *reading* wakati wote isipokuwa zile mashine ndio zinamfanya pale ajue mgonjwa wa kitanda namba fulani *temperature* yake ikoje na iko vipi. Mashine zile Mheshimiwa zimekufa zamani sana, na mpaka leo serikali haijaona umuhimu wake wa mashine zile. Naomba sana Mhe. Waziri hili suala tuweze kulifanyia haraka haraka.

Mhe. Spika, kwa kumalizia na huku twende kwenye malaria. Hivi karibuni tulisikia maneno kwamba vyandarua vimeua, hebu leo Mhe. Waziri tupe ufasaha wako hasa ili wananchi wajue ukweli halisi. Kwa sababu kule kwangu tulivifua debe zima baada ya kusikia vinaua tukaona bora tuvikoshe, lakini kumbe tunaiua ile dawa yenyewe kwa kutojua na kuona kwamba tunachukua tahadhari ya kuwa tusiendelee kuwaua watu wengine. Naomba Mheshimiwa utueleze jinsi gani hii hali halisi ya kwamba ni kweli au uongo, ili wananchi waweze kujua kama ni kweli au ni mtu tu alivumisha kwa matakwa yake mwenyewe tu, hilo ni moja.

Katika ukurasa wa 37, hitimisho langu mimi ya huu ukurasa huu nikubaliane nalo kuwa fedha zinazoingizwa katika Wizara yako ni ndogo sana, na sijui kwa sababu gani serikali wizara hii inatoa fedha pungufu wakati wizara hii ni yenye uokozi kwa jamii katika kisiwa chetu cha Zanzibar. Vile vile kuna fedha ambazo nyinyi wenyewe mna miradi yenu pale maalum kwa nini Wizara ya Fedha wasiziache zile pesa kukuachieni nyinyi wenyewe ili mkaweza kukimu masuala madogo madogo pale. Kwa mfano zikisha zile filamu muweze kununua wenyewe na mambo mengine madogo madogo. Hebu Wizara ya Fedha msione choyo na hizi fedha hebu ziacheni. Waachieni hawa wenyewe wajihudumie wenyewe. Hata hizi pesa kidogo kidogo nazo pia mnazitaka za kuchangia? Hebu tuwapeni jamani mambo mengine sheria na huruma. Tuwape wenyewe pesa zao Babu Juma Duni alete maendeleo pale kwenye Wizara, hebu tuziacheni tumuachie mwenyewe. Lakini hizi nazo utasikia zinakwenda kwenye mfuko wa serikali, heeh! Jamani hebu tuziache.

Mhe. Spika, vile vile tukubaliane pia kuna wafanyakazi wengine katika hiyo nyongeza ya juzi. Juzi alisema pale Mheshimiwa wangu Haji Omar Kheri yeye hakubaliani na suala hilo na hajasikia. Wapo Wizara ya Afya hawajapata nyongeza ya Fedha. Hao wapo kabisa na ushahidi tosha na ukitaka nikuletee hata *Rover* nzima mimi nipo tayari kukuletea, uwaone hao watu, bado hawajanufaika na Mswada huu. Naomba sana hao watu wapo

sehemu za ufundi na sehemu nyengine. Hao watu hawajaongezwa na hawajanufaika katika hii nyongeza ya asilimia 25.

Mhe. Spika, vile vile kwa kumalizia hapa hapa niseme kwamba kuna mfanyakazi siku zote mimi huwa nasema wa Wizara ya Afya, hebu jamani tumuhurumieni huyu mtu. Tulimsimamisha kwa kuwa na wasi wasi wa jambo, lakini baadae ameshinda kunako kesi. Mhe. Spika, hebu tumrudishieni haki zake, tumuhurumieni yule jamani ana watoto na familia. Serikali jamani wanakuwa wanatoa maneno ya jazba inawezekana mtu akatamka neno lilokuwa si zuri, lakini ukimkuta upande mwengine ana haki ya kusema hivyo kwa mujibu wa sheria kwani anadai haki yake. Babu Juma Duni nakuona Waziri wangu mahiri kabisa, tumsaidie huyu hatuwezi kumrudisha kazini, sawa, basi tumpe haki zake. Hii Mahakama si tumeiunda wenyewe kwa mujibu wa sheria, sasa kashinda kwa mujibu wa sheria kwa hivyo tunaomba kabisa, jamani watu wa Wizarani tumpe haki zake Mwenyezi Mungu asije akatupiga radi, tumpeni pesa zake huyu mtu.

Mwisho Mhe. Spika, Wizara ya Elimu nawashukuru sana. Wizara ya Elimu naisifu sana na nimkaribishe Waziri mpya na yeye nimpe hongera sana kapewa kijiti na Mhe. Waziri Ramadhan Abdalla Shaaban, tumenufaika sana katika majimbo yetu yote ya Zanzibar, hii kwa kweli hakuna sehemu Wizara hii wametia mkono wao wa kuyamaliza majengo ya skuli kwa wale waliojenga skuli. Nawapongeza sana kwa jitihada hizi na Waziri mpya Mwenyezi Mungu amjaalie naye afuate nyayo zile zile ili kuweza kupata neema. Mhe. Spika, ahsante sana naunga mkono.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando): Nakushukuru Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi hii na nitajitahidi nichukue muda mdogo sana kama maombi yako yalivyo. Kwanza nianze kumshukuru Mhe. Makamo Mwenyekiti wa Kamati hii ambaye ametusomea hotuba yake kwa niaba ya Mwenyekiti wake pamoja na wajumbe wake wote.

Mhe. Spika, mimi nimejaribu kuyafupisha fupisha baada ya kuona muda nao unatuhimiza tuende kwa muda mdogo, kwa hiyo nitakwenda kwa njia kama ya maswali kidogo tu ili nimalize kwa haraka haraka zaidi.

Nianze na Wizara ya Elimu, kulikuwa kuna tatizo la wanafunzi ambao walifanya mtihani mwaka 2008 wakawa hawakufaulu wakaingia kwenye *private*, mwaka 2009/2010 *credit* zikawa hazikutosha lakini mwaka 2011 wakafanya mtihani ule wakawa wamefaulu vizuri kujiunga na *form five*, lakini bahati mbaya serikali haikuwachukuwa wanafunzi hawa sijui kwa nini labda Mhe. Waziri anaweza akatusaidia hapa akatupa maelezo. Kwani kuna malalamiko mengi ya wanafunzi wa aina hii, kwamba wamechukuliwa wa mwaka jana ile miaka ya nyuma wote wameachwa.

Vile vile kulikuwa kuna suala la *scheme of service* ya wafanyakazi wa Mamlaka ya Mafunzo ya Amali, ambayo ilifanyiwa marekebisho kwenye mwaka 2009 na mishahara ile ikaanza kuingia kwenye mwaka 2010 mwezi wa Julai. Lakini tangu kipindi hicho ambacho marekebisho yale yamefanywa, nyongeza ile hawajaipata lakini ukiangalia Wizara ya Fedha kule fedha zile zinaingizwa katika bajeti ya matumizi ya ile nyongeza mpya, lakini wao wafanyakazi hawajaanza kuipata mpaka hii leo.

Nilikuwa nataka kujua sijui kwa nini. Kwa sababu ukipiga hesabu ya haraka haraka kuna deni karibu shilingi milioni 800 ambazo wanadai wafanyakazi wale kama ni malimbikizo. Nilikuwa nataka kujua fedha hizi kama hawajalipwa zinakwenda wapi na zinatumika kwa ajili gani.

Nisogee mbele kidogo kwenye mambo ya *NECTA*. Hawa jamaa zetu kuna taarifa kuwa baadhi ya wanafunzi wa masomo ya *arts* wamepata matokeo yameletwa kwao ya sayansi, na kuna baadhi ya wanafunzi wa sayansi yamekuja matokeo ya *arts*. Labda hili sijui limechangiwa na nini, na kama ni kweli maana ni taarifa tu hizo lakini sina uhakika nazo vizuri. Sasa Mhe. Waziri atatusaidia labda kwake yeye atakuwa amepata mambo kwa uhakika kabisa.

Mhe. Spika, jengine nilikuwa nataka kujua kwenye zile Skuli za Sekondari zinazojengwa za kila Wilaya. Kwa mfano kama kule kwetu kwenye Wilaya “A” zimejengwa Sekondari mbili kuna moja ipo Matemwe kabisa na moja ipo hapa Chaani.

Sasa ukitizama skuli zile utakuta kwa pale ilipojengwa kama ile ya Matemwe mimi nina wasi wasi wa kupata wanafunzi, kwa sababu Matemwe yenyewe iko kiasi lakini skuli itahitaji wanafunzi wengi zaidi. Kwa eneo ambalo imejengwa hakuna *bording* pale. Juzi kulikuwa kuna swali tulipokuwa tunachangia mambo ya elimu haya, tuliligusa hili swali lakini sikupata jawabu nzuri pale kwa Mhe. Naibu Waziri.

Sasa sijui Mhe. Waziri mpya utatusaidiaje, kwa hivyo nafikiri atakapokuja atatusaidia ni utaratibu gani utakaotumika pale au ukiangalia walimu ambao watasomesha pale, lakini na wanafunzi ambao watasoma pale. Kwa mfano mtu atoke Nungwi aje Matemwe mtoto wa kimasikini hiyo nauli ya kila siku ni karibu sh. 1000 kuja na sh. 1000 kurudi, maana apande gari mbili mpaka afike pale. Nafikiria lile lengo ambalo limekusudiwa katika ujenzi wa kuli zile litakuwa halipatikani. Ndio pale wataalamu wa mambo ya PAC wanasema *value for money* haipo pale. Mmejenga skuli nzuri tu lakini matokeo yake elimu ambayo iliyokuwa inatakiwa itolewe kwa watu wetu pale haitopatikana, kwa sababu watu wa kuwapa ile elimu watakuwa hawapo.

Jengine hili liliguswa sana na mtoa hoja Mhe. Hamza kipindi kile, aliulizia sana kuhusu fedha zile karibu milioni 800 za wale wanafunzi ambao walikopeshwa hazijakusanywa, akatoa na rai Mhe. Hamza kwa nini basi tusipeleke Kamati ya Uchunguzi ili iende ikachunguze fedha zile ili iweze kumsaidia Mhe. Waziri. Hebu leo Mhe. Waziri ukija tueleze unasemaje ili tuipeleke *PAC* ikafanye kazi ile. Hilo nilikuwa namalizia kwenye Wizara ya Elimu.

Mhe. Spika, niende kwenye Wizara ya Wanawake na Watoto. Mimi hapa nina maswali mawili. Swali langu la kwanza linahusiana na kwamba, pamoja na kujenga yale magereza kwa ajili ya watoto. Nimewahi kutembelea magereza ya hapa nikakuta kuna watoto kwenye gereza lile la watu wazima. Kwa kweli wamejiinamia vibaya, maana wale watoto ni wadogo lakini lile gereza kuna *mibaba* na unajua kuna *mijitu* mikubwa kweli kweli, ile mibabe ya huku mjini kote na huko vijijini ikikamatwa inapelekwa kule. Lakini nimeyakuta wamechanganywa pale na wale watoto na mijitu mizima katika muda wa mchana. Sijui usiku maana mimi nimepelekwa mchana, lakini kwa kweli nilipatwa na huzuni sana. Watoto wale wakiwatizama tu wababe wale wanaanza kulia tangu mda ule mpaka wanalala jioni. Mhe. Waziri hebu ukija utwambie uko wapi katika kujenga magereza kwa ajili ya hawa watoto. Mahakama nafikiri iko mbioni kuzianzisha, je kujenga magereza kwa ajili ya hawa watoto, nataka nije nipate taarifa yake.

Mhe. Spika, halafu nilikuwa nataka niulizie suala moja la skauti. Najua tulikuwa tunayo skauti hapa Zanzibar na ndio waanzilishi hasa sisi wa skauti, lakini imekufa. Hebu Mhe. Waziri una mkakati gani katika wizara yako katika kulianzisha suala hili. Naomba hayo Mhe. Spika, naunga mkono hoja.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, nakushukuru kunipa nafasi hii na mimi nichukue muda mfupi kama ulivyonieleza, nitajitahidi.

Mhe. Spika, mimi nataka nimshukuru sana Makamo Mwenyekiti wa Kamati kwa kuleta ripoti yake hii, ambayo kwa kweli inajitosheleza lakini na sisi tumeona iko haja ya kuitia tia nyama ili Mhe. Waziri aje apate mambo mengi ya kuweza kuyafanyia kazi kabla ya kuja kutusomea hotuba yake ya bajeti katika kikao kinachokuja.

Mhe. Spika, mimi nataka nianze moja kwa moja na Wizara ya Elimu zaidi katika hivi vyuo vya Amali. Mimi nataka nizungumze katika Chuo cha Amali kilichopo Mkokotoni. Kulikuwa kuna malalamiko ya Wazazi wa wanafunzi ambao waliwapeleka pale kwa ajili ya kupata taaluma nadhani kama sikosei nadhani katika mafunzo, nadhani ya Hoteli na Utalii. Tumepata taarifa kwamba chuo kile kimekodishwa, au baadhi ya majengo yamekodishwa kwa watu binafsi kwa ajili ya kutoa hiyo taaluma, lakini baadae wanafunzi wale wameshasoma, baada ya kwenda kutafuta kazi au baada ya kupata elimu ya juu zaidi wakaambiwa vyeti vile havitambuliki kisheria.

Kimsingi kwa ukweli vyuo hivi tulivijenga au serikali yetu ilivijenga kwa makusudi ili kuwapatia vijana wetu taaluma. Lakini leo kijana ameshasoma mwaka mmoja ana cheti chake anakuja kuambiwa cheti kile hakitambuliwi. Hili sijui Mhe. Waziri analielewa vipi, na kuna hatua gani za kisheria zitaweza kuchukuliwa kwa hawa waliohusika. Kwa sababu unapokikabidhi chuo kukikodisha, halafu vyeti vyake au certificate zake zinakuwa hazitambuliki. Kulikuwa hakuna vigezo ambavyo vya kuweza kuvikabidhi hicho huo? Nilikuwa naomba hili Mhe. Waziri ajaribu kutafuta taarifa aje kutuelimisha vizuri.

Lakini vile vile nataka nije katika suala zima la wanafunzi wasioona. Mhe. Spika, sasa hivi tunashukuru sana Wizara yetu ya Elimu kwa kusomesha elimu mjumuisho. Kwa kweli tunapokuwa katika ziara za kamati, kwa sababu mimi kamati yangu inashughulikia watu wenye ulemavu. Kuna tatizo kubwa kwa wanafunzi wasioona wanakosa zile mashine za kuweza kusomea, na wengine hivi sasa hivi wanajiandaa kufanya mitihani pengine ya darasa la 7 au form II.

Mhe. Spika, hili nilikuwa namuomba sana Mhe. Waziri katika bajeti yake mwaka huu atenge fedha za kuweza kununulia hivi vifaa. Ukizingatia kwanza wanafunzi wenyewe sio wengi wa kuweza kuikwaza Wizara ya Elimu kuweza kuwapatia vijana wetu hawa vifaa vya kuweza kusomea ambavyo vitakuja kuwasaidia zaidi katika

kujitafutia ajira za kujitegemea, kwa sababu unajua mtu asiyeona tofauti na yule ambaye mwenye kuona. Mwenye kuona anaweza akahangaika hapa kwenda kutafuta ajira kwenye sehemu nyengine, lakini kwa asiyeona tunahitaji tumuandalie mazingira mazuri ili akishamaliza tu masomo basi ile ajira iweze kuwa karibu na mikono yake.

Mhe. Spika, nije katika suala zima la watoto waliokuwepo vyuo vya mafunzo au magerezani, nadhani iko haja kwa hivi sasa kuwekwa magereza ya watoto au Vyuo vya Mafunzo vya watoto vitenganishwe na vile vya watu wazima. Ingawa kuna jawabu tuliwahi kuambiwa kwamba mfungwa ni mfungwa tu au mwanafunzi ni mwanafunzi. Lakini pamoja na hayo, hivi sasa wenzetu tumejifunza tulivyokwenda nchini Kenya mimi na Kamati tukiwa pamoja na wewe. Katika jimbo la Naivasha kule tulikuta wamejenga jela ya watoto lakini wale watoto wanasomeshwa. Ina maana watoto kule gerezani sio kwamba wakitoka walikuwa wanatumikia adhabu tu, lakini wanaendelea kusomeshwa na pengine wakija kutoka wanaweza kujiendeleza na masomo yao zaidi.

Mhe. Spika, wenzetu Tanzania Bara kuna jambo ambalo tumejifunza. Kuna wafungwa kule watu wazima, wanasoma na wanafanya mitihani na wanachukua shahada zao kule kule magerezani. Sasa nadhani wakati umefika kwa Zanzibar kuwa na Magereza au Vyuo vya Mafunzo vya watoto, lakini vile vile kule waweze kupatiwa elimu na ndio maana hapa kwetu Zanzibar hatuiti magereza tunaita Vyuo vya Mafunzo.

Mhe. Spika, nilikuwa namuomba sana Mhe. Waziri ajaribu kuwasiliana na Mkuu wa JKU, kwa sababu pale wenzetu wana eneo lao wamechora ramani nzuri kwa ajili ya ujenzi wa skuli ya sekondari. Tunamuomba Mhe. Waziri wa Elimu anapopata wahisani katika kuomba misaada elimu ya sekondari, basi angalau ajaribu kuwatupia jicho la huruma na wenzetu wa JKU, ili na wao ile skuli yao iweze kupata ule msaada. Kwa sababu kwa bajeti tu wanayopatiwa JKU hawatakuwa na uwezo wa kujenga skuli ile ya Sekondari. Lakini wana ramani nzuri na wana eneo kubwa ambalo Mhe. Waziri wa Elimu inaweza kumsaidia kuweza kuongeza nguvu pale.

Mhe. Spika, nilikuwa nataka nimpunguzie majibu Mhe. Waziri, sio serikali lakini nataka nimpunguzie majibu hasa suala la Mhe. Mtando kuhusu suala la zile fedha bilioni 8 na za elimu ya juu, na wale wanafunzi, tuna taarifa kwamba fedha zile walipewa wanafunzi ambao hawakuwa na sifa au hawakustahili. Hili Mhe. Waziri ninavyokumbuka ukiangalia katika *hansard* alikwisha kulijibu, yeye alisema hana pingamizi.

Kwa hiyo ina maana suala hili Mhe. Mtando labda ungelimuuliza Mhe. Spika, kwa sababu sasa hivi muongozo ulibakia kwa Spika, lakini Mhe. Waziri nafikiri atakapokuja kujibu hili alikuwa keshalitolea maelezo kwamba hana matatizo, wacha likachunguzwe na taarifa itakayoletwa yeye ataifanyia kazi. Hili tu nilikuwa najaribu kumpunguzia majibu swahibu wangu Mhe. Ali Juma Shamuhuna Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali.

Mhe. Spika, nataka nimalizie katika suala zima la mitihani ya kidatu cha nne. Tulipokuwa tukichangia Mswada uliopita wengine tulijaribu kushauri kwamba hii mitihani ya kidatu cha nne sasa hivi ni vizuri ikaweza kutungwa Zanzibar. Hili tumelishauri sio kwa jambo jengine lolote, tunajaribu kuangalia sera.

Mhe. Spika, sasa hivi Sera yetu ni kuanzia skuli ya chekechea mpaka kidatu cha nne hiyo ndiyo elimu ya lazima. Je, bado iko haja ya kwamba masuala mazima ya ile elimu ya lazima tukatungiwe mitihani kutoka upande wa pili wa muungano. Mhe. Waziri hili najua sasa hivi kwamba mitihani hii inatungwa Bara kwa taratibu tulizozizoea, lakini kipindi kile elimu ya lazima ilikuwa inamalizia kidatu cha pili. Lakini sasa hivi kwa mujibu wa Sera yetu ya Elimu, elimu ya lazima inamalizia kidatu cha nne.

Mhe. Spika, hili mimi nadhani bado tunao walimu wazuri, watungaji wazuri wa mitihani, tuna ma-profesa wazuri wanaweza wakaifanya hii kazi na elimu ya juu ikabaki kama tafsiri inavyosema kwamba elimu ya juu ni zaidi ya kuanzia viwango vya kidatu cha sita na kuendelea.

Mhe. Spika, vile vile katika masuala ya vijana wetu waliofutiwa mitihani bado tunaendelea kumuomba sana Mhe. Waziri ile adhabu iliyotolewa na NECTA kwa kweli ni kubwa sana. Vijana wetu mpaka sasa hivi hatujapata jawabu ni muda gani ambao watakaoruhusiwa kuja kurejea tena ile mitihani yao.

Hili nalizungumza kwa sababu tuna uzoefu Bara, safari hii wanafunzi waliopasi darasa la saba ni karibu 5000 sina uhakika kama sio 5000 itakuwa ni 500 hawajui kusoma na kuandika, tena mitihani hiyo wamefanya Bara na wamepasi kutoka darasa la saba kuingia kidatu cha kwanza, hawajui kusoma na kuandika. Hili ni suala la kuliangalia hasa katika suala zima la uvujaji wa mitihani.

Leo sisi huku watoto wetu wameadhibiwa lakini kule Bara utakuta wanafunzi karibu 500 hawajui kusoma na kuandika, na sijui adhabu gani itachukuliwa kwa wale walimu ambao wamesimamia mitihani yao lakini vile vile waliowapasisha wale wanafunzi.

Mhe. Spika, kwa kumalizia kabisa nataka nimalizie kutoa pongezi sana kwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, kwa kuweza kukamilisha ile ahadi ya ujenzi wa skuli ya Sekondari na kwa kuwa jimbo langu la Kwamtipura moja katika jimbo lililobahatika na kupata mradi huu wa skuli ya sekondari pamoja na wenzangu wa Kiembesamaki na Mpendae. Mhe. Spika, tunamshukuru sana Mhe. Waziri, lakini kitu ambacho tunachokiomba ni kwamba wizara iwe karibu sana na wale wakandarasi.

Mhe. Spika, kwa nini nikasema hivyo? Kwa sababu tuna uzoefu wa ma-*consultant* na tulivyojaribu kuangalia wale *consultant* waliopata kazi ya kusimamia hizi kazi za ujenzi wa sekondari hapa Zanzibar, ni kwamba *consultant* wale Mhe. Spika, wanatoka Bara. Mhe. Spika, ni kwamba tuna uzoefu wa ujenzi wa jengo la Wizara ya Fedha Pemba na wao wametoka Bara matokeo yake hawana muda wa kusimamia yale majengo, ni kwamba wakandarasi wanaachiwa muda mrefu wanafanya wanavyotaka wao ndio majengo yanakosa ubora.

Kwa hivyo, tunaomba sana Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali ajitahidi sana kua karibu na ujenzi wa skuli hizi tatu zilizobakia, zile za mwanzo hatukujua usimamizi wake ulikua vipi. Lakini kwa kweli hatutopendelea kuja kupata majengo ambayo hayana ubora. Baada ya hayo machache Mhe. Spika, mimi nilikua na wazo la mwisho katika ile Skuli ya Sekondari ya Matemwe, nadhani skuli ile ingelifanywa ya *boarding*.

Mhe. Spika, ni kweli katika mazingira iliyopo skuli ile ni pahala pazuri sana lakini ukiangalia mazingira na jiografia ya maeneo ya Matemwe na Mkwajuni na sehemu nyengine kwa kweli ile skuli ingelibadilishwa maudhui ikawa ni ya *boarding* ambayo itaweza kukidhi hasa yale mahitaji yaliyojengewa skuli ile. Mhe. Spika, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kwamtipura naunga mkono ripoti ya kamati kwa asilimia mia moja, nakushukuru sana Mhe. Spika.

Mhe. Ali Abdalla Ali: Ahsante Mhe. Spika, na mimi kwa kunipa nafasi ya kuchangia ripoti hii ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii. Kwanza nimpongeze Makamo Mwenyekiti kwa kuwasilisha vizuri ripoti pamoja na wajumbe wake wote ambao wameandika ripoti kiutaalamu sana.

Mhe. Spika, mimi nilikua na michango michache tu na naanza na Wizara ya Afya. Mhe. Spika, katika ripoti kuna eneo limeeleza kwamba chuo chetu cha afya ni kidogo na ndio sababu ya kuweza kushindwa kuchukua wanafunzi wa kutosha. Mhe. Spika, tatizo hili linajirejea katika ripoti hii kwa mara ya pili, mimi nilikua naomba nimuulize Mhe. Waziri kwa kua tayari suala limeonekana tatizo lipo. Je, kama wizara na serikali inachukua hatua gani kuliondosha tatizo hilo?

Mhe. Spika, suala la pili kuhusu chuo kulikua kuna madaktari wetu wanasomeshwa walianza kusomeshwa hapa tukasikia mwisho watamalizia Cuba. Nilitaka kujua je, madaktari wale wameshamaliza muda wao na kama wamemaliza wamepangiwa katika vituo gani?

Mhe. Spika, nikiendelea kwenye Wizara ya Afya nije kwenye Hospitali yetu ya Rufaa ya Mnazi Mmoja. Mhe. Spika, tunashukuru na tunapongeza waziri na watendaji wake wote kwa jitihada kubwa wanazozichukua katika kuendeleza hospitali yetu. Lakini bado kuna changamoto zinawakabili na bado zinataka zifanyiwe kazi na wizara pamoja na serikali. Changamoto moja iko sehemu ambazo wanaingia wagonjwa, kule wagonjwa wanaingia saa zote, mimi hivi karibuni jirani yangu aliumwa ghafla saa nane za usiku nikatoa msaada wa kumpeleka, basi akapokewa halafu akachunguzwa, lakini ikabidi alazwe. Mhe. Spika, tatizo lilokuwepo kwamba wakati mwingi ma-*orderly* wanakua wanawake, sasa unaambiwa mpeleke mgonjwa ghorofa ya tatu. Kwa hivyo, siku hiyo nilibeba mimi mgonjwa mpaka juu, mimi nasema na hilo litizamwe kwa kuweza kuondosha tatizo kama hilo lisitokee. Mhe. Spika, wakati wa usiku ukimuweka *orderly* mwanamke pale inakua tabu kupeleka wagonjwa juu wakati *lift* ni mbovu. Mhe. Spika, tungeshauri wangekuwepo watu maalum ambao ikitokea kesi kama hiyo wakasaidia kupeleka wagonjwa juu.

Mhe. Spika, jengine katika Hospitali yetu ya Mnazi Mmoja pana tatizo ambalo juzi lilizungumzwa katika Baraza juu ya suala la taka za hatari zilizopo pale na *machine* yetu ya kuchomea ni mbovu. Kwa hivyo, tungeishauri serikali ikatwambia kwa dharura inachukua hatua gani kuondosha tatizo hili.

Mhe. Spika, pia suala jengine ambalo linaleta matatizo sana ni sehemu yetu ya *mortuary* kwani ni ndogo na muda mwingi tunazungumza suala hilo, lakini kwenye taarifa sikuona lolote. Kwa hivyo, naomba kuiuliza wizara ina utaratibu gani wa kuweza kuongeza kwa sababu tukiwa na watu wawili waliofariki pale inakua

hapatoshi tena. Mhe. Spika, naomba na hili pia kama kuna maelezo labda ya utaratibu wa kuweza kusaidia basi wangetueleza.

Mhe. Spika, nikitoka kwenye Wizara ya Afya sasa nije kwenye Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali. Mhe. Spika, hapa niungane na wenzangu katika masuala mengi ambayo wameyaona, lakini zaidi yamezungumzwa kwenye *private*. Mhe. Spika, hivi sasa wanafunzi wetu wengi wanafeli mitihani ya kidato cha nne kwenda kidato cha tano. Lakini wenye wazee wao wenye uwezo wanawasaidia kuwanunulia mitihani, na wanafunzi wale wanapata sifa kwenda kidato cha tano. Lakini bado wanabaki mitaani na wizara haichukui jitihada ya kuweza kuwasaidia. Kwa hivyo, naomba je wanafunzi kama wale kama tunao huko mitaani tuwasilishe wizarani watasaidiwa ili waendelee na masomo yao ya kidato cha tano?

Mhe. Spika, jengine wanalalamika sana juu ya suala la mitihani wanasema ununuzi ni bei kubwa mtihani mmoja ni shilingi 50,000 na wengi wao ni wanyonge. Kwa hivyo, tunaiomba wizara wakae ili walione hili ili tuweze kupata wanafunzi wengi wanaonunua mitihani kwa kujitegemea.

Mhe. Spika, suala jengine sasa hivi majimbo yetu yote tumefungua Skuli za Sekondari kuanzia kidato cha kwanza mpaka kidato cha nne. Lakini tunachokwama ni kwamba wakati wa mitihani *laboratory* zetu zinakua hazina vifaa, umtoe mtoto aje kufanya mtihani Lumumba ama Benbella kutoka shamba hiyo inakua inaleta usumbufu. Kwa hivyo, tunaiomba wizara na hili imelichukulia hatua gani ili kuweza na sisi kule shamba tufanye mitihani kule kule na vifaa vyote viwepo.

Mhe. Spika, sisi waheshimiwa tumesaidia sana kuchangia lakini vifaa vya *laboratory* ni ghali sana. Kwa hivyo, naomba na hili wizara kama wana jibu lolote watwambie ili tuweze kulisikia.

Mhe. Spika, suala jengine ni upungufu wa walimu, hivi sasa skuli nyingi sana hasa Mjini na Magharibi tuna upungufu sana wa walimu, bahati nzuri wenzetu Kusini na Kaskazini tayari walimu wameajiriwa lakini bado walimu wengi wamesoma na wameshakaa miaka mingi nje lakini bado kwa Mkoa wetu wa Mjini hawajaajiriwa. Kwa hivyo, naomba na hili kwenye ripoti sikuliona kama Mhe. Waziri ana lolote atwambie ili tuweze kujua na wenyewe wale waliokuweko nje wasikie wawe na matumaini gani katika kazi waliyoisomea.

Mhe. Spika, mwisho nije kwenye Wizara ya Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Wanawake, Vijana na Watoto. Hapa vile vile nilikua nina masuala kwanza naipongeza wizara kwa kuongeza mchango kwa wazee wetu wa Sebleni, Welezo, Limbani Pemba na kadhalika. Lakini ninachosikitika kwamba wameonekana wazee wale walioko katika sehemu maalum, lakini wazee wa vijijini na mitaani sijaona nyongeza yoyote. Mhe. Spika, kama ipo basi tutajiwe ili tuweze kuijua wazee wa mitaani wanachukua fedha kupitia kwenye shehia, masheha, Wakuu wa Wilaya sijaona nyongeza yoyote, kama ipo tuambiwe ili wenyewe wapate kusikia.

Mhe. Spika, suala jengine katika ukurasa wa 55 imeelezwa kuna kesi 10 za udhalilishaji wa watoto na ubakaji. Mhe. Spika, ni kwamba sikuona hatua zilizochukuliwa katika kesi hizo hivyo naomba kama kuna hatua yoyote iliyochukuliwa katika kesi hizo 10 za udhalilishaji na ubakaji kama kuna jibu lipo basi tulisikie. Mhe. Spika, baada ya hayo nimalizie *point* ya mwisho kwamba pia katika taarifa imesema kumefanywa tathmini ya watu walioumia makazini na kuweza kufanyiwa tathmini ya kulipwa haki zao. Mhe. Spika, mimi nilitaka nijue tathmini hii imeanzia mwaka gani na kama tayari wako watu wangapi wameshalipwa?

Mhe. Spika, baada ya hayo kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu la Mfenesini naunga mkono ripoti ya kamati, nakushukuru sana.

Mhe. Abdalla Mohammed Ali: Ahsante Mhe. Spika, na mimi nitatunza nidhamu nitatumia muda mchache sana kwa sababu hoja imeshazungumzwa sana Mhe. Hija wengi wamekupongeza na mimi nasema nakupongeza.

Mhe. Spika, mimi nataka kidogo niende katika hospital, ni kweli kwamba hivi sasa tuna upungufu mkubwa wa madaktari na dawa. Lakini ninachotaka kukwambia waziri ni kwamba hivi sasa yale mabango yaliyoandikwa kituo cha afya yamebadilishwa majina yamekua kituo *chafa*. Kwa sababu ukenda katika vituo vingi vya mashamba madaktari hakuna, pili hata dawa hizi ndogo ndogo pia hazipatikani na pengine unaweza kumkuta huyo daktari anatembea zaidi ya kilomita tano kufika hapo hospitali. Kwa hivyo, haya ni matatizo kusema kweli ambayo yanajitokeza kiasi kwamba wananchi wanayo sababu yakusema kwamba kituo sasa kiitwe *chafa* baadala ya kituo cha afya.

Mhe. Spika, hapa kwetu tunayo hospitali ambayo labda tunaielekeza iwe ndio hospitali ya rufaa na hospitali hii ina madaktari bingwa. Mhe. Spika, imani yangu kwamba daktari bingwa hawa utaalamu huu hawakuupatia hapa Zanzibar wamepata nje ya nchi hii. Na hii inafanyika kwa sababu ya kupunguza gharama kwa sababu wengi huwa wanataka watafute matibabu bora zaidi, lakini kwanza huwa wanaanzia kwao. Lakini jambo la kushangaza Mhe. Spika, ni kwamba hivi sasa unapokwenda Mnazi Mmoja unakutana na daktari bingwa na inapotokea wakati kwamba umepewa *refer* mara nyingi hua tunakwenda kufanya *refer* katika hospitali zilizoko Bara aidha, utatakiwa ufanye vipimo au uonane na daktari.

Mhe. Spika, lakini unapofika Bara hata kama umepata maelekezo ya daktari kutoka huku kwetu unakutia yale maelekezo yote hayathaminiwi, kiasi kwamba yule mwananchi anapata gharama ya mara mbili. Mhe. Spika, sijui hii hawa madaktari wetu bingwa kwa nini ikafikia hatua ya kwamba ripoti yao ikifika katika hospitali zilizoko Bara zinakua hazitambuliki, sijui ni kwa sababu gani? Kwa hivyo, ningemuomba Mhe. Waziri suala hili akaliangalia kwa kina je, ni sababu gani kwa sababu wananchi wetu wanafanya vipimo mara mbili gharama zinakua kubwa sana. Kwa hivyo, kama ni hivyo bora aende moja kwa moja hata akifika Bara anajua mimi nafanya kipimo halafu narudia nyumbani.

Mhe. Spika, jengine ni kwamba tuna chuo chetu cha afya, chuo hiki hapo nyuma kabla ya mwaka mmoja ada yake ilikua ni karibu 250,000 lakini hivi sasa ada hii imeruka sana imefika mpaka 650,000 kiasi kwamba 400,000 imeongezeka na tunaowatarajia kuingia hapa hawana mikopo ni watoto wa wakulima na wafanyakazi ndio sisi ambacho kipato chetu ni kidogo. Kwa hivyo, ningeomba akaiangali hii kama kuna uwezekano basi hii ada ikapungua zaidi.

Mhe. Spika, sasa hivi nije kwenye Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali. Mhe. Spika, wizara hii ina michango mengi sana na michango hii hua wanabebeshwa walimu. Hivi sasa tuna sherehe za elimu bila ya malipo, na sherehe hizi hua zinaambatana na mambo mengi yakiwemo michezo kutoka eneo moja kwenda jengine. Lakini katika kuchangia michezo hii jukumu kubwa wanabebeshwa walimu wanatakiwa wachangie safari za wanafunzi kwa mfano wanapotoka Bubwisudi wanakwenda Bwejuu basi mwalimu ndiye anayetakiwa achangie masuala yale.
Mhe. Spika, katika hili pia utakutia kuna ujenzi wa mabanda mara nyingi wanatakiwa wafanye *initiative* wao walimu wenyewe. Kwa hivyo, kama ni kuanzisha banda jipya la chekechea basi walimu ndio wanaotakiwa mwanzo waanze wao kuchangia. Kwa hivyo, huu ni mzigo kwa wao naomba tuangalie masuala haya na tujue hatma ya kuwapeleka. Lakini pia kuna ile siku ambayo tunaita siku ya walimu duniani, kuna wengine huwa wanaondoka kutoka sehemu moja ya nchi wanakwenda sehemu nyengine. Pia na wao huwa wanatakiwa wajilipie gharama za siku hii, lakini siku ya chakula duniani sijui kama wale watu wa Wizara ya Kilimo wao wanakua wanachangia, lakini walimu ndio wanaobeba mzigo mkubwa.

Mhe. Spika, nakuja sasa katika uhamisho wa walimu mara nyingi hua unafanywa bila ya kuzingatia mwalimu na fani yake. Mara nyingi unaweza kusikia mwalimu ameshazoeleka na fani yake katika skuli ile na umuhimu wake, lakini unakutia mara moja mwalimu yule kaondoka na amepelekwa katika skuli nyengine mbali na pale anapofanya kazi. Hii mara nyengine inakua ni usumbufu tuangalie mwalimu kutoka hapa akenda akasomesha Donge inakua ni usumbufu kupata gari mapema akawahi kufika mapema sio rahisi.

Mhe. Spika, pia katika hilo kuna uhamisho wa walimu hasa walimu wa kike au pengine na walimu wa kiume. Mhe. Spika, katika mila zetu kuna kuoa na kuoelewa, sasa walimu wengi wanakua wanapoingia katika ndoa inakua uhamisho ni mgumu sana. Kwa hivyo, wale waliosomea mambo ya udaktari sijui Mhe. Waziri wa Afya anajua kuna mambo yanaitwa *neuroses* sasa haya yakikukumba si kweli kwamba utafanya kazi katika hali ya kawaida. Kwa hivyo, ningeomba Mhe. Waziri masuala haya akayaona kwa uimarishaji wa hizo skuli zetu kwa sababu mwalimu kama mume wake yuko Pemba yeye yuko hapa amehamishwa kwa sababu ya kazi za ulinzi na usalama, si rahisi kwamba ataweza kufanya kazi zake kama kawaida.

Mhe. Spika, lakini katika hiyo hiyo sekta ya walimu tunasema kwamba tunataka kuongeza kunyanyua kiwango cha walimu hasa kupata walimu wa sayansi. Lakini naona hii kama inasemwa tu hatujakua na mpangilio maalum na hatujakua na utaratibu wa kusema kwamba sasa tunaelekea kupata walimu wa sayansi, imebakia kama ni maneno tu.

Mhe. Spika, ukiangalia jadweli la wanafunzi au walimu ambao wameingia katika Chuo cha SUZA mara hii ni walimu 47 tu ambao watachukua fani ya sayansi, lakini walimu 163 wataingia katika fani ya sanaa. Hii ni dalili tosha kuonesha kwamba *preparation* yetu yakufanya kwamba tunataka tupate walimu wa sayansi bado imebakia katika midomo tu. Kwa hivyo, ningemuomba Mhe. Waziri masuala haya akayaangalia kama kweli tunataka kuingia katika mfumo huu wa kupata walimu wenye fani ya sayansi.

Mhe. Spika, mimi naona nisikupotezee muda kuna wengine wanataka kuja kuchangia kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Mkoani nawapongeza walioandaa ripoti hii, ahsante sana.

Mhe. Mahmoud Mohammed Mussa: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa muda mfupi sana kuchangia katika maelekezo ya kamati hii. Mhe. Spika, kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kutokana na uwezo aliotujaalia lakini pia namshukuru Makamo Mwenyekiti ambaye amewasilisha maelekezo haya ya kamati yake na kwa kweli maelekezo yalikua ni mazuri sana, na ningeliomba mawaziri husika waangalie maoni ya kamati ambayo yalikua yana malengo na madhumuni mazuri sana kwa lengo la kuendeleza wizara zetu katika nchi yetu. Kwa kweli kama tutakwenda vizuri na maelekezo haya ya kamati basi tutafika mahala ambapo kila mmoja wetu alikua anapatarajia.

Mhe. Spika, mimi nikija katika ukurasa wa 37 kuna maelekezo kwamba wizara imeagizwa kufuata sheria ya kazi yakuwapatia likizo walimu kila mwaka pamoja na maposho yao badala ya kuendelea na mfumo uliopo sasa wakuwapatia maposho walimu kila baada ya miaka mitatu. Mhe. Spika, kusema kweli kipindi cha miaka mitatu ni kipindi kirefu sana kwa mwalimu ambaye hali yake kama tunavyoielewa kwa hivyo ningelitilia msisitizo zaidi ili tuangalie namna gani yakuweza kuwasaidia walimu hawa na kuweza kupata manufaa na kufanya kazi zao kwa ufanisi mzuri zaidi.

Mhe. Spika, sehemu ya pili nilikua nataka kuelezewa tu ni sababu zipi zilizopelekea katika mradi wa kuimarisha elimu ya ufundi ambapo tumeona kwamba kumetengwa pesa milioni mia nne, lakini matumizi ya pesa zile ikawa ni milioni kumi tu. Kwa hivyo, ningependa kupata ufafanuzi katika hilo.

Mhe. Spika, sehemu ya mwisho kabisa kwa uharaka ule ambao nilikua nimetakiwa kufanya ni kwamba kuna eneo la ununuzi wa vifaa katika maskuli yetu kwa sasa. Mhe. Spika, ili kuweza kulinda rasilimali zetu za misitu kwa sasa ndugu zetu wale wa India wana utamaduni wa kutengeneza viti vya *plastic* ambavyo havina madhara kama vile *plastic* nyengine ambazo zinapigwa marufuku katika nchi yetu.

Nahisi kwamba wakati umefika kwa sasa wizara husika kuweza kuonana na hawa watu ambao wanashughulika na masuala ya utengenezaji wa vifaa hivi vya skuli ili tuweze kupata vikalio hivi ambavyo vitakua vina gharama ndogo na vitakavyoweza kuwasaidia wananchi wetu pamoja na kuzuia uharibifu wa mazingira katika maeneo yetu Mhe. Spika, baada ya maelekezo hayo kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kikwajuni naunga mkono maelezo ya kamati, ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii kutoa majumuisho kwa ufupi kwa wale ambao wamechangia. Kwanza kabisa namshukuru na nampongeza sana Makamo Mwenyekiti wa Kamati hii ambaye alisoma hotuba kwa niaba ya mwenyekiti, aliisoma vizuri na imefahamika. Pili nawashukuru wachangiaji wote waliochangia kwa ufupi lakini kwa uadilifu mzuri sana na kwa ufasaha mzuri na kiasi kikubwa michango iliyochangiwa nimeifahamu na sasa naomba niitolee ufafanuzi.

Mhe. Spika, kwanza kilichozungumzwa sana katika wachangiaji ilikua ni matokeo ya mtihani, matokeo ya mtihani yamewagusa sana wachangiaji lakini si wachangiaji tu lakini ni wa Zanzibari wote yamewagusa kwa sana. Mhe. Spika, hasa pale ambapo Wazanzibari wengi sana walifeli lakni pia kukawa kumetolewa adhabu ya wale waliokua na vibomu, waliokopia, waliojibu masuala ya ajabu ajabu kwa jumla wakaonekana hawa walikopia, hawafai na mitihani yao ifutwe na hatimae wazuiliwe kusoma kwa miaka mitatu, na baadae ndio warudi kusoma wafanye mitihani.

Mhe. Spika, hilo lilimgusa kila mtu na lilimgusa kila mtu kwa sababu kumfungia mwanafunzi kijana mwanamke na mwanamme miaka mitatu asisome wala asifanye mtihani ni sawa sawa na kummaliza kabisa katika ile jitihada yake kutoka chumba cha kwanza mpaka pale alipofika cha kujijengea maisha yake lakini ghafla anapata adhabu kama hii ambayo kwa kweli ni adhabu kubwa sana.

Mhe. Spika, hivi majuzi tarehe 6 tulifanya kikao cha Mheshimiwa aliyekua Waziri wa Elimu Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban akafanya kikao na Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi kutoka Tanzania Bara. Mhe. Spika, nilialikwa katika kikao hicho kwa sababu nilikua sijakabidhiwa rasmi wizara, lakini nilialikwa kwa sababu tayari nilikua nimeshatangazwa na nikaipata *orientation* nzuri sana ya mjadala uliokua unafanywa pale kati ya mawaziri wawili. Mhe. Spika, mjadala ambao haukufikia tamati lakini umefika pahala pazuri.

Mhe. Spika, ni kwamba Waziri wetu wa Elimu alizungumza *concern* yake kama nilivyoizungumza mimi sasa hivi kwamba baada ya miaka mitatu kama mtoto huyu alikua mwana mwari tayari ameshaolewa hatoachiwa mpaka miaka mitatu imalize halafu aanze kusoma, kama ni wakiume ameshakata tamaa na kadhalika. Mhe.

Spika, tulitoa maelezo marefu na ya uadilifu na mimi nilishiriki katika kutoa maelezo hayo na hatimae tukakubaliana kimsingi amelikubali mwenzetu kulipeleka katika Kamati ya Elimu ya Juu ya Mitihani ili likazungumze zaidi. Mimi binafsi sikati tamaa bado nimeshazungumza na wenzangu katika kazi ya mwanzo ya kuifanya tuifanye kazi hiyo kuhakikisha wanafunzi hawa kama kuna adhabu nyengine ya kutolewa itolewe lakini sio adhabu yakumfungia mwanafunzi miaka mitatu mfululizo asende skuli.

Mhe. Spika, hili natumai na mwenzangu huko aliko analisikia nilivyolizungumza aendelee kua msikilizaji wa maoni ya wenzake nina hakika tutakapokwenda tena mara nyengine tutafika pahala pazuri sana, tuombe Mungu hawa jamaa wasamehe kama kuna adhabu nyengine ndogo maana wamekosa hilo tukubali kabisa. Lakini mtu anayeiba kuku na kufungwa maisha nafikiri Jaji huyu kidogo atakua ana matatizo. Kwa hivyo, tutarudi kuzungumza na wenzetu na hili limechangiwa na watu wengi kwa hiyo kila aliyelichangia suala hili la mitihani nimeshalitolea ufafanuzi.

Mhe. Spika, juzi tulikua tuna mahafali pale Mwanakwerekwe C alialikwa Mhe. Makamo wa Kwanza wa Rais katika hotuba yake aliyakemea mambo ya kughushi kwa nguvu zake zote, mambo ya kwenda kwenye mitihani na vibomu aliyakemea na alitwambia Wazanzibari tuone haya na tuone aibu kufanya hivi, maana hii sio sifa ya Wazanzibari. Mimi nasema amenifungulia njia nimeshawaambia wenzangu tufanye ziara ya Mikoa yote ya Zanzibar kwenda kuzungumza na Walimu Wakuu wa Skuli za Sekondari pamoja na wazazi. Mhe. Spika, mimi nataka tujitahidi kuondosha ile dhana kwamba waliofeli kwa sababu ya ni Waislamu na waliopasi ni Wakiristo. Hiyo dhana Mhe. Makamo wa Kwanza aliizungumza vizuri sana na tuliokuwepo pale alituelimisha na tunaichukulia hatua ya kuisambaza kwa wenzetu na wao wapate taaluma.

Mhe. Spika, kuhusu SUZA imezungunzwa vizuri na wachangiaji na kwa kweli tumeshakaa kitako mimi, Waziri wa Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, China na wengine tumeshakaa kitako tunatafuta utaratibu mwengine sasa wakulijenga lile jengo la skuli ya SUZA pale Tunguu. Mhe. Spika, nina hakika tutafanikiwa na tutakapofanikiwa tutakua tumepata hatua kubwa sana na *inshaallah* Mwenyezi Mungu atatusaidia.

Mhe. Spika, kuhusu elimu ya amali imezungumzwa sana na katika jumla ya mazungumzo tumeonesha kidogo wasi wasi wa maneno ya watu wanayoyazungumza. Mhe. Spika, hata mimi niliwahi kuyasikia kama mwezi mmoja uliopita, nilisikia wananchi wanasema kwamba Chuo cha Amali hakitambuliwi na serikali na wanaopasi pale wanapasi bure tu hawapati chochote, waliniambia hebu Mhe. Waziri kalitafute hili uje utwambie.

Mhe. Spika, lakini wananiuliza hayo wakati sisi katika jimbo tumeshachukua watu 12 waliomaliza masomo ya ufundi mifereji pale Mkokotoni, tumetumia kama shilingi laki sita kuwanunulia zana na vifaa vya mifereji, tukawaomba au tukawalazimisha waunde ushirika wao wakaunda. Hawa vijana sasa hivi ni mafundi wazuri sana katika sekta yetu ya maji hapa Zanzibar, tayari wameshapata ajira, wameajiriwa wanasaidia kazi pale. Na wengine watakaokuja katika sekta nyengine wamejikusanya tutawasaidia hivyo hivyo, ili kama chuo hakiwezi kuwapa zana sisi tutajitahidi kadiri ya uwezo wetu kuwapa zana lakini ile elimu yao waliyoipata pale waitumie vizuri. Kwa hivyo, kwanza napenda kulitangaza suala hili kwamba, hakuna aliyesema kwamba Chuo cha Amali hakitambuliki au hakitambuliwi, Chuo cha Amali kinatambuliwa na serikali na mwaka huu tutajitahidi kuongeza bajeti yake kuhakikisha tunakikuza na kukiendeleza vizuri zaidi.

Jengine wizara iangalie mifumo iliyopo ya mikopo na kadhalika. Nilipokuwa natoa taarifa moja hapa ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, nilizungumza kwamba nilitaja yale maeneo ambayo tuliyapitia kutafuta fedha ili kuongeza fedha zetu tuweze kuwakopesha watu wengi. Nimeelezea vile vile kwenye serikali tutaongeza bajeti kutoka shilingi bilioni 4 zilizoko sasa tufikishe bilioni 7 mpaka 8 kwa mwaka wa fedha ujao, ili tuweze kuwasomesha au kuwasaidia wengi zaidi.

Tumezitafuta taasisi rafiki China, Misri na kadhalika, wapo waliotuangalia watatusaidia kuwalipia wanafunzi wetu wanaosoma hapa ambao wanataka mikopo, lakini wao watawalipia hapa masomo yao, lakini wapo pia waliosema watawasomesha lakini watawatoza riba wakati wa malipo yao. Hilo tumelichukua lakini bado tunaendelea nalo kulizungumza, kwa sababu kama watakubali kuwakopesha halafu walipe bila ya riba hiyo itawasaidia zaidi.

Tumekisifu Chuo cha Ualimu cha Benjamini Mkapa wamepewa pesa nzuri kidogo, na wanaendelea na ujenzi na karibu watakimaliza tofauti na kile chuo chetu cha Tunguu cha *SUZA*. Nawashukuru wale waliotupongeza au walioipongeza serikali kwa uamuzi makhsusi wa kuzijenga skuli za ghorofa katika baadhi ya maeneo. Hata swahibu wangu Mhe. Hamza Hassan ameipongeza hatua hiyo ya kuzijenga hizi skuli za ghorofa Mpendae, Kibuteni, kule Pemba nimekusahau kidogo lakini kuna eneo moja Pemba litajengwa skuli hiyo. Kwa hivyo,

jumla kutajengwa skuli saba za ghorofa katika maeneo saba ya Unguja na Pemba kwa lengo la kuendeleza taaluma na elimu yenyewe.

Mhe. Suleiman Hemed wa Konde, yeye ana uzoefu sana wa elimu alirudia yale ya kizamani kwamba, ukaguzi wa walimu haupo, walimu hawakaguliwi matokeo yake syllabus haimaliziki inabakishwa kiporo. Na wale wanaokaguliwa na ukaguzi unapofanywa taarifa hazipelekwi, kwa hivyo ukaguzi unakuwa haukukamilika. Kamati ya Wazee hasa wa Kidato cha Nne hawakushirikishwa vya kutosha, na hawashirikishwi vya kutosha katika ukaguzi, ufuatiliaji wa mitihani na kadhalika.

Hayo ni matokeo ambayo bahati nzuri tumeyazungumza kwa pamoja katika wizara, tumetengeneza programu za kuzitembelea na kuzungumza na wazee mbalimbali, na walimu wakuu, kuzungumza na walimu wa *secondary schools.* Lengo la ziara hii ni kutoa changamoto kwa walimu wetu na wazee wetu wenye watoto wanaosoma na kadhalika, kuhakikisha kwamba elimu kuipata kunatakiwa vitu vitatu vifanywe. Kwanza mwalimu awe mzuri, awe *committed;* la pili, mwanafunzi awe mzuri, awe *committed* asome; lakini la tatu, na mzazi wa mwanafunzi ashiriki.

Tumeyajadili mambo hayo matatu kwa upana na urefu wake, na sasa tuko tayari kuyafanyia kazi mara tu Baraza hili likimalizika hizo ziara zitafanywa Unguja na Pemba kama ni *orientation* yetu ya kujua hasa tatizo liko wapi, na tufanye nini ili kupunguza kufeli kwa wanafunzi wetu katika mwaka ujao na miaka mingine itayofuata.

Mhe. Spika, Mhe. Mbarouk Wadi Mussa alikuwa zaidi na masuala, kwa mfano suala la kuunda ile Kamati ya *PAC* ili kujua fedha zetu zilizopotea ambazo zinafika kama shilingi bilioni moja, hili nililitolea ufafanuzi siku ile nilipokuwa nikitoa hotuba yangu.

Mimi nawakaribisha kamati hiyo na wengine wote wanaotaka kusaidia kuzitafuta fedha hizi. Kwa sababu fedha hizi ni za walipa kodi, fedha hizi zinataka zizunguke, leo unakopeshwa wewe ukimaliza ulipe ili mwengine tupate kumkopesha. Kuna wenzetu wengine hawakututendea haki, na tutahakikisha haki inatendeka na fedha hizi zinalipwa.

Nafikiri nimalizie kwa kusema kwamba, JKU tuliombwa tuisaidie kwa sababu sasa inasomesha skuli ya sekondari yao. Mimi nadhani JKU tunaendelea kuwasaidia hivi sasa, tunawapa vitabu na zana mbali mbali za kusomeshea na tutaongeza msaada wetu si kwa JKU tu, kama alivyochangia mmoja akasema hata si vibaya sasa kuanza kuweka msukumo katika skuli za Magereza. Tufungue skuli Magereza tuwafundishe wafungwa au wanafunzi, sisi tunaita wanafunzi hatuwaiti wafungwa, wanafunzi ili yule ambaye anaondoka skuli anakuja sasa uraiani na yeye anakuja na *degree* kama yule mmoja aliyepata *degree* yake kule Tanzania Bara. Hilo tunalizingatia sana na karibu tutalianzisha.

Kwa kuokoa wakati Mhe. Spika, nimemsikia Mhe. Ali Abdalla Ali nitazingatia maoni yake, Mhe. Abdalla Mohammed nitazingatia maoni yake na Mhe. Mohammed M. Mussa nimemsikia. Mhe. Spika, naomba radhi sana wale ambao sikuwagusa katika majumuisho yangu.

Kwa mfano, Mhe. Ismail Jussa Ladhu alitoa wazo zuri na akataka nilitolee ufafanuzi, kwa sababu ya wakati Mhe. Spika, naomba radhi sana lakini tutakutana mimi na yeye na nitampa ufafanuzi wangu, na kila yule ambaye sikumgusa naomba radhi, lakini lengo lilikuwa niwaguse wote bahati mbaya muda ni mchache Mheshimiwa naomba kuwasilisha ahsante sana.

UTARATIBU

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, samahani sana Mhe. Waziri nilikuwa naomba kidogo atutolee ufafanuzi kwa sababu kuna jambo kidogo kalitolea ufafanuzi lakini halijakamilika suala la Chuo cha Mkokotoni. Hatukuzungumza kwamba sio kama elimu inayotolewa pale ni elimu ambayo inawafanya vijana wetu tayari kuwajengea uwezo wa kuweza kujitegemea, tatizo lililokuwepo pale Mheshimiwa vyeti vya chuo kile havitambuliki. Kwa taarifa tuliyokuwanayo vijana waliotoka na vyeti walivyovipata pale havikukubaliwa, na hivi sasa wanashindwa kutoa hivyo vyeti. Sasa mimi nadhani Mhe. Waziri angelijaribu kama hana uhakika vizuri angelifuatilia ili akaja akatupa majibu mazuri.

Kwa sababu Mhe. Spika, hapa tunazungumza kuna correspondence zinaendelea, unajua sasa hivi mambo ya mtandao kwamba hawa wanafunzi wenyewe ndio wanaotwambia, na kuna wanafunzi wengine karibu huu mwaka wa pili hawajapata vyeti, kuna wengine vyeti vyao wameshakwenda sehemu nyengine kujiendeleza havitambuliwi, inawezekana taaluma inatoka nzuri lakini vyetu havitambuliwi.

Mhe. Spika: Sasa Mheshimiwa huo ni utaratibu au kitu gani hicho? Mimi nadhani Mhe. Waziri ameshasema kwamba mengine yote wizara wanayafanyia kazi ni pamoja na hilo.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, naomba nami nikushukuru wewe na kuwashukuru Wajumbe wote waliochangia kutaka baadhi ya ufafanuzi na kutoa ushauri kuhusu Wizara yetu ya Afya. Kwa kuanzia naomba nimshukuru Mhe. Hija Hassan Hija, Makamo Mwenyekiti wa Kamati hii kwa uchambuzi wake wa ripoti, nadhani yeye Mheshimiwa anaifahamu Wizara ya Afya zaidi kuliko hata mimi. Kwa sababu amekuwa Mjumbe wa Kamati kwa muda mrefu, na hivi sasa kufika cheo cha Makamo Mwenyekiti.

Si vibaya kusema amekuwa akinisaidia sana, kwa sababu siku aliyokuja katika majumuisho pale wizarani akanambia babu, kwa sababu ndio anavyoniita, akasema: 'Babu, sisi mkitupa la kusema tutasema, maana ndio biashara yetu, kwa hivyo jitahidini tukose la kusema".

Mhe. Spika, nilimjibu nikamwambia kama utachokuwa unasema ni cha kweli mimi nitakushukuru, kwa sababu utakuwa unanisaidia, ametusaidia sana pamoja na kamati yake.

Mh. Spika, kwa ujumla kuna Mhe. Hija Hassan, Mhe. Suleiman Hemed, Mhe. Ismail Jussa Ladhu, Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, Mhe. Ali Abdalla Ali na mwisho Mhe. Abdalla Mohammed kama sikosei. Kwa jumla masuala mengi yaliyozungumzwa Mhe. Spika, ni ya ufafanuzi na ushauri, na mengi yameelezwa ingawa kwa ufupi katika maelezo tuliyotoa wakati wa kamati, isipokuwa ni wajibu wangu vile vile nieleze yale ambayo yanahitaji kueleweka.

Masuala kwa jumla yalikuwa ni ya aina tatu, kwanza ni udhaifu wa huduma zile zinazotakiwa zitolewe, pili upungufu wa madaktari ambao ndugu zao huo udhaifu wa huduma, tatu upungufu wa dawa na vitendea kazi ambapo ndio huzaa huo udhaifu wa huduma, na nne kwamba labda wengine hawakupewa nyongeza au hawana motisha ambapo pengine nayo inaweza kusababisha huo udhaifu wa huduma.

Mhe. Spika, kwa jumla lazima nikubali kwamba upungufu wa madaktari si suala la kumalizika muda mchache, ni suala la muda mrefu na kuchukua madaktari kutoka nchi za nje halikuanza jana au juzi, ni maisha tangu hapo tulipokuwa mwaka 1964 tumekuwa madaktari tunaomba msaada kutoka nchi za nje kuja kutusaidia. Kilichotakiwa ni kweli kwamba kila siku zikipita liwe suala hilo linapungua, sasa madaktari hawatoshi kwa sababu nyingi, muda hautoshi Mheshimiwa lakini ningelieleza.

Kuna suala la wale wanaozeeka, tumeshafanya *man power survey* ya Wizara ya Afya, kwa kweli hali si nzuri kwa sababu wale wazee wanaomaliza muda wao ni wengi kuliko wale vijana ambao wanaingia. Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora anajua kwamba kila mara huwa tunamuomba madaktari wengine wanamaliza muda watuongezee muda, ili waendelee kuwepo. Kwa hivyo, hii hali anayoisema Mhe. Abdalla Mohammed, ya kwamba vituo vyengine vina upungufu ni kweli kwa sababu hiyo, wengine wanamaliza muda inabidi tumwambie Mhe.Waziri wa Utumishi awaache waendelee kwa sababu waliokuwepo hawatoshi.

Lakini vile vile juzi nilipokuwa najibu swali hapa kuhusu madaktari, ni kwamba kusomesha tunajitahidi sana na naomba Mhe. Suleiman Hemed nimwambie kile Chuo cha Mbweni hakitoi ma-*specialist* kile kinatoa wale wafanyakazi wa kati, ma-*nurse*, ma- *pharmacist* na watu wa aina hiyo, madaktari wanasomeshwa nchi za nje, na hivi sasa ndio tuna hicho chuo chetu cha madaktari wanaosomeshwa na wa Cuba ambayo nayo nitaeleza baadae. Kwa hivyo, juhudi za kuwasomesha zinafanywa, lakini wengine wakishasomeshwa ndio wanajiona mtamu sasa anatukimbia.

Juzi nilieleza kwa urefu na Mhe. Mwanasheria Mkuu anajua kwamba, tunajaribu turejeshe ile sheria kwamba, kama mtu tumemsomesha kwa pesa za serikali awe na wajibu basi angalau kutulipa halafu ndio aondoke au afanye kazi muda fulani kabla ya kuondoka. Na kama ametoroka huko kwa kujiona yeye ni bora, basi itabidi wazee wake hapa walipe kwa sababu inakuwa kila siku kama tunaotia maji kwenye pakacha hayajai na sababu ni sisi, na ni kweli Mhe. Spika, ni sisi.

Leo nilikuwa nazungumza na Dr. Malik kuna *specialist* alisomeshwa kwa kazi maalum amepelekwa Nairobi *hundred percentage* amelipiwa na serikali mbali wale niliowasema juzi wa nusu kaputi, kaja hapa mwaka mmoja tukimtegemea pale kwenye *department* ya watoto, basi hivi hivi tu, tunamkuta hayupo. Ni kweli inawezekana kwamba mazingira hayamridhishi lakini hata alipokuwa akisoma vile vile mazingira hayakuridhisha tumemsaidia, sasa angalau basi wangekaa wakatusaidia kwa muda halafu wakaondoka. Lakini nilitoa mfano huo Mhe. Spika, unajua kwamba sisi tulikuwa tukilipwa *gross* hapa. Kwa hivyo kuna sababu

nyingi, kuna waliozeeka, kuna wanaokimbia, kuna wanaoacha kazi kwa njia za taratibu, kwa hivyo kila tukisomesha wengine wanapungua na ni suala la muda mrefu. Ningeomba niliseme hivyo nisichukue muda zaidi.

Lakini maoni ya Waheshimiwa tunayazingatia, na tutarekebisha pale tunapoweza na kama maslahi vile vile serikali imejaribu, mishahara imerekebishwa, hivi sasa tuna mazungumzo na Wizara ya Utumishi kuwapa maslahi yao madaktari hata kama si vile inavyostahiki lakini kama zile alivyosema Mhe. Ismail Jussa *night call* au *special allowance* kwa kazi maalum. Tunaendelea kuzungumza naye ili tupate kuwasaidia, nao wajione kwamba wapo wanafanya linalofaa.

Kuna suala la Hospitali ya Wagonjwa wa Akili kwamba hakuna dawa za kutosha. Kwa kweli hakuna dawa ghali Mhe. Spika kama dawa za wagonjwa wa akili, na bahati mbaya si kitu cha kufurahia kwamba kila siku wagonjwa wa akili wanaongezeka. Zamani tulikuwa tunasema wagonjwa wa akili wamerogwa ndugu zetu kapewa jini na babu yake au kapata tu jini, siku hizi wagonjwa wa akili ni wa kujitakia, jamaa anapiga unga mpaka unamshinda anachanganyikiwa wote wanaletwa kule.

Kwa hivyo ule uwezo wa kuwahudumia ni mdogo zaidi kuliko ule wingi wao. Hiyo si sababu ya kutosha lakini ni kweli kwamba dawa za Idara ya Wagonjwa wa Akili ni ghali na wagonjwa ni wengi, mbali ya wale wanaokuja pale wengine tunawahudumia kwa *out reach* wanafuatwa huko, lakini tunajitahidi kama tunavyoweza.

Mhe. Ismail Jussa kuna watu kutoka nje wanasaidia. Ni sawa, lakini kuna wengine vile vile wanatumia ule udhaifu wa wagonjwa wa akili kutaka kupata manufaa yao, *is very unfortunate* na tumegundua kesi hiyo mmoja tukamwambia aa, hawa kuwa wagonjwa si kuwa wewe utajirike. Lakini tumepata misaada ya kutosha, majengo yamejengwa, hivi ninavyosema nadhani leo kontena la *furniture* kwa ajili ya ofisi mpya pale linatoka, leo nimetia saini ya kuomba msamaha wa kulipishwa kodi kwa ajili ya *furniture* zifungwe na lile jengo nitawakaribisha tuje tulifungue na kule ndani kumejengwa jiko jipya na kuna wodi nyengine zimejengwa kule. Kila tunapopata nafasi tunafanya wajibu wetu, tunaomba wale wanaowajua wengine waje watusaidie katika masuala haya.

Vifo vya akina mama na watoto limeelezwa hilo na hili lina matatizo mawili, lina matatizo kwamba ndani lazima tujitahidi wasife, lakini vile vile kuna ile miradi ya MDG ambayo inataka tufike *target* fulani. Kwa hivyo, linatupa changamoto kali sana na juzi tu amekuja yule mama mmoja ambaye anasimamia mambo ya *population*, amekwenda, ameeleza, ameona, tumemueleza matatizo yetu, bado kweli huduma za mama waja wazito na wazazi haziridhishi, lakini moja katika *challenge* ambazo kama ile ya *ICU* na hii inaninyima usingizi.

Mhe. Spika, hii inaninyima usingizi kwa sababu na sisi vile vile tumezaliwa, na kama tungekuwa hatukupata huduma nzuri pengine tusingekuwepo hapa. Kwa hivyo, tuna wajibu kwa mama zetu kama vile wanaozaliwa wanavyowajibika kusaidiwa kwa mama zao. Hili linatusumbua sana na naendelea kulishughulikia, ni moja katika suala lililo juu ya meza yangu kwamba vipi tufanye katika kulimaliza.

Kuna masuala ya Chuo cha Mbweni, kulikuwa na masuala ya aina tatu, chuo hakitoshi. Ni kweli hakitoshi kinaendelea kupanuliwa, karibuni tumekwenda kufungua majengo pale ya *hostel* mapya, na jengine linaendelea kujengwa halijakamilika ili tuongeze hiyo idadi ya wanafunzi wanaoweza kuingia. Tunategemea ikimaliza hiyo idadi itaongezeka, lakini idadi kuongezeka maana yake walimu wawe zaidi, walimu wawe zaidi ina maana mishahara iwe zaidi, kwa hivyo ni moja linazaa jengine lakini hilo tunalishughulikia.

Kuna suala ambalo kalisema Mhe. Ismail Jussa la kuingizwa chuo. Naomba nimwambie Mhe. Jussa kwamba hali haikuwa mbaya kama ilivyokuwa, na katika wakati mgumu niliopata hakuna kama mwaka huu kuhakikisha kwamba hakuna amri zinazotoka wizarani kwenda kule kwamba huyu mchukue.

Kuna baadhi wengine humu humu walinijia nikawaambia waheshimiwa Juma Duni alipokwenda kusoma Chuo Kikuu sidhani kwamba Mzee Duni alikwenda kuonana na Mkubwa wa Chuo, nilifuata taratibu zilizowekwa nikaambiwa unastahiki kwa sababu pasi zako zinakutosheleza, tafadhili tufuate utaratibu huu.

UTARATIBU

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Spika, kanuni ya 59(1) (c) utaniruhusu kuzungumza kuweka sawa kile ambacho tumekizungumza. Tulichokizungumza Mhe. Spika, sio kwamba kuna maelekezo ya wizarani kwenda katika chuo, hiyo nakubali kwamba wamechukua hatua. Nilichozungumza ni kwamba viongozi wa chuo na

wanaohusika na kufanya uteuzi kwa wale wanaoingia pale ndio wanaotumia vibaya nafasi zao. Naomba waziri ajue hilo ahsante sana.

Mhe. Spika: Nadhani hili ni kutoa ufafanuzi tu ule unaofaa, lakini nadhani alichokuwa anakieleza waziri hapa kwamba, baadhi yetu si kutokana na wewe, baadhi yetu huwa tunakwenda tukiwaomba sasa ndio akaisema hiyo sio kwamba ana-*refer* maneno yako, isipokuwa kwa ujumla baadhi yetu viongozi tunakwenda tukimuomba kwamba asaidie. Waziri endelea.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, nashukuru kwa masahihisho hayo, nilikuwa naendelea kulieleza hili kwamba halikuwa suala rahisi, na huko chuoni tumehakikisha ndio maana nikatoa mfano kwamba hakutakiwi mtu kwenda. Huko chuoni kile chuo kina Baraza lake, sheria yake na kina utawala wake, tulichojitahidi ni kuhakikisha kwamba walimu wanafuata taratibu za utawala, mkuu wa Chuo anafuata utaratibu wa utawala na uamuzi wa mwisho unafika kwenye Baraza Kuu. Sasa inawezekana makosa hayo ndio maana nikasema sio suala la mara moja, makosa hayo yakatokea, lakini hivi sasa tumewalazimisha na wao wamekubali itakuwa njia ya kwenda mwanafunzi ni kujaza kwa kuingia kwenye kompyuta moja kwa moja. Kwa hivyo, hakuna tena lile suala la kuwa fulani kapendelewa, data zimewekwa unakuja kwenye kompyuta unaambiwa jaza data zako zinakwenda moja kwa moja zina ku-*classify.*

Naomba nieleze vile vile kwamba, pamoja na utaratibu wote huo tuliofanya *still* baada ya kwishapata watu ambao tulipata watu 600 walio *qualify* ilibidi wachukuliwe 300, wengine wakabaki, tulikwenda tukafuatilia mmoja mmoja shahada yake kwamba ni sahihi wala sio ya kughushi na kama vijana watano mpaka sita tuliwakuta wameghushi na tukasema wafukuzwe. Kwa hivyo, juhudi za kurekebisha utaratibu wa *admission* utaendelea kuwa mzuri kila siku zinapopita. Hilo ndilo nililotaka nilieleze.

Mhe. Spika, pamezungumzwa masuala mawili kuhusu *ICU*. *ICU* imezungumzwa ile kujengwa mpya na Wachina, Mhe. Waziri wa Fedha alikuwepo hapa nilitegemea angeweza kusaidia. Ninachokumbuka kwamba karibuni Serikali ya Watu wa China imetupa 50 milioni *Yuan* kwa pesa za Kimarekani ni kama shilingi milioni saba na kama sijasahau kama wiki tatu nne Mhe. Waziri wa Fedha ametia saini mkataba wa kutumia fedha hizo. Fedha hizo zilipitishwa katika vikao vya serikali na ikaamuliwa zipewe Wizara ya Afya na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, wizara mbili tu katika haja ya kuona kwamba zile ahadi za serikali zilizowekwa zinatekelezwa. Ninavyoamini na nilivyomsikia mwenzangu kwa pamoja katika matumizi ya fedha hizo zitakazokuja Wizara ya Afya ni kujenga *ICU*.

Mhe. Spika, ile ya zamani ambayo tuliahidi kwamba itengenezwe hapa, kwa taarifa ya wajumbe vifaa vinaendelea kufungwa hivi sasa, baada ya uagiziaji ambao kidogo ulichukua muda na kuna taratibu. Moja katika ugumu wa kutumia fedha za serikali ni kwamba huku unaambiwa tumia huku unaambiwa fuata sheria ya *tender*, hii sheria ya *tender* hii *Allahu Akbar* unaweza ukamaliza mwaka hujamaliza taratibu. Lakini nina furaha kusema kwamba vifaa vinaendelea kufungwa na Mhe. Makame Mshimba alishindwa kuthubutu kusema ilikuwa ni *monitors* ambazo daktari akikaa hapa kule anaweza kuona jinsi ya mgonjwa anavyoendelea kwa sababu inakuwa na sauti ile inalia kwii, kwii, ukisikia kwiiii ina maana mambo mabaya.

Kwa hivyo, nilitaka kulielezea hilo Mhe. Spika, kwamba shughuli hiyo inakwenda mashine za kufunga mitambo ya kusambaza *oxygen,* hatukusudii hivi sasa ukitaka kumtibu mgonjwa wa *ICU* unaichukua ile *cylinder* nzima Mheshimiwa kama unayekwenda kufanya *welding*. Kwa kweli haifurahishi na si vizuri, maana mara nyengine iko ghorofa ya pili inabidi ipandishwe iende ghorofa ya tatu. Tunakusudia kutia *in funnel system* kama vile unavyofungua mfereji, ili akiwepo mgonjwa kuna *pipe* moja kwa moja inakwenda kwenye mwili wake anasaidiwa.

Hilo lilikuwa limalizike mwezi wa Julai kila kitu kilikuwa tayari, lakini utaratibu mpya wa kuagiza vitu kule Serikali ya Muungano ambayo ndio ile *contract* ya Tanzania *Oxygen* iliyopata kufanya hivyo, inabidi vile vitu vinavyoletwa vichekiwe huko huko kabla havijaja kwa sababu ya *quality control.* Sasa kidogo vinaweza kuchelewa, lakini vile vya kwenye *theatre* tu vyenyewe vinafungwa hivi sasa. Kwa hivyo, naomba hili niwaeleze Waheshimiwa Wajumbe.

Mhe. Spika, kuna suala la fedha za ukimwi kwamba kuna malalamiko wengine wanasema zinatumiwa vibaya na wakubwa. Taarifa hapa imeeleza kwamba taarifa zile zinawakilishwa kwenye Wizara ya Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo katika Mpango wa *MTEF (Medium Term Expenditure Framework).*

Huwezi kupata pesa nyengine za wafadhili hasa hizi za ukimwi na zile za malaria, kama *auditors* hawakuja wenyewe kutoka nje wakathibitisha kwamba zile zilivyotumika ndivyo ilivyotakiwa. Kwa hivyo, Wizara ya

Fedha inapelekewa hizi taarifa watu wanaruhusiwa na sisi hatuna matatizo waje watu wa *auditing* wazicheki kama vile inavyotakiwa. Lakini tunaomba kuhakikisha kwamba, hatuwezi kupewa pesa nyengine za ukimwi na miradi hii kama wenyewe hawakuridhika kwamba zimetumika ilivyotakiwa.

Mhe. Spika, vyandarua haviui alitoka tu mmoja na mwenye raha zake kutaka kutuparaganya, alipotoka msikitini alfajiri akaanzisha hiyo ikaanza kutembea kwenye simu kila mmoja akampelekea ujumbe mwenzake lakini haikuwa sahihi kufanya hivyo na tulimtafuta mpaka tukampata tukamwita tukamwambia sasa tupe aliyekufa kwa chandarua au vyenginevyo tunakushtaki. Alikaribia kutoka mikojo tukaona adabu imetosha tukamuachia. Vyandarua haviui, vyandarua vimetiwa dawa.

Mhe. Spika, kuhusu nyongeza za mshahara Mhe. Makame Mshimba Mbarouk bado tunathibitisha kwamba takriban watu wote wameingizwa katika mfumo mpya, na bado naendelea mbele ya Mhe. Waziri, kama kuna mtu hajapata haki yake au hajaridhika hajazuiliwa kuendelea kutuletea taarifa hizo. Wale ambao wote waliotuletea taarifa tumefikisha Wizarani na Katibu Mkuu ameshughulikia madai yao na watu wengi wamepata haja zao. Sasa kama kuna sehemu ya ufundi wana malalamiko isingekuwa vizuri kukwambia wewe kwanza kabla hawajaja Wizarani.

Mhe. Spika, Mhe. Makame Mshimba Mbarouk amekuwa kila mara anamzungumza mfanyakazi huyu aliyefukuzwa naomba nimwambie mambo mawili. Kwanza kama ikiwezekana kesho aje nae yeye mwenyewe ofisini kwangu. Mhe. Spika, samahani kule kwetu tunasema imekuwa ndwele, na ndwele lazima imalizwe isiwe ndwele tena. Ninachokumbuka mfanyakazi huyu kesi yake sisi kama Wizara tuliifikisha Wizara ya Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Utumishi wamejibu nini hatujajua siwezi kulithibitisha. Lakini kama ni suala hilo basi twende mpaka kwa Katibu Mkuu au Waziri tulijue limefika wapi limalizike, na kama anastahiki kupewa haki zake apewe kama hastahiki ajibiwe, lakini haiwezi kuwa kila siku mfanyakazi mmoja huyu.

Mhe. Spika, Mhe. Ali Abdalla Ali amezungumza habari ya taka za hospitali tulilizungumza juzi hapa kwamba tumelifikisha serikalini na tumeomba nchi nyengine kama Ujerumani tumeshapitisha watusaidie linahitaji dola 200,000 limalizwe. *Mortuary* ndogo tumeagizwa na serikali kwamba ijengwe kubwa hasa baada ya kutokea haya maafa ya meli yaliyotokea.

Kwa kawaida Waswahili maiti akifa huwa ana mali zaidi kuliko akiwa mzima, si kawaida kulazwa pale siku moja siku ya pili Waswahili wamemchukua, pengine anakufa damu haijatulia keshazikwa. Lakini kutokana na hii kuzingatia hali ya ajali inavyotokea ambayo haiagi, tumeagizwa na serikali ijengwe kubwa na tunategemea kuingiza kwenye makisio yetu ya mwaka unaofuata kulizingatia hilo.

Mhe. Spika, la mwisho ningeomba kueleza mambo mawili kuhusu ukusanyaji wa mapato. Ukusanyaji wa mapato kweli ni mdogo na pakubwa palipotegemewa ilikuwa ni hospitali ya Mnazi Mmoja. Kwa wastani taarifa niliyopewa na wenzangu wa Mnazi Mmoja hazijazidi milioni 25 kwa mwezi, ambazo kwa kwetu tunasema ni kiduchu kuweza kuhimili yale mahitaji ya hospitali nzima.

Ukiacha pesa hizi kuna pesa nyengine wanapata kutoka kwenye *DANIDA*, na zile zinazotolewa pesa hazijawa nyingi na ndio maana hii hapa ikaonekana asilimia iko chini mno, tunategemea labda kila muda ukienda zinaweza kuongezeka.

Lakini tatizo moja ambalo halijapata ufumbuzi tuliambiwa tutapewa wahasibu kama wanane, hatujapewa bado nadhani labda na wao watu wa Wizara ya Fedha wana matatizo hayo. Pia tulitegemea iwe masaa 24 wawe pale watu wanaokusanya pesa wapo, uwezo huo haujakuwepo, kwa hivyo mara nyengine ikifika saa 10:00 yule mwenye zamu ya asubuhi inamuishia tena mnajua hali ya mambo yalivyo. Lakini kama leo tutaongezewa wafanyakazi wale wa Fedha, basi huenda na makusanyo yakaongezeka na lile suala la *cost sharing* nalo tunalimalizia.

Mhe. Spika, naomba nimalize suala la Mhe. Makame Mshimba Mbarouk kuhusu ugonjwa wa kisukari. Mhe. Spika, katika watu ambao wana taasisi iliyokamilika ni wagonjwa wa kisukari, wana *NGO* yao, wana Katibu, wana Mwenyekiti, wanahudumiwa na daktari wao mkubwa ni yule Dk. Faiza Kassim Suleiman na ndiye anayewaongoza.

Mhe. Spika, sukari ni mmoja katika ugonjwa unaoitwa *NCD (Non Communicable Diseases)*, kumetoka *resolution* Umoja wa Mataifa kwamba, suala hili lipewe kipaumbele kwa sababu sasa maradhi ya kuambukiza ni machache zaidi kuliko haya ambayo si ya kuambukiza. Hivi sasa tumeshafungua akaunti maalum, na kuna

visenti fulani tayari tumefadhiliwa na taasisi moja kwamba suala la *NCD* lipate nguvu zaidi na lisimamiwe zaidi, na sasa tunatafuta ofisa maalum awe ni *desk* kuliendeleza hili.

Mhe. Spika, inawezekana kabisa wengine sikuwajibu moja kwa moja naomba wanisamehe, lakini niliona nitoe maelezo haya kwa ufupi. Mhe. Spika, nashukuru sana.

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Wanawake na Watoto: Mhe. Spika, kwanza nikushukuru kwa kunipatia nafasi hii na mimi niweze kuchangia kupitia Kamati hii ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii. Mhe. Spika, pili sina budi niwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wote wa kamati hii.

Mhe. Spika, nataka nikwambie kwamba, mafanikio tuliyoyapata ambayo kamati imeyaeleza yanatokana sana na ushauri na mchango unaotokana na kamati hii. Kwa hivyo, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa kamati hii na sote Wizara kwa kauli moja tunasema ahsanteni sana na tutaendelea kushirikiana. Mhe. Spika, pia sina budi kuwashukuru wale wote waliotuchangia sisi katika Wizara yetu hii ya Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Wanawake na Watoto. *(Makofi)*

Mhe. Spika, sasa naomba kujibu masuala mbali mbali kama hivi ifuatavyo. Nataka nianze na kujibu suala la skauti. Mhe. Spika, Wizara bado inalo suala hili la skauti, na tumeshawasiliana na Mkuu wa Skauti Zanzibar kwamba tukutane kwa pamoja ili tuweze kuendeleza na kufufua skauti tulionao hapa Zanzibar. Hilo la kwanza.

Mhe. Spika, nikiendelea nataka nijibu juu ya suala la watoto walioko gerezani. Mhe. Spika, kulingana na Sheria ya Mtoto iliyopitishwa hivi karibuni imetutaka Wizara ya Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Wanawake na Watoto tuhakikishe kwamba tunajenga majengo maalum ya watoto wanaotenda matendo yanayosababisha kwenda Chuo cha Mafunzo, sambamba na ujenzi wa Mahkama za Watoto zitakazoendeshwa kwa kutumia vigezo vinavyolingana na hali zao. Kwa hivyo, Mhe. Spika, wakati wowote sisi tukipata uwezo tutajenga magereza na serikali nadhani itasaidia hasa hawa watoto.

Mhe. Spika, kuhusu uanzishwaji wa vyuo vya mafunzo vya watoto. Mhe. Spika, tayari watoto wameshatenganishwa na watu wazima kwa taarifa ya kikao hichi. Kuna mpango unaoendelea wa kuangalia ni jinsi gani wanaweza kujengewa eneo la magereza yao hao watoto.

Mhe. Spika, nikiendelea nataka nizungumzie kuhusu suala la wazee wa mitaani. Sisi katika Wizara yetu tunahusika sana na wazee ambao wamewekwa na wanatunzwa na serikali ndio tunawapa posho la shilingi 40,000. Lakini sasa hivi tuna mpango wa kuandaa sera ya hifadhi ya jamii ya wazee, inawezekana katika kuandaa sera hii hawa wazee walioko nje sina uhakika huenda kwamba pengine baadae tukawa nao, lakini kwa sasa hivi wako nje ya wizara.

Mhe. Spika, kuhusu suala la udhalilishaji anasema jambo hili hadi sasa mbona hajaliona matokeo yake kupitia kwenye majimbo na kadhalika. Mhe. Spika, suala hili la udhalilishaji tunalifanyia kazi sana Wizara yetu, na sasa hivi tumo katika hatua ya kufanya utafiti ili tuone tatizo hili uzito wake ukoje na ufumbuzi wake mwisho wake utakuwaje. Kwa sababu watu wanaendelea tu kuwadhalilisha watoto na watu wazima wanawake pamoja na hatua zote tunazochukua za kuwaelimisha na kuwaambia jamani suala hili si zuri na likitokea basi tuseme tusilifiche, lakini mambo haya bado yapo. Kwa hivyo, tunaangalia sasa hivi tumetafuta wataalamu katika Wizara yetu ambao tutajumuika kwa pamoja kuona suala la utafiti litatueleza uzito wa jambo hili litafikia kiasi gani.

Mhe. Spika, nataka nimalizie kwa Mahkama za Watoto. Mhe. Spika, tathmini ya kuangalia haki za watoto zinasikilizwa kwa taratibu zisizowaogopesha watoto imeshafanyika, yaani sasa hivi *juvenile cases* zipo na zinafanya kazi. Kwa mashirikiano na wadau utaratibu wa kuweka *camera* maalum ya kumrekodi mtoto anapopigwa au anapofanyiwa matatizo yoyote yale akihojiwa basi asiogope wala asiwe na wasi wasi wowote. Lakini pamoja na hayo, mimi ninalotaka kusema kwamba jamani tujitahidini hili suala la udhalilishaji ni zito katika nchi yetu, na watu wanalichukulia kijuu juu sana.

Mhe. Spika, naomba uniachie nitoe mfano mmoja mzuri wa udhalilishaji uliotokea Mkoani Pemba. Kule kuna mtoto alifanyiwa vitendo vibaya sana, *alirarulіwa* mbele na nyuma na askari polisi. Lakini kwa bahati nzuri mimi napenda nichukue nafasi hii nimpongeze Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Kusini Pemba, hatua ya kwanza aliyochukua ni kuhakikisha kwamba askari yule anamfukuza kazi hafai, hatua ya pili ni kumuweka gerezani. Sasa tatizo kubwa tunalolipata sisi hasa ni hapa Unguja, Pemba jamaa mmoja alikuwa mlinzi nae usiku analinda akapita mtoto akambaka akafungwa nae miaka kumi sijui.

Mhe. Spika, hapa kesi zinaonekana wazi wazi lakini matokeo yake hazihukumiwi, tatizo kubwa hukumu bado hatujaipata. Nahangaika, na Mwenyezi Mungu akitujaalia tutahangaika mpaka siku moja mtu mmoja hapa angalau aende zake huko ndani na yeye akaone mambo.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo naomba kukushukuru tena, na nasema naunga mkono ripoti hii ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii mia juu ya mia. Ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwa kuwa muda ulio mbele yetu hautoshi kukamilisha shughuli zetu tulizozipanga leo, kwa hivyo naliomba Baraza lako tukufu liweke kando kanuni ya muda, ili tuweze kumaliza shughuli zilizo mbele yetu. Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Spika: Niwahoji Waheshimiwa Wajumbe wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Waziri wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda.

Mhe. Hija Hassan Hija (Kny: Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii): Mhe. Spika, naomba nikushukuru kwa mara ya pili na nimshukuru Mhe. Waziri kwa kunigaia muda wake mfupi ambao naomba nitumie kama dakika kumi ili niweze kutoa majumuisho ya jumla kwenye hoja hii ya kamati.

Mhe. Spika, ripoti yetu imechangiwa na wajumbe 11 ikiwa ni Mawaziri watatu na Wajumbe wanane. Naomba niwataje wajumbe waliochangia kama ifuatavyo:

1. Mhe. Suleiman Hemed Khamis
2. Mhe. Ismail Jussa Ladhu
3. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
4. Mhe. Mbarouk Wadi Mussa
5. Mhe. Hamza Hassan Juma
6. Mhe. Ali Abdalla Ali
7. Mhe. Abdalla Mohammed Ali
8. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa
9. Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali
10. Mhe. Waziri wa Afya
11. Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Wanawake na Watoto

Mhe. Spika, baada ya kuwataja hao naomba leo nikupe siri ambayo sijakupa katika maisha yangu. Mhe. Spika, kamati yako unapotutuma kwenye Wizara hizi tatu tumekuwa na mashirikiano makubwa sana ndani ya Wizara hizi, na kama kuna maksi basi ningetoa maksi ya kwanza kwa Waziri wa Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Wanawake na Watoto kwa sababu hatujawahi kwenda kwenye ziara ya kamati tukamkosa yeye na wajumbe wake. Pia nafasi ya pili ningewapa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali. Lakini mara zote tumekuwa tukishindwa kuwapata wajumbe wa Wizara ya Afya, na leo naomba uangalie kule juu hakuna mtendaji hata mmoja wa Wizara hiyo aliyesikiliza ripoti yetu. Huu ni ushahidi kwamba Wizara ya Afya mara zote wamekuwa na tatizo la kusikiliza ripoti zetu. *(Makofi)*

Kwa hivyo, Mhe. Spika, sisi taarifa hizi kimsingi huwa tunampa Waziri, lakini tunawapa watendaji wa serikali. Sasa yale ambayo yamechangiwa hapa Waziri ameyasikia lakini watendaji hakuna aliyesikia. Sasa huu ni udhaifu na hii ni siri ninayokupa mara zote tumekuwa na tatizo la Wizara ya Afya katika watendaji wake.
Mhe. Spika, baada ya siri hiyo sasa naomba nisaidie ufafanuzi kwa baadhi ya mambo ambayo yameelezwa. Kwanza kabisa suala la fedha za miradi ya uchumi kutoonesha kwenye Bajeti ya Serikali. Mhe. Spika, kamati yangu inakiri udhaifu huu kwamba watendaji wa Wizara ya Afya mara zote wamekuwa wakijenga hoja kwamba fedha za miradi ya ukimwi ni fedha ya wafadhili na wao hawaoni haja ya kuoneshwa kwenye Bajeti ya Serikali. Lakini msingi wa fedha hizi ni fedha za umma nazo zimeidhinishwa kwenye Bajeti ya Serikali ya Zanzibar.

Mhe. Spika, hoja ya pili ambayo nilitaka nitoe ufafanuzi ni utaratibu wa kupatikana wanafunzi wa Chuo cha Afya Mbweni, Mhe. Waziri hili amelizungumza vizuri matatizo yaliyokuwepo, lakini sasa kuna utaratibu wa kompyuta mambo yote yatakaa sawa. Hoja ya tatu ambayo Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali pia ameijibu ni suala zima la matatizo ya fedha kutotimiza malengo yake.

Mhe. Spika, kwa kweli tatizo kubwa hapa ni fedha. *SUZA* wanahitaji zaidi ya shilingi bilioni 26, serikali imewapatia bilioni 4 hawana uwezo wa kutekeleza majukumu kwa fedha ndogo. Kwa hivyo, hoja ya hapa ni fedha.

Mhe. Spika, tatizo jengine ni hoteli iliyopo Skuli ya Forodhani, naomba nikiri kwamba hili ni jambo jipya na kamati yangu itachukua changamoto hiyo kuifuatilia hoteli hii ni ya nani.

Mhe. Spika, jengine ambalo ningetaka nizungumze kwa upana wake ni tatizo la *scheme of service* ya Mamlaka ya Mafunzo ya Amali ambayo Mhe. Mbarouk Wadi Mussa amezungumza kwamba kuna matatizo ya matumizi ya Fedha.

Mhe. Spika, kweli kuna tatizo katika eneo hili, na kwa mantiki hiyo ambayo wafanyakazi hawajalipwa fedha mbele ya kamati yamewasilishwa, na naomba niwaahidi wajumbe wangu kwamba kamati yangu itafuatilia ili kupata ukweli. Hatuwezi kuacha malalamiko ya wafanyakazi bila ya kulipwa haki zao tukawavumilia lazima tufuatilie.

Mhe. Spika, hoja nyengine ni fedha za *scale levy*, hoja hii ambayo Wizara ya Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo mara zote tumekuwa tukiwaambia kwamba fedha hii inatolewa na washirika wa maendeleo wakiwemo waajiri binafsi, lakini Wizara ya Fedha yenyewe wameshindwa kutoa fedha hii na kuipeleka katika Mamlaka ya Mafunzo ya Amali. Mhe. Spika, pia hii ni hoja ambayo kamati yangu imekusudia kuifuatilia.

Mhe. Spika, hoja nyengine ni fedha za deni la Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu. Namshukuru sana Mhe. Waziri kwa kukubali kwamba kuna haja ya kuwasaidia ili shilingi bilioni 8 hizi ambazo zimekopeshwa ziweze kurejea serikalini kwa ajili ya kuwasaidia watu wengine.

Mhe. Spika, jambo la mwisho ambalo ni la jumla katika Wizara zangu zote tatu, naomba nitoe kilio kwa niaba ya Wizara zangu kwamba Wizara zangu zote tatu zina tatizo la ufinyu wa bajeti, hatuwezi kuwa na elimu ya maana, hatuwezi kuwa na afya ya maana, hatuwezi kuwa na maendeleo ya jamii ya maana bila ya kuwepo kwa fungu kubwa la Bajeti ya Serikali. Nachukua nafasi hii kwa niaba ya wajumbe wangu kuiomba Serikali Kuu kwamba Wizara zangu ziongezewe Bajeti Kuu, ili waweze kupata ufanisi wa shughuli zao. Mhe. Spika, nakushukuru naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Baada ya majumuisho hayo basi, sasa Waheshimiwa Wajumbe niwahoji wale wanaopokea ripoti wanyanyue mikono, wanaokataa, waliopokea wameshinda. Waheshimiwa Wajumbe ripoti imepokelewa na iko tayari sasa kufanyiwa kazi na serikali.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, muda wetu uko finyu kidogo, kwa hivyo nafikiri tutumie muda huu na hasa kwa utaratibu wa kesho. Nafikiri ripoti hii ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ingesomwa ili kesho tukenda kwenye michango moja kwa moja. Kwa kukubali huko basi nimuombe Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala.

Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala: Mhe. Spika, napenda kuchukua nafasi hii kutanguliza shukrani zangu za dhati kwa Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Baraza lako tukufu katika hali ya uzima na afya njema, ili kuwasilisha muhtasari wa ripoti ya utekelezaji wa shughuli za serikali kuanzia Julai hadi Disemba kwa mwaka 2011/2012 kwa mujibu wa kanuni ya 106 (14) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi Toleo la 2011.

Mhe. Spika, pili napenda kukushukuru wewe binafsi, kwa kunipa nafasi hii adimu na adhimu kuweza kuwasilisha taarifa ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, katika kufuatilia utekelezaji wa shughuli za serikali kama ambavyo imeelezwa hapo kabla.

Mhe. Spika, pia napenda niwashukuru Mawaziri wote wawili, ambao Wizara zao ziko chini ya kamati yetu pamoja na watendaji wao kwa namna moja au nyengine ya kushirikiana na kamati, iliwezesha kwa kiasi kikubwa kutekeleza majukumu yake ya ufuatiliaji kama ambavyo imeelezwa na kanuni ya 111 ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi Zanzibar.

Mhe. Spika, nitakuwa mtovu wa nidhamu kama sikutoa pongezi kwa wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Katiba, Sheria na Utawala ya Baraza la Wawakilishi, kwa ushirikiano wao mkubwa waliouonesha wakati wote

ambao kamati ikifanya kazi za ufuatiliaji, ikiwa ni pamoja na kuhoji serikali na kutoa maoni yao kwa lengo la kuimarisha utendaji na kukuza uwajibikaji katika serikali.

Mhe. Spika, naomba kuwataja wajumbe hao kama ifuatavyo:

1. Mhe. Ali Abdalla Ali - Mwenyekiti
2. Mhe. Panya Ali Abdalla - Makamo Mwenyekiti
3. Mhe. Ismail Jussa Ladhu - Mjumbe
4. Mhe. Mussa Ali Hassan - Mjumbe
5. Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak - Mjumbe
6. Mhe. Suleiman Hemed Khamis- Mjumbe
7. Mhe. Wanu Hafidh Ameir - Mjumbe
8. Ndg. Nassra Awadh Salmin - Katibu
9. Mhe. Abubakar Mahmoud Iddi - Katibu

Mhe. Spika, Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala imepewa mamlaka ya kusimamia jumla ya Wizara mbili za Serikali, pamoja na Idara na Taasisi ziliomo katika Wizara ile. Wizara zenyewe ni kama zifuatazo:

1. Wizara ya Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora.
2. Wizara ya Katiba na Sheria.

Mhe. Spika, kiujumla kamati yetu imeridhishwa na utendaji wa Wizara hizi. Hata hivyo, bado kuna kasoro ndogo ndogo za kiutendaji kwa baadhi ya taasisi zilizomo kwenye wizara hizi, ambapo juhudi zaidi zinapaswa zichukuliwe na taasisi hizo ili kukuza ufanisi wa utendaji kwa nia ya kutekeleza mafanikio ya taasisi hizo na maendeleo katika nchi yetu kwa ujumla.
Mhe. Spika, Wizara ya Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Wizara hii imefanikiwa kutekeleza majukumu yake mbali mbali kupitia idara zake zilizomo ndani ya Wizara.

Miongoni mwa majukumu hayo ni kama yafuatayo:

Idara ya Mipango Sera na Utafiti

Mhe. Spika, kamati yetu imeridhishwa na utekelezaji wa Idara ya Mipango Sera na Utafiti, miongoni mwa mambo muhimu ambayo idara hii inaweza kuyatekeleza ni pamoja na kutayarisha rasimu ya sera ya usafiri yenye lengo la kuweka mfumo bora wa usafiri, utakaohakikisha kuwepo kwa utaratibu na miongozo ya upatikanaji wa huduma ya usafiri kwa watumishi wa umma.

Kuwawekea mazingira mazuri watumishi wa umma na wananchi wa Zanzibar kwa jumla kwa kutayarisha muongozo wa hadidu rejea na sera ya mawasiliano *electronic.*

Mhe. Spika, kamati inashauri kuharakishwa kwa mfumo wa bima ya afya, kuwa mfumo huu ndio mkombozi wa upatikanaji wa huduma bora. Hivyo, wizara hii kwa kushirikiana na Wizara ya Afya pamoja na mfuko wa hifadhi ya jamii Zanzibar, ichukue hatua ya haraka katika kufanikisha suala hili

Idara ya Uendeshaji na Utumishi

Mhe. Spika, katika ufuatiliaji wa kazi za kamati pia imekagua na kutoa maelezo katika idara ya uendeshaji na utumishi na imeridhishwa na utekelezaji wa majukumu yake.

Hata hivyo, kamati inashauri wizara izidishe mawasiliano na wizara nyengine za SMZ ili kutoa taarifa za mabadiliko ya mageuzi ya utumishi serikalini, ili kupunguza migongano na uwekaji uwiano katika utumishi.

Idara ya Utawala Bora

Mhe. Spika, kwa upande wa idara ya utawala bora katika kuwajengea wananchi juu ya dhana nzima ya uelewa wa utawala bora. Elimu ya Uraia wa Umma imepitia katika vipindi vya redio, semina na makongamano imetolewa kwa jumla ya vipindi 7 vimerushwa hewani kupitia Shirika la Utangazaji Zanzibar.

Hata hivyo, kamati inaelekeza kuingiza katika mitaala ya skuli somo la haki za binadamu na utawala bora.

Idara ya Nyaraka na Kumbukumbu za Taifa

Mhe. Spika, Idara ya Nyaraka na Kumbukumbu za Taifa imeweza kuwahudumia watafiti mabli mbali waliofika idarani hapo. Idara imewahudumia jumla ya watafiti 133, ambao kati ya hao 109 ni Watanzania na 26 ni wageni kutoka nchi mbali mbali za nje. Vile vile idara katika kuimarisha usalama wa jengo la nyaraka, maofisa wawili wamefanya ziara ya kikazi huko Tanzania Bara, kwa lengo la kukagua mitambo ya CCTV, inayotarajiwa kufungwa katika Ofisi ya Nyaraka hapa Unguja.

Mhe. Spika, kamati inaishauri serikali na wizara kwa jumla, itafute eneo kwa lengo la kujenga ofisi mpya hasa tukizingatia kwamba eneo liliopo sasa ni dogo na pia limezungukwa na majengo ya wananchi. Pia wizara ifanye jitihada ya kuitafutia Idara ya Nyaraka Pemba jengo la ofisi.

Chuo cha Utawala wa Umma

Mhe. Spika, kamati inapongeza Chuo cha Utawala wa Umma kwa kufanikisha na kufanya marekebisho ya mitaala ya masomo ya diploma rasilimali watu. Utawala wa umma na mtaala wa mafunzo ya cheti cha sheria.

Kamati inaomba serikali kuvishajihisha vyuo viliopo hapa nchini ili kutoa mafunzo ya cheti katika fani mbali mbali, ili kuipunguzia serikali gharama ya kuwapeleka vijana nje ya nchi.

Tume ya Utumishi Serikalini

Mhe. Spika, katika kutekeleza majukumu yake, tume ya utumishi serikalini imefanikiwa kukaa kikao cha uzinduzi wa bodi ya tume ya utumishi serikalini. Kununua vifaa mbali mbali vya ofisi, kufanya mikutano mbali mbali ya kuelimisha watumishi wa serikali juu ya sheria mpya ya utumishi wa umma.

Idara ya Mafunzo na Maendeleo ya Watumishi

Mhe. Spika, idara ya mafunzo na maendeleo ya watumishi katika kutekeleza majukumu yake, imeratibu mafunzo ya muda mrefu na mfupi, ambapo jumla ya watumishi 95 wamehudhuria mafunzo mafupi nchini India, watumishi 18 nchini Korea, Singapore 4, China 9, Japan 2, Tanzania Bara 24. Kwa upande wa mafunzo ya Stashahada ya Pili, China 2, Japan 1 na India 2.

Idara ya Miundo ya Taasisi

Mhe. Spika, katika kutekeleza malengo ya idara ya miundo ya taasisi, utumishi wa umma na maslahi ya wafanyakazi, imepitia miundo ya utumishi na kuifanyia marekebisho ili kuwawezesha watumishi kutambua daraja zao, mishahara wanayostahiki na utaratibu wa kupandishwa vyeo. Kamati inaunga mkono suala hili kwani ndio chachu ya mabadiliko ya utumishi serikalini.

Idara ya Mipango na Rasilimali Watu

Mhe. Spika, idara ya mipango na rasilimali watu katika kutekeleza majukumu yake imefanikiwa kuimarisha kumbukumbu za watumishi wa umma ambapo idara imeanzisha mfumo wa uwekaji taarifa rasilimali watu, ambayo itawasaidia kuweka na kutumia taarifa hizo katika masuala ya kiutumishi, zikiwemo mahitaji ya watumishi, taaluma zao na kuweka makisio ya wastaafu pamoja na mwelekeo na mafao yao.

Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali

Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali inaendelea na majukumu yake ya kazi za ukaguzi kwa mwaka 2009/2010, katika taasisi mbali mbali za serikali na kufuata muongozo wa ukaguzi. Aidha, ripoti ya ukaguzi ya mwaka 2008/2009 zimekamilika na tayari zimewasilishwa serikalini.

Ofisi Kuu Pemba

Mhe. Spika, Ofisi Kuu Pemba miongoni mwa malengo yaliyotekelezwa na Ofisi Kuu Pemba, ni pamoja na kuandaa semina na sera ya mawasiliano ya serikali kwa njia ya *electronic* na *e- government* na kutayarisha mpango wa matumizi ya muda wa kati *MTEF* wa ofisi.

Wizara ya Katiba na Sheria

Mhe. Spika, wizara hii kwa kupitia taasisi zake mbali mbali katika kipindi hichi wametekeleza yafuatayo.

Idara ya Mipango na Sera

Kamati yetu imeelezwa na Idara ya Mipango na Sera kua pamoja na mambo mengine imeanza maandalizi ya kuandaa mikakati ya utekelezaji wa sera ya NGOs, kwa kutangaza tenda kwa ajili ya kutafuta mshauri mwelekezi. Pia kuimarisha ubadilishaji wa taarifa kutoa elimu kwa umma juu ya sekta ya sheria. Vimeandaliwa vipindi ambavyo vinarushwa hewani hivi karibuni.

Idara ya Utumishi na Uendeshaji

Mhe. Spika, Idara ya Utumishi na Uendeshaji imeendelea kuratibu utekelezaji wa *programme* za mageuzi ya watumishi wa umma kwa upande wa wizara. Kuratibu utekelezaji wa *programme* za mageuzi ya watumishi wa umma kwa upande wa wizara vile vile.

Mhe. Spika, idara hii inakabiliwa na changamoto ya kutoingiziwa fedha za ujenzi wa jengo la wizara kwa wakati, kutokana na hili Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala inaomba serikali iingizie fedha idara kwa ujenzi huo kwa wakati, kwa sababu fedha za idara hiyo tayari zipo.

Mahakama

Mhe. Spika, miongoni mwa malengo yaliyotekelezwa na mahakama ni kuimarisha majengo ya mahakama kuendelea na hatua za kuanzisha mahakama ya biashara, kujenga mazingira bora ya utendaji kazi, kurahisisha mwenendo wa kesi na kuimarisha mahakama ya kazi.

Ofisi ya Mwanasheria Mkuu

Mhe. Spika, miongoni mwa mambo ambayo Ofisi ya Mwanasheria Mkuu inaendelea kuyatekeleza ni pamoja na kuendeleza kazi ya ujenzi wa makao makuu ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu katika hatua ya pili, imeanza kunyanyua kuta ya ghorofa ya kwanza na pia imetayarisha waraka wa mapendekezo ya muundo wa kitengo cha mikataba na kuwasilisha waraka wizarani.

Kamati ya makatibu wakuu na Baraza la Mapinduzi ili kujadili.

Tume ya Kurekebisha Sheria

Mhe. Spika, kamati imetoa pongezi kwa hatua ilizofikiwa na utekelezaji wa tume ya kurekebisha sheria kwa kuzipitia sheria pamoja na kupendekeza marekebisho yanayohitajika kufanyiwa, ambapo sera ya watu wenye ulemavu nambari 9 ya mwaka 2006 na sheria ya ushahidi sura nambari 5 ya mwaka 1917 imerekebishwa, marekebisho yao yanaendelea na tayari *issue paper* zimesambazwa kwa wadau.

Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka

Mhe. Spika, Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka inaendelea na majukumu yake ya kuimarisha na kuendeleza uwezo wa ofisi kiutendaji, kiuendeshaji kazi za rasilimali watu, kuimarisha miundombinu ya ofisi na kukamilisha makaazi kwa wanasheria huko Chake Chake, pamoja na kituo cha mafunzo cha utafiti wa sheria na kuanza kazi kwa kituo cha mafunzo ya utafiti wa sheria.

Ofisi ya Mrajisi MKuu

Mhe. Spika, Ofisi ya Mrajisi Mkuu inaendelea na majukumu yake ya kuendelea kufanyia marekebisho mifumo ya sheria zinazoongoza usajili, kuimarisha usimamizi wa usajili wa tathnia ya mali za ubunifu na kuandaa

vipindi vya TV na redio vinavyoshajihisha umuhimu kwa wasajili wa tathnia ya mali ya ubunifu pamoja na kurekebisha kasoro za utendaji zilizocheleweshwa kupatikana kutokana na vyeti vya kudumu na vyenginevyo.

Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana

Mhe. Spika, kamati yetu imeridhishwa na utekelezaji wa Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana, miongoni mwa mambo muhimu ambayo idara hii inaweza kuyatekeleza ni pamoja na kuimarisha mfumo wa usimamizi wa mali za wakfu na amana, kuweka mfumo bora wa shughuli za zaka.

Katika kufanikisha hili mshauri mwelekezi ameajiriwa kwa ajili ya kuandaa kanuni za muundo wa mkakati wa miongozi ya utekelezaji wa diwani ya zaka na kuendeleza watendaji kuimarisha mazingira ya kazi.

Ofisi ya Mufti

Mhe. Spika, Ofisi ya Mufti imeweza kusimamia ipaswavyo harakati za kujenga umoja wa ushirikiano wa Waislamu. Afisi pia imepokea migogoro 19 inayohusu mashamba na ndoa, kwa kupatia ufumbuzi unaofaa. Kati ya hiyo migogoro miwili ya mashamba imepelekwa mahakamani kwa kupatiwa ufumbuzi zaidi.

Hata hivyo, kamati inashauri kupatiwa ufumbuzi migogoro iliyopo sasa baina ya sheria ya ardhi na ya wakfu.

Ofisi ya Msajili wa Haki Miliki

Mhe. Spika, Ofisi ya Msajili wa Haki Miliki inaendelea na majukumu ya kuongeza kasi ya ulipaji wa kazi ya haki miliki kwa watumiaji wa biashara na kuimarisha uwezo wa ofisi kiutendaji kwa kuandaa mafunzo ya muda mfupi kwa watendaji wa ofisi, pamoja na kununua dhana za kufanyia kazi na mawasiliano, kama mafuta, umeme, mtandao na vifaa vya kuandikia.

Aidha, Ofisi ya Msajili wa Haki Miliki inakabiliwa na changamoto mbali mbali zikiwemo za kushindwa kuandaa rasimu ya awali ya marekebisho ya sheria ya hati miliki nambari 14 ya mwaka 2003 na uhaba wa watendaji hususani Pemba.

Afisi Kuu Pemba

Mhe. Spika, miongoni mwa malengo yaliyotekelezwa na Ofisi Kuu Pemba ni pamoja na kuandaa mikutano iliyowashirikisha wafanyakazi wa kawaida, pamoja na maofisa watumishi wa idara kuhusiana na suala zima la maslahi ya wafanyakazi na marekebisho ya mishahara, kwa mujibu wa toleo jipya la serikali, pamoja na kusikiliza maoni au malalamiko yao mbali mbali kuhusiana na uimarishaji na uendeshaji wa ofisi kwa lengo la kuyapatia ufumbuzi na kujenga ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yao.

Hitimisho

Mhe. Spika, naomba nimalizie muhutasari huu kwa kuwashukuru wajumbe wote kwa kunisikiliza kwa makini, ili na wao waweze kuchangia. Aidha, napenda kukushukuru wewe binafsi kwa mara ya pili kwa kuniruhusu kuwasilisha mukhtasari wa taarifa na kufuatilia utekelezaji wa shughuli za kamati ya Katiba, Sheria na Utawala.

Mhe. Spika, baada ya hayo naomba kuwasilisha.

Mhe. Spika: Nawashukuru Waheshimiwa Wajumbe, pia nakushukuru Mhe. Mwenyekiti kwa kuwasilisha ripoti hiyo. Kesho penye majaaliwa tutaendelea kujadili ripoti hii, baada ya kipindi cha maswali kama kawaida. Sasa niakhirishe kikao hiki mpaka kesho tarehe 17/04/2012, saa 3:00 za asubuhi.

(Saa 2:10 usiku Baraza liliakhirishwa mpaka
tarehe 17/04/2012 saa 3:00 za asubuhi)